# UCHANGANUZI LINGANISHI WA MATINI YA HOTUBA ZA KISIASA KUHUSU UFISADI KUANZIA MWAKA 2015 HADI 2020


**NA:**

**FELIX SHIMENGA MWOREH**

**C50/CE/34020/2016**


**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**JUNI, 2025**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kikuu kingine kwa mahitaji ya kuhitimu shahada yoyote.

Sahihi........................................ Tarehe 23/06/2025........................................

**Felix Shimenga Mworeh**

**C50/CE/34020/2016**

Tasnifu hii imewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yangu kama msimamizi.

Sahihi........................................ Tarehe 23-06-2025........................................

**Dkt. Boniface Ngugi**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

## TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa baba yangu Alfred Mworeh Ambani na marehemu mamangu Anjeline Lihabi. Hakika singeweza kuafikia haya yote bila ya kuwajibika kwenu katika kunilea na kunielimisha.

Asanteni sana!

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, ukakamavu na uwezo wa kiuchumi ulioniwezesha kufanikisha safari hii ya masomo katika kiwango cha uzamili. Shukrani za dhati pia kwa msimamizi wangu; Dkt. Bonface Ngugi kwa ushauri wake wa hekima na uelekezi wa kipekee. Mungu akubariki. Aidha, nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili kwa mafunzo na ushauri tangu niliposajiliwa kuanza shahada yangu ya uzamili mwaka wa 2016. Ningependa kuwataja wafuatao kwa namna walivyoyagusa maisha yangu kiusomi na kiulezi: Dkt. Chacha Mwita, Dkt. Pamela Ngugi, Dkt. Jacktone Onyango, Dkt. Miriam Osore, Dkt. Joseph Gakuo, Dkt. Edwin Masinde, Prof. Kitula King'ei na Dkt. Steve Kamau. Siwezi kumsahau mke wangu mpendwa Winnie Muhindi, wanangu Lucius Ambani na Lance Warren kwa kuniruhusu kutengana nao nilipokuwa chuoni. Nawapeni shukrani za dhati pia babangu Alfred Mworeh na ndugu zangu Longinus Raleigh, Edwin Ambani, Caroline Kadogo, Jackline Addah, Silas Ambani, Brian Spira na Faith Shalu kwa kunifaa kwa hali na mali bila kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioshiriki nao madarasa ya uzamili; Ustadh James Wanga Wagabi, Nyariki E. Nyariki, Calvince Omondi, Eunice Obatu, Samuel Wachira, Caroline Munyau, Mercy Mwende, Janet Muela, Hellen Wairimu, Angeline Wamaitha na Jacob Kirimi.

## IKISIRI

Hotuba ni chombo muhimu kinachotumiwa na wanasiasa kuwasilisha sera zao, itikadi na hata kukemea maovu yanayotendeka katika jamii. Nchini Kenya, suala la ufisadi ni mojawapo ya maovu yanayotekelezwa na baadhi ya viongozi na wananchi. Kwa sababu hii, wanasiasa wengi huliangazia suala hili katika hotuba zao kwa umma kama mojawapo ya mikakati ya kuupiga vita ufisadi. Wao hutumia lugha kwa njia ya kipekee wanapoangazia suala hili hususan vita dhidi yake. Hii basi ndiyo sababu utafiti huu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi nchini Kenya. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (UUH) iliyoasisiwa na Fairclough katika kuchanganua hotuba sita za viongozi wawili wa kisiasa wa nchi ya Kenya kuhusu ufisadi ili kuchanganua na kulinganisha namna matini ya hotuba za kisiasa yanavyoshughulikia suala la ufisadi, kubainisha athari za hotuba hizi kwa wananchi na kisha kubaini mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba hizi. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa kuwachagua wasailiwa na pia viongozi wa kisiasa ambao matini za hotuba zao zilichanganuliwa na kulinganishwa. Wanasiasa teule ni wale ambao wameliangazia suala hili la ufisadi kwa kina, hivyo basi hotuba zao ni faafu katika utafiti huu. Ili kupata matini za hotuba za kisiasa ambazo zilitumiwa kama data katika utafiti huu, mtafiti alikusanya video kutoka mtandao wa "YouTube". Data nyingine pia ilikusanywa nyanjani kupitia hojaji funge ya likati na hojaji wazi ili kubaini athari na mielekeo ya wananchi wa Kenya kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi. Mtafiti alizisikiliza na kuzinukuu hotuba teule kisha kuchanganua na kulinganisha matini zake. Aidha, data ilichanganuliwa na kulinganishwa kwa kutumia majedwali, takwimu na maelezo na kisha matokeo yake kuwasilishwa vilevile kwa kutumia maelezo, majedwali na takwimu. Matokeo ya utafiti huu yatawapa wananchi ama matumaini kuwa hotuba za kisiasa zinatekeleza dhima kuu katika vita dhidi ya ufisadi au ni gumzo tupu. Utafiti huu pia utachangia katika taaluma ya uchanganuzi matini ya hotuba za kisiasa zinazolenga maudhui teule kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki.

# ABSTRACT

Political speeches are important tools used by politicians to present their policies, ideologies and even to condemn evils committed in the society. In Kenya, corruption is one of the evils committed by some leaders and citizens. Because of this, many politicians address the issue of corruption in their political speeches to the public as one of the strategies of fighting the vice. They use the language uniquely to address the issue of corruption in Kenya especially the fight against it. This therefore is the reason why this research purposed to critically analyse and compare political speeches in Kenya that focus on the issue of corruption. This research was guided by Critical Discourse Analysis (CDA) theory by Fairclough in analyzing six political speech texts of two Kenyan political leaders on corruption to critically analyze and compare how texts in political speeches address the issue of corruption, the effects of these speeches on the citizens and also find out the attitude of the citizens on these speeches. The researcher employed purposive type of sampling in selecting the politicians whose speeches were studied as well as the respondents in the field research. The selected politicians are those who have highlighted the issue so much in their speeches therefore, their speeches were much relevant to this research. To get the political speeches on corruption which was the required data in this research, the researcher downloaded video clips of the speeches from YouTube. He listened to the speeches, noted them down then analysed and compared the texts in line with the research objectives. The researcher also collected another data in the field by use of likert scale closed questionare as well as an open ended questionare to ascertain the effects and attitude of the citizens on political speeches that focus on the issue of corruption. However, the data was analysed and comparisons made using tables, figures and explanations. The findings were presented also using tables, figures and explanations. The researcher believes that the findings of this research will either give people hope that political speeches play a significant role in the fight against corruption or they are just empty rhetorics. The researcher also believed this research would make a significant contribution to the field of critical discourse analysis of political speeches that gives special focus on a specific theme using Critical Discourse Analysis theory.

## ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA

| | | |
|---|---|---|
| **ANC** | **:** | Amani National Congress |
| **CDA** | **:** | Critical Discourse Analysis |
| **DCI** | **:** | Directorate of Criminal Investigation |
| **EACC** | **:** | Ethics and Anti-Corruption Commission |
| **F** | **:** | Frequency (Idadi jumla ya wahojiwa) |
| **FBI** | **:** | Federal Bureau of Investigation |
| **ISIS** | **:** | Islamic State of Iraq and Syria |
| **NACOSTI** | **:** | National Commission for Science Technology and Innovation |
| **NYS** | **:** | National Youth Service |
| **NT** | : | Nimekataa |
| **NTK** | : | Nimekataa kabisa |
| **ODM** | **:** | Orange Democratic Movement |
| **RO** | **:** | Raila Odinga |
| **STK** | **:** | Sikatai wala kukubali |
| **T.I** | **:** | Transparency International |
| **UK** | : | Uhuru Kenyatta |
| **UM** | **:** | Uchanganuzi Matini |
| **UUH** | **:** | Uchanganuzi Usemi Hakiki |

## ORODHA YA MAJEDWALI NA PAI- CHATI


Jedwali 3.1: Istilahi Maalumu ........ 53

Jedwali 3.2: Matumizi ya Viwakilishi Nafsi ya Kwanza Umoja na Wingi ........ 56

Jedwali 3.3: Matumizi ya Nafsi ya Pili ........ 59

Jedwali 3.4: Matumizi ya Nafsi ya Tatu Wingi ........ 60

Jedwali 3.5 Usawiri wa Wananchi kama wenye Mamlaka Makuu ........ 61

Jedwali 3.6: Matumizi ya Toni ya Kejeli ........ 63

Jedwali 3.7: Lugha yenye Takwimu ........ 65

Jedwali 3.8: Matumizi ya Lugha yenye Matumaini ........ 67

Jedwali 3.9: Toni ya Kukashifu ........ 68

Jedwali 3.10: Kuchanganya Msimbo ........ 70

Jedwali 3.11: Matumizi ya Mbinu ya Kinaya ........ 71

Jedwali 3.12:Matumizi ya Takriri ........ 73

Jedwali 3.13: Matumizi ya Maswali Balagha ........ 75

Jedwali 3.14: Virai Shawishi ........ 77

Jedwali 4.1 Athari za Hotuba kwa Wafisadi ........ 82

Pai chati 4.1 Athari za Hotuba kwa Wafisadi ........ 83

Jedwali 4.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi ........ 85

Pai-chati 4.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi ........ 86

Jedwali 4.3 Sababu za Kubadili Nia ........ 86

Jedwali 4.4 Sababu za Kutobadili Nia ........ 87

4.1.3 Athari kwa Wananchi Wanaopiga Vita Ufisadi ........ 88

Jedwali 4.5 Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi ........ 88

Pai-chati 4.3 Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi ........ 89

Jedwali 4.6 Sababu za Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi ........ 89

Jedwali 4.7 Sababu za Kupinga Hotuba Zisiangazie Ufisadi ........ 90

Jedwali 4.8 Hali ya Wanasiasa Kutoangazia Ufisadi ........................................................ 91

Jedwali 4.9 Sababu za Kutoridhika ........................................................................ 91

Jedwali 4.10 Sababu za Kuridhika ........................................................................ 92

Jedwali 4.11Ulinganisho wa Mitazamo kuhusu Hotuba za Kisiasa ................................. 93

Jedwali 4.12 Sababu za Kufurahishwa na Hotuba za Kisiasa .......................................... 93

Jedwali 4.13 Sababu za Kuchukizwa na Hotuba za Kisiasa ............................................ 94

Jedwali 4.14 Mielekeo kuhusu Usikilizaji wa Hotuba za Kisiasa .................................... 97

Jedwali 4.15 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kuangaziwa Kila Mara ....................................... 98

Jedwali 4.16 Mielekeo kuhusu Ufanisi wa Hotuba za Kisiasa ........................................ 98

Jedwali 4.17 Mielekeo kuhusu Athari za Hotuba kwa Wafisadi ...................................... 99

Jedwali 4.18 Mielekeo kuhusu namna Ufisadi Unavyoangaziwa ................................. 100

Jedwali 4.19 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kutokemewa Nchini ........................................ 101

Jedwali 4.20 Mielekeo kuhusu Madai Yanayoangaziwa kwenye Hotuba ..................... 102

Jedwali 4.21 Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa …………………..103

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........................................ **ii**

**TABARUKU** ........................................ **ii**

**SHUKRANI** ........................................ **iv**

**IKISIRI** ........................................ **v**

**ABSTRACT** ........................................ **vi**

**ORODHA YA VIFUPISHO NA ALAMA** ........................................ **vii**

**ORODHA YA MAJEDWALI NA PAI- CHATI** ........................................ **viii**

**YALIYOMO** ........................................ **x**

**SURA YA KWANZA** ........................................ **1**

**UTANGULIZI** ........................................ **1**

**1.0 Usuli wa Mada** ........................................ 1

**1.1 Suala la Utafiti** ........................................ 3

**1.2 Malengo ya Utafiti** ........................................ 4

**1.3 Maswali ya Utafiti** ........................................ 4

**1.4 Sababu za Kuchagua Mada** ........................................ 4

**1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti** ........................................ 5

**1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada** ........................................ 7

**1.6.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu Uhakiki wa Hotuba** ........................................ 7

**1.6.2 Maandishi Jumlifu kuhusu Uhakiki wa Matini ya Hotuba za Kisiasa** .............. 9

**1.6.3 Tafiti Zilizofanywa kuhusu Uchanganuzi Matini za Hotuba za Kisiasa** .......... 11

**1.6.4 Tafiti Zilizofanywa kuhusu Uchanganuzi Linganishi wa Matini ya Hotuba za Kisiasa** ........................................ 15

**1.7 Misingi ya Kinadharia** ........................................ 18

**1.8 Mbinu za Utafiti** ........................................ 22

**1.8.1 Muundo wa Utafiti** ........ 22

**1.8.2 Eneo la Utafiti** ........ 23

**1.8.3 Uteuzi wa Sampuli** ........ 24

**1.8.4 Idadi ya Sampuli** ........ 25

**1.8.5 Masuala ya Kimaadili……26**

**1.8.6 Mbinu za Ukusanyaji Data** ........ 26

**1.8.7 Uchanganuzi wa Data** ........ 29

**1.8.8 Uwasilishaji wa Matokeo** ........ 29

**1.9.0 Hitimisho……..30**

**SURA YA PILI ........ 30**

**MATINI YA HOTUBA ZA KISIASA NA UFISADI ........ 30**

**2.0 Utangulizi** ........ 30

**2.1 Dhana ya Lugha na Matini** ........ 31

**2.2 Lugha na Siasa** ........ 34

**2.3 Dhana ya Hotuba za Kisiasa** ........ 37

**2.3.1 Sifa za Hotuba za Kisiasa** ........ 41

**2.3.2 Mamlaka katika Hotuba za Kisiasa** ........ 43

**2.4 Mielekeo na Athari za Hotuba za Kisiasa** ........ 46

**2.5 Hotuba za Kisiasa na Ufisadi** ........ 47

**2.6 Hitimisho** ........ 50

**SURA YA TATU ........ 51**

**ULINGANISHAJI WA NAMNA MATINI ZA HOTUBA ZA KISIASA ZINAVYOSHUGHULIKIA UFISADI ........ 51**

**3.0 Utangulizi** ........ 51

**3.1 Istilahi Maalumu** ........ 52

**3.2 Matumizi ya Viwakilishi vya Nafsi** ........ 55

**3.3 Kuwasawiri Wananchi kama wenye Mamlaka Makuu** ........ 61

**3.4 Matumizi ya Toni ya Kejeli**........................................................................ 63

**3.5 Lugha yenye Takwimu** ........................................................................ 64

**3.6 Lugha yenye Matumaini** ........................................................................ 67

**3.7 Toni ya Kukashifu**........................................................................ 68

**3.8 Kuchanganya Msimbo**........................................................................ 69

**3.9 Matumizi ya Kinaya** ........................................................................ 71

**3.10 Matumizi ya Takriri** ........................................................................ 72

**3.11 Matumizi ya Maswali Balagha** ........................................................................ 74

**3.12 Matumizi ya Virai Shawishi**........................................................................ 77

**3.3 Hitimisho**........................................................................ 78

**SURA YA NNE ........................................................................ 81**

**ATHARI NA MIELEKEO YA WANANCHI KUHUSU HOTUBA ZA KISIASA . 81**

**4.0 Utangulizi**........................................................................ 81

**4.1 Athari za Hotuba za Kisiasa kwa Wananchi wa Kenya**........................................ 81

**4.1.1 Athari kwa Wafisadi**........................................................................ 82

**4.1.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi**........................................ 85

**4.1.3 Athari kwa Wananchi Wanaopiga Vita Ufisadi** ........................................ 88

**4.2 Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa**........................................ 96

**4.2.1 Mielekeo kuhusu Usikilizaji wa Hotuba za Kisiasa** ........................................ 97

**4.2.2 Mielekeo kuhusu Hali ya Ufisadi Kuangaziwa Kila Mara** ........................................ 97

**4.2.3 Mielekeo kuhusu Ufanisi wa Hotuba za Kisiasa** ........................................ 98

**4.2.4 Mielekeo kuhusu Athari za Hotuba kwa Wafisadi**........................................ 99

**4.2.5 Mielekeo kuhusu Namna Ufisadi Unavyoangaziwa** ........................................ 100

**4.2.6 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kutokemewa Nchini** ........................................ 101

**4.2.7 Mielekeo kuhusu Madai Yanayoangaziwa kwenye Hotuba** ........................................ 102

**4.2.8 Muhtasari wa Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa**.................. 103

**4.3 Hitimisho**........................................................................ 105

**SURA YA TANO ........................................................................................................ 107**

**MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................... 107**

**5.0 Utangulizi**.............................................................................................................. 107

**5.1 Muhtasari**.............................................................................................................. 107

**5.2 Matokeo ya Utafiti** ................................................................................................ 109

**5.3 Mahitimisho ya Utafiti**.......................................................................................... 119

**5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi**................................................................................ 121

**MAREJELEO ............................................................................................................. 123**

**VIAMBATISHO ......................................................................................................... 129**

**Kiambatisho I: Hojaji**............................................................................................... 129

**Kiambatisho II: Vibali vya Kufanya Utafiti**............................................................... 133

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Hotuba ni maelezo maalum yanayojumuisha mawazo na maoni ya mhutubu ambayo huwasilishwa kwa hadhira katika hafla maalum kwa njia ya kusimulia au kusoma. Kwa mujibu wa Webster's New World College Dictionary, toleo la tano (2018), hotuba ni kitendo cha kuongea, kujieleza au kuwasilisha mawazo na hisia kwa kutumia matamshi. Matamshi nayo hutokana na lugha mbalimbali za binadamu. Cook (1989) anafafanua lugha kama mfumo wa sauti nasibu na ishara za kisarufi ambazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao. Kwa msingi wa maelezo haya, hotuba huwasilisha mawazo na hisia za mhutubu kuhusu yanayotendeka katika jamii yake na hotuba hizi ni lazima zitekelezwe katika lugha ambayo inaeleweka vyema na hadhira lengwa.

Crystal (1969) anaeleza kwamba, lugha katika sekta mbalimbali za kutenda kazi huibua mitindo ya kipekee. Kwa misingi hii, anaeleza kuwa kuna sajili mbalimbali za lugha kama vile; lugha ya kisiasa, lugha ya kisheria, lugha ya kidini, lugha ya kibiashara miongoni mwa nyingine. Utafiti huu ulilenga hotuba za kisiasa hivyo basi sajili lengwa ni ya lugha ya kisiasa. Siasa ni shughuli ya kijamii ambayo huweza kufafanuliwa kama kinyang'anyiro cha uongozi baina ya watawala na watawaliwa (Chilton, 2004).

Hotuba za kisiasa ni mojawapo ya kipera cha hotuba za kushawishi ambazo ni miongoni mwa aina tatu kuu za hotuba kwa mujibu wa University of Pittsburgh (2019) kama

ifuatavyo; hotuba za kuarifu (taarifa), hotuba za shughuli maalum kama vile sherehe na hotuba za kushawishi ambazo huhusisha masuala mbalimbali kama vile mabishano ya kisiasa, mijadala ya kibiashara miongoni mwa mengine. Hotuba za kisiasa ni mazungumzo yanayotolewa na wanasiasa katika miktadha ya kisiasa kuangazia masuala mbalimbali yanayoathiri jamii. Kwa mujibu wa Wilson (2001), hotuba za kisiasa ni lugha (aidha rasmi au isiyo rasmi) inayotumiwa na wanasiasa katika ulingo wa siasa wakiwa na lengo la kisiasa.

Kwa kuwa shughuli ya kisiasa hujikita ama katika msukumo wa mabadiliko au kutokana na hali fulani inayoshuhudiwa wakati huo kama anavyoeleza Chilton (2004), utafiti wetu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matini za hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi kwani ni mojawapo ya masuala yanayoangaziwa sana nchini Kenya katika kipindi hiki. Dhana ya ufisadi inaweza kufafanuliwa kama matumizi mabaya ya mamlaka au mali ya umma kwa lengo la kujifaidi au kuwafaidi jamaa na marafiki zako. Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Dunia na shirika la kimataifa la *Transparency International* (T.I), ufisadi ni matumizi mabaya ya mamlaka kwa faida za kibinafsi (World Bank, 1997; Transparency International, 2019). Ufafanuzi huu ni sawa na wa tume huru ya kupambana na ufisadi nchini Kenya ya *Ethics and Anti-Corruption Commission* (EACC) ambayo inafafanua ufisadi kama matumizi mabaya ya ofisi ya umma kujinufaisha. Katika mwaka wa 2019, Kenya iliorodheshwa nambari 137 kati ya nchi 180 duniani kwa uchache wa visa vya ufisadi kwa mujibu wa ripoti ya shirika la T.I (Transparency International, 2019). Hii ina maana kuwa Kenya ni miongoni mwa nchi zilizo na visa vingi vya ufisadi duniani. Ingawa kampeni dhidi ya ufisadi zimeendelezwa kwa miaka kadha sasa, ufisadi haujaisha wala

kupunguka kwa kiwango cha kuridhisha. Ni kwa sababu hii, utafiti wetu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matini za baadhi ya hotuba za kisiasa ili kubaini zinavyoangazia suala la ufisadi kama mkakati mojawapo wa kupiga vita ufisadi. Tulihakiki vipengee vya kimatini kama vile neno, virai, vishazi, aina za sentensi na mbinu mbalimbali za kiisimu katika hotuba teule. Kadhalika, tulichunguza athari za hotuba hizi kwa hadhira na pia mielekeo yao kuzihusu.

**1.1 Suala la Utafiti**

Hotuba za kisiasa zimetumiwa kwa muda mrefu kukemea mafisadi na vitendo vya ufisadi lakini haibainiki iwapo zina mchango wowote katika vita dhidi ya ufisadi nchini Kenya. Hii ni kwa sababu nchi imesalia kuwa miongoni mwa nchi zinazoshuhudia visa vingi vya ufisadi duniani kwa mujibu wa ripoti ya shirika la T.I ya mwaka wa 2019. Kwa hivyo ilikuwa muhimu kuchunguza na kulinganisha matini katika hotuba za baadhi ya wanasiasa kuhusu ufisadi ili kubaini iwapo hotuba zao zinachangia kwa vyovyote vile katika vita dhidi ya ufisadi. Aidha, ilikuwa muhimu pia kuchunguza jinsi hadhira inavyoathirika kutokana na hotuba hizi na vilevile kubaini mielekeo yao kuzihusu.

Fauka ya hayo, uchanganuzi matini katika hotuba za kisiasa ni uwanja uliowavutia wanaisimu wengi hasa wanaisimujamii. Majarida mengi, vitabu na hata tasnifu kuhusu uchanganuzi matini za hotuba za kisiasa zimeandikwa. Baadhi yao ni Habwe (1999, 2010), Sarfo na Krampa (2013), Musa (2015), Warambo na wenzake (2015) na Rajab, (2017). Kwa kuzingatia tafiti hizi zilizofanywa kuhusu uchanganuzi wa matini katika hotuba za kisiasa, ni dhahiri kuwa hakuna aliyechanganua na kulinganisha matini za hotuba za kisiasa kuhusu mada teule ya ufisadi nchini Kenya ingawa ufisadi ni suala ambalo limepewa

kipaumbele katika hotuba za wanasiasa hasa kuanzia mwaka wa 2015. Ni kwa sababu hii, utafiti huu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi ili kuziba pengo lililopo.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo yafuatayo: -

1. Kulinganisha namna matini ya hotuba za kisiasa yanavyoshughulikia ufisadi.
2. Kubainisha athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya.
3. Kudhihirisha mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo: -

1. Je, matini ya hotuba za kisiasa yameshughulikia vipi suala la ufisadi?
2. Hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi zina athari gani kwa wananchi wa Kenya?
3. Wananchi wana mielekeo gani kuhusu hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unatokana na ilhamu ya mtafiti kuvutiwa na jinsi wanasiasa wanavyoitumia lugha katika hotuba zao kuangazia masuala mbalimbali katika jamii kwa madhumuni maalum. Kwa kuwa ufisadi umeathiri nchi ya Kenya pakubwa, wanasiasa hujitokeza kila mara kuliangazia suala hili katika hotuba zao kwa wananchi. Takwimu kutoka shirika la T.I zinaorodhesha nchi ya Kenya miongoni mwa mataifa fisadi sana duniani (Transparency International, 2019). Kutokana na hali hii, vita dhidi ya ufisadi vimepewa kipaumbele

katika hotuba za wanasiasa nchini Kenya hasa kuanzia mwaka wa 2015 ambapo visa vya ufisadi viliripotiwa katika shirika la NYS. Kwa sababu hii, mtafiti aliona kuwa ni muhimu kuchunguza na kulinganisha matini za baadhi ya hotuba hizi ili kubaini namna zinavyoangazia suala hili.

Kwa sababu utafiti huu umo katika uwanja wa isimu, hasa isimujamii, matokeo yake yatachangia katika shehena ya maarifa katika sajili ya kisiasa na pia katika uchanganuzi wa matini ya hotuba za kisiasa kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (UUH). Aidha, yatawafaidi wanasiasa, umma na wanaoendeleza kampeni dhidi ya ufisadi kujua iwapo matumizi ya hotuba za kisiasa katika kuangazia suala la ufisadi yana athari chanya au hasi.

**1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.0, kuna aina tatu kuu za hotuba; hotuba za kuarifu, hotuba za shughuli maalum na hotuba za kushawishi. Utafiti huu ulilenga kuchanganua hotuba za kisiasa pekee ambazo ni mojawapo ya hotuba za kushawishi.

Hotuba za kisiasa huweza kuangazia masuala mbalimbali katika jamii. Masuala haya ni kama; mijadala kuhusu miradi ya maendeleo katika nchi, elimu, vita dhidi ya ugaidi, suala la umaskini, majanga kama vile ukame, ugonjwa na mafuriko, utunzaji wa mazingira, vita dhidi ya ufisadi miongoni mwa masuala mengine. Utafiti huu ulilenga suala la ufisadi pekee katika hotuba za kisiasa kwa nia ya kubaini namna wanasiasa wanavyotumia hotuba kuupiga ufisadi vita.

Utafiti huu ulidhamiria kulinganisha hotuba za wanasiasa wa Kenya peke yake ingawa kuna wanasiasa wengine watajika duniani ambao wameangazia suala hili la ufisadi kama vile Barack Obama (rais mstaafu wa Marekani), marehemu John Magufuli (aliyekuwa rais wa Tanzania) miongoni mwa wengine. Sababu ya kuchagua wanasiasa wa nchi ya Kenya ni kuwa ufisadi umeenea sana nchini Kenya kwa mujibu wa ripoti ya shirika la T.I (2019) na wanasiasa wameamua kuukabili kwa kukemea mafisadi katika hotuba zao za kila mara kwa wananchi.

Wanasiasa wanaoangazia suala la ufisadi nchini Kenya ni wengi. Kwa mfano, Rais Uhuru Kenyatta ambaye pia ni kiongozi wa chama cha kisiasa cha *Jubilee*, naibu wa Rais Wiliam Ruto, kiongozi wa upinzani Raila Odinga, Musalia Mudavadi- kiongozi wa chama cha *Amani National Congress* (ANC), wajumbe wa bunge la kitaifa na seneti, wawakilishi wa wadi mbalimbali nchini miongoni mwa wanasiasa wengine. Mtafiti alichanganua na kulinganisha hotuba za wanasiasa wawili pekee; Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga. Wawili hawa ni viongozi wa serikali na upinzani mtawalia, vyama vyao vya kisiasa vina wafuasi wengi nchini na vilevile waliliangazia sana suala hili katika hotuba zao.

Hotuba 6 zilizotolewa baina ya mwaka wa 2015 na 2020 kuhusu sakata mbili kuu za ufisadi; sakata katika shirika la NYS na sakata ya mabwawa ya Arror na Kimwarer, zilichanganuliwa. Idadi hii ya hotuba ilimpa mtafiti data ya kutosha aliyohitaji katika utafiti huu. Mtafiti alichagua kipindi hiki kwa sababu 2015 kuliripotiwa sakata kubwa ya ufisadi

katika shirika la huduma ya vijana kwa taifa la NYS na kwa sababu hii, viongozi wengi waliangazia sana sakata hii. Aidha, visa vingine vilizidi kuripotiwa baada ya sakata hii. Baadaye Machi tarehe 9 mwaka wa 2018, viongozi hawa waliamua kuzika tofauti zao na kuamua kufanya kazi pamoja ambapo vita dhidi ya ufisadi ni mojawapo ya ajenda tisa za maafikiano yao (The Star, 2019).

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Katika sehemu hii, mtafiti alishughulikia maandishi ya kijumla kuhusu uhakiki wa hotuba, maandishi jumlifu kuhusu uhakiki wa matini ya hotuba za kisiasa kisha tafiti zilizofanywa kuhusu hotuba za kisiasa.

### 1.6.1 Maandishi ya Kijumla kuhusu Uhakiki wa Hotuba

McCarthy (2000) anasema kuwa uhakiki wa usemi unahusishwa na kutafiti uhusianao baina ya lugha na miktadha ambamo unatumika. Aidha, uchambuzi wa hotuba haulengi tu ruwaza za lugha bali pia huzingatia muktadha wa matini. Kwa msingi huu, tulichanganua na kulinganisha hotuba za kisiasa kwa kuzingatia miktadha ambamo hotuba teule zilitolewa.

Mahshid (2014) akimrejelea Shabanali (2001) anaeleza dhima za uhakiki wa usemi kama ifuatavyo: kwanza ni kubainisha uhusiano baina ya mwandishi, maandishi na msomaji; ya pili ni kuainisha muundo wa ndani wa uzalishaji wa matini au mchakato wa uhakiki wa matini; ya tatu ni kubaini athari za matini na muktadha kwa usemi; nne ni kutambua matakwa spesheli ya mtayarishaji wa hotuba; tano ni kuonyesha mabadiliko ya maana

katika matini na mwisho ni kuonyesha uhusiano baina ya matini na itikadi. Dhima hizi zilimuongoza mtafiti katika uhakiki na ulinganisho wa matini za hotuba za wanasiasa teule kuhusu ufisadi hasa athari za muktadha kwa usemi.

Kuna kanuni zinazopaswa kutimizwa ili ukubalifu wa matini kama tukio la mawasiliano upatikane. Kanuni hizi ni; mshikamano, muwala, muktadha, kusudio, ukubalifu, ufahamishaji na mwingiliano wa matini (Beaugrande na Dressler, 1981). Wanaendelea kusema kuwa vigezo hivi visipotimizwa, kazi haiwezi kukubalika kama matini. Kigezo cha muwala katika usemi ndicho kinachodhihirisha kuwa makala ni matini au si matini. Kuna matini za kimazungumzo na kimaandishi. Utafiti huu ulihakiki matini za kimazungumzo na pia kuzingatia kanuni nyingine za ukubalifu wa matini kama tukio la mawasiliano kwa mujibu wa Beaugrande na Dressler.

Beaugrande na Dressler (1981) wanaeleza kuwa miktadha ya matukio ni muhimu katika ufasiri wa maana katika matini. Ufasiri wa matini hufanywa kwa njia mbili muhimu. Njia ya kwanza ni ufasiri wa kawaida ambapo uchambuzi huzingatia wakati fulani maalum, mahali, na muktadha wa usemi. Njia ya pili ni ufasiri wa kiulinganishi ambapo kitu fulani kinalinganishwa na muktadha fulani. Maoni haya ni sawa na ya Wendell (1992) anayesema kwamba, uamilifu wa lugha katika matini hukamilika ndani ya matumizi yake katika muktadha maalum. Utafiti huu ulizingatia aina hizi mbili za ufasiri wa matini katika uchambuzi wa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa kuzingatia miktadha yake, mahali na wakati au vipindi tofauti vya kisiasa.

### 1.6.2 Maandishi Jumlifu kuhusu Uhakiki wa Matini ya Hotuba za Kisiasa

Van Dijk (1993) anaeleza kuwa dhana ya uhakiki wa hotuba za kisiasa ni tata kwa kuwa ni lazima uamuzi kufanywa kwanza kuhusu ni hotuba gani zinazingatiwa kuwa za kisiasa. Ili kuukabili utata huu, anapendekeza kuwa lengo kuu liwe ni ufafanuzi wa kiutondoti kuhusu jinsi uhakiki wa hotuba za kisiasa unavyotekelezwa badala ya kulenga kupata ufafanuzi wa maana ya dhana hii. Fauka ya hayo, anasema kuwa uchanganuzi wa hotuba za kisiasa unaweza kuchukuliwa kuwa uchunguzi unaolenga kuonyesha jinsi utawala wa kisiasa unavyojengwa, kuimarishwa na kutumiwa vibaya na pia miundo tofautitofauti ya upinzani. Anaongeza kuwa uhakiki huu pia huangazia matumizi ya hotuba za kisiasa kutawala. Kwa muhtasari, uhakiki wa hotuba za kisiasa unahusisha suala la utawala na athari za kijamii zinazotokana na ukosefu wa usawa unaojengwa na utawala (Van Dijk, 1993; Fairclough, 1995). Utafiti huu ulihakiki na kulinganisha hotuba za viongozi wa kisiasa nchini Kenya na hivyo basi kutathmini uwezo wa viongozi hawa wa kuimarisha uongozi wao kwa kudhibiti visa vya ufisadi nchini.

Kwa mujibu wa Van Dijk (keshatajwa), wanasiasa ni kikundi cha watu wanaochaguliwa au kuteuliwa na hulipwa kwa kutekeleza wajibu mkuu katika siasa. Ingawa wanasiasa ni muhimu zaidi katika sayansi ya siasa na uwanja wa uhakiki wa mijadala ya kisiasa kama washiriki wakuu, wao si washiriki pekee katika siasa. Hadhira mbalimbali katika mawasiliano ya shughuli za kisiasa kama vile umma na vikundi vingine ni sharti vijumuishwe. Kwa msingi huu, anaeleza kuwa mtazamo wa kuchukulia kuwa hotuba za kisiasa zinahusishwa tu na wanasiasa pekee umepungukiwa. Anapendekeza kujumuishwa kwa wale wote wanaohusishwa na mchakato huu. Verba na wengine (1993) wanakubaliana

na maelezo haya na kuongeza kuwa shughuli za kisiasa huhusisha watu kama vile wananchi na wapiga kura; vikundi vya kutetea maslahi ya wengine kama vile waandamanaji na wapinzani miongoni mwa vikundi vingine. Hivyo basi uhakiki wa hotuba za kisiasa ni sharti uweze kuhusisha wale wote wanaochangia katika shughuli za kisiasa kando na wanasiasa. Ni kwa misingi hii, utafiti huu kando na kuchanganua na kulinganisha hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi; ulilenga pia kubainisha mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba hizo na vilevile kubainisha hotuba hizo zinavyowaathiri wananchi.

Matini ya kisiasa na miktadha yake huweza kuwa na sifa za kutekeleza malengo maalum ya kisiasa kama vile kuunda au kuathiri maamuzi ya kisiasa kama vile kutenda shughuli fulani kwa pamoja, ugawanyaji wa raslimali za jamii, kuunda au kubadilisha desturi fulani, kaida na sheria. Mijadala ya kisiasa sawa na sayansi ya kisiasa huchukuliwa kimsingi kuwa aina ya matendo ya kisiasa na mpangilio wa mchakato wa kisiasa (Van Dijk, 1985). Ingawa hii imechukuliwa kuhusisha mitagusano ya mazungumzo au dayolojia; ni wazi kuwa waandishi wa matini ya kisiasa au uandishi wa matini kwa ujumla ni aina ya matendo ya kijamii au kisiasa. Baada ya kuhakiki sifa za miktadha ya hotuba za kisiasa, uhakiki wa hotuba hizi mara nyingi utakuwa kama aina nyingine za uchanganuzi wa matini (Van Dijk, 1993). Utafiti huu ulichanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa ili kubainisha zinavyoathiri vita dhidi ya ufisadi kama sifa mojawapo ya matini ya kisiasa anayoeleza Van Dijk (1985)

Fairclough (1995) anatofautisha kati ya mamlaka ndani ya hotuba na mamlaka yanayotokana na hotuba iliyotolewa. Anaeleza kuwa mamlaka ndani ya hotuba huhusisha

hotuba na mahali ambapo mahusiano ya mamlaka hutekelezwa kwa mfano; mamlaka katika mazungumzo ya moja kwa moja, mamlaka katika tamaduni ambapo washiriki wanatoka katika makabila tofauti tofauti na mamlaka fiche ya hotuba ya wanahabari. Aidha, mamlaka inayotokana na hotuba iliyowasilishwa inahusishwa na jinsi amri za hotuba zinavyoundwa na mahusiano ya mamlaka. Kwa kuzingatia misingi hii, mamlaka ndani ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi yalichunguzwa katika utafiti huu kwa lengo la kubaini nafasi ya hotuba hizi katika kuupiga ufisadi vita.

Van Leeuwen (2008) alieleza mbinu kadha ambazo wanajamii wanaweza kutumia katika hotuba zao kama vile; mbinu ya kuwachangamsha wahusika, kuwajumuisha au kuwatenga, kuwaficha au kuwaweka wazi, uhuishaji au kutohuisha, ujumuishaji wa wahusika kama kikundi kimoja au kuwaangazia kibinafsi, kutilia mkazo maneno au virai (kusisitiza maudhui) miongoni mwa mbinu nyinginezo. Katika utafiti huu, mtafiti alilinganisha hotuba teule za wanasiasa kuhusu ufisadi ambapo vipengee mbalimbali vya kimatini vilibainishwa vikiwemo mbinu mbalimbali za kiisimu.

### 1.6.3 Tafiti Zilizofanywa kuhusu Uchanganuzi Matini za Hotuba za Kisiasa

Haugerud na Njogu (1991) walitafiti kuhusu mikutano ya kisiasa nchini Kenya. Walishikilia kwamba lugha ya kisiasa ilitumiwa na wanasiasa kama mbinu ya kuelezea ujumbe wao kwa njia tofauti ili kuwanufaisha wao wenyewe na malengo ya taifa. Utafiti huu unalingana na wetu kwa kuwa pia nao ulihakiki hotuba za kisiasa nchini Kenya. Utafiti huo basi ulikuwa wa manufaa kwenye utafiti huu katika kutathmini uwasilishaji wa ujumbe

kuhusu ufisadi katika hotuba za wanasiasa ingawa unatofautiana na wetu kwa kuwa sisi tulilinganisha matini ya hotuba za kisiasa ambazo zinaangazia mada ya ufisadi pekee.

Habwe (1999) alitafiti kuhusu hotuba za kisiasa nchini Kenya. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa wanasiasa hutumia mbinu za sitiari na maswali ya balagha katika hotuba zao. Aligundua pia kuwa maana za hotuba huwa zaidi ya maana ya maneno yanayotumiwa na kwamba wanasiasa hugeuza maana ili kutosheleza hali tofauti, matarajio na mahitaji ya hadhira yao. Katika utafiti huu, Habwe alilenga kubaini matatizo ya mshikamano, muwala na maana kipragmatiki katika matini ya hotuba teule za kisiasa katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unakaribiana na wetu kwa kuwa ulishughulikia hotuba za kisiasa nchini Kenya. Ulitusaidia katika utafiti wetu kwa kuwa unaangazia kipengele cha fani katika hotuba za kisiasa ambacho ni mojawapo ya vipengee tulivyohakiki katika matini za hotuba. Tofauti baina ya utafiti huu na wetu ni kuwa, sisi tulilenga hotuba zinazoangazia suala la ufisadi wala si maudhui yote katika hotuba za kisiasa kama alivyoshughulikia Habwe.

Adero (2005) alishughulikia uwezo wa lugha katika matini ya siasa nchini Kenya kuanzia mwaka wa 2002 hadi 2005. Alitumia nadharia ya usemi hakiki ya Fairclough (1989) kudhihirisha vile lugha hutumiwa na wanasiasa ili waweze kuonyesha itikadi zao na pia kupata mamlaka. Alibaini kuwa mtindo wa maongezi wanaotumia wanasiasa hujenga washirika wao na kubomoa wapinzani wao. Utafiti huu unakaribiana na wetu kwa kuwa unaangazia uchanganuzi wa matini ya kisiasa nchini Kenya ingawa wetu ni tofauti nao kwa sababu umeshughulikia hotuba za kisiasa zinazoangazia mada ya ufisadi na vilevile kipindi cha miaka ni tofauti. Utafiti huu wa Adero (keshatajwa) ulikuwa muhimu kwetu kwa kuwa

aliangazia uwezo wa lugha katika hotuba za kisiasa nasi tulilenga kubaini nafasi ya hotuba za kisiasa katika vita dhidi ya ufisadi hivyo basi uwezo wa lugha iliyotumiwa ulitathminiwa.

Habwe (2010) alishughulikia dayolojia katika hotuba za kisiasa nchini Kenya na uamilifu wake. Alibaini kuwa wanasiasa hutumia dayolojia kutathmini namna maoni yao yanavyopokelewa na hadhira; umaarufu wao kisiasa na pia kama mbinu ya kushirikisha hadhira ili isikinai. Utafiti wetu ulifaidika na kazi hii kwa kutathmini mbinu za kiisimu zinazotumiwa katika hotuba za kisiasa na athari zake kwa kulenga mada yetu ya ufisadi. Utafiti wetu, ingawa unahusiana na huu wa Habwe kwa kuchanganua hotuba za kisiasa, ulilenga maudhui maalum ya ufisadi ilhali wa Habwe ulilenga tu matumizi ya mbinu ya dayolojia.

Musa (2015) alichanganua hotuba za Mwalimu Nyerere ili kubaini ikiwa maudhui mahsusi na mbinu za kiisimu zinazua ushawishi katika hotuba zake kwa mujibu wa nadharia ya balagha. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kwamba kulikuwa na maudhui ya umoja wa kitaifa na wa wafanyakazi, uongozi bora, azimio la Arusha miongoni mwa mengine na baadhi ya mbinu za kiisimu kama vile maswali balagha; tashbiha, tashhisi, kinaya na uchanganyaji ndimi katika hotuba za mwalimu Nyerere. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa kuwa zote zilishughulikia hotuba za kisiasa kwa kuangazia maudhui na pia uamilifu wa hotuba za kisiasa kwa ujumla. Hata hivyo, tafiti hizi zinatofautiana kwa kuwa wetu ulilenga hotuba za wanasiasa wawili nchini Kenya kuhusu maudhui teule ya ufisadi pekee

ilhali huu wa Musa ulilenga kubaini maudhui kadhaa na mbinu mbalimbali za kiisimu katika hotuba za Nyerere.

Rajab (2017) aliangazia tathmini ya mabadiliko ya maana ya msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa siasa. Utafiti huu ulifanyika nchini Tanzania na alichanganua hotuba za kampeni za uchaguzi wa mwaka wa 2015. Aligundua kuwa, mabadiliko ya maana ya msamiati yalisababisha mabadiliko ya kisemantiki. Miongoni mwa mabadiliko haya ni kuimarika kwa maana, udhalilikaji wa maana na usogezi wa maana. Aidha aligundua pia kuwa asilimia 82.35% ya watafitiwa walikiri kuwa msamiati uliobadilika maana katika muktadha wa kisiasa unakubalika katika jamii. Utafiti huu unakaribiana na wetu kwa kuwa zote zinahusu uchunganuzi wa hotuba za kisiasa katika juhudi za kubaini zinavyowasilisha ujumbe fulani, hivyo basi matokeo ya utafiti huo yalikuwa muhimu kwetu. Tofauti ni kuwa, hotuba zinazoangaziwa ni za wanasiasa wa nchi ya Tanzania ilhali huu unaangazia hotuba za wanasiasa wa nchi ya Kenya na unalenga hasa mada teule ya ufisadi.

Obiero (2017) alichanganua na kuhakiki hotuba ya kutawazwa ya aliyekuwa Rais wa Marekani, Donald Trump. Alilenga kubaini jinsi lugha aliyotumia Trump ilivyowaweka wahusika katika makundi tofauti tofauti. Utafiti ulibaini kuwa Trump alijiweka katika nafsi ya kwanza ambayo ilidhihirisha msisitizo mkuu. Hii ilimfanya Obiero (keshatajwa) kumsawiri kama mwenye kiburi na mwenye kuzua mafarakano. Katika hotuba yake aliusawiri uongozi wa Obama kama dhaifu uliofeli kudhibiti hali mbalimbali na hivyo Marekani kukosa ushawishi dhidi ya nchi nyingine. Kwa upande mwingine, hotuba zake zilisawiri muungano wa nchi za kiislamu za Iraq na Syria wa *Islamic State of Iraq and*

*Syria* (ISIS) na Saudi Arabia kuwa na uwezo mkubwa wa kudhibiti hali zao na hivyo kudhihirisha kuwa zina uwezo mkubwa kuliko Marekani. Utafiti huu ulitusaidia katika kuhakiki lugha inayotumika katika hotuba za wanasiasa kuangazia suala maalum katika jamii. Utafiti huu ingawa unahusiana na wetu kwa kuchanganua hotuba za kisiasa, unatofautiana pia kwa kuwa mwanasiasa anayerejelewa ni kutoka nchi tofauti na pia aliangazia maudhui tofauti na tunayoangazia katika utafiti huu.

### 1.6.4 Tafiti Zilizofanywa kuhusu Uchanganuzi Linganishi wa Matini ya Hotuba za Kisiasa

Lwaitama (1988) alishughulikia mtindo wa maongezi ya wanasiasa nchini Tanzania ambapo aliwalenga marais wa hapo zamani, Mwalimu Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi. Alibaini kuwa kuna utumiaji wa viwakilishi ambao sio tu wa mtu binafsi, bali pia kutegemea muktadha husika. Mwalimu Nyerere na Mwinyi walitumia viwakilishi vya nomino katika nafsi ya kwanza kwenye miswada ya maongezi kuliko miswada iliyoandikwa. Nafsi ya pili nayo ilitumiwa nao wote walipoangazia urasimishaji wa mamlaka. Utafiti huu ulikuwa faafu kwetu kwa kuwa ulishughulikia jinsi wanasiasa wanawasilisha ujumbe wao kwa raia kwa kutumia hotuba. Hivyo ulitusaidia katika ubainishaji na ulinganishaji wa namna wanasiasa wanavyotumia hotuba kama nyenzo muhimu katika vita dhidi ya ufisadi nchini Kenya. Ingawa utafiti huu ulikuwa muhimu kwetu, unatofautiana na wetu kwa kuwa uliangazia marais wa Tanzania na wetu unaangazia viongozi wa kisiasa wa Kenya.

Lwaitama (1995) alitumia nadharia ya uhakiki wa lugha kuchunguza mtindo wa marais wa Tanzania: Rais Nyerere na Rais Mwinyi wakati wa hotuba zao. Alichunguza nomino, vitenzi na mwingiliano wa sintaksia katika hotuba za marais hawa. Utafiti huu ni wa manufaa kwetu kwa kuwa ulishughulikia vipengele mbalimbali vya kimtindo katika hotuba za wanasiasa na wetu ulilenga pia kuchanganua na kulinganisha matumizi ya hotuba miongoni mwa wanasiasa teule. Tofauti baina ya tafiti hizi ni kuwa wetu umeangazia hotuba zilizoangazia suala la ufisadi pekee ilhali ule wa Lwaitama ulishughulikia mtindo bila kuegemea maudhui maalum.

Hakansson (2012) alitafiti matumizi ya viwakilishi nafsi katika hotuba za kisiasa ambapo alichanganua na kulinganisha hotuba zilizoangazia umoja wa kitaifa za marais wawili wa Marekani- Barack Obama na George Bush. Alilenga kubaini anayerejelewa na marais hawa wanapotumia viwakilishi nafsi; *mimi, wewe, sisi* na *wao* na pia kulinganisha tofauti katika matumizi yake miongoni mwa hawa marais wawili. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa uchaguzi wa viwakilishi nafsi miongoni mwa marais hawa haukutofautiana pakubwa. Matokeo pia yalionyesha kuwa kiwakilishi *mimi* hutumika wakati mzungumzaji anataka kujizungumzia yeye binafsi badala ya kuwa mwakilishi wa kikundi.

Hakansson (keshatajwa) akimrejelea Beard (2000), anasisitiza kuwa kiwakilishi nafsi *mimi* huonyesha kujitolea kwa mzungumzaji kwa hadhira yake katika suala analoangazia katika hotuba yake. Kiwakilishi *wewe* hutumika wakati mzungumzaji hazungumzi kwa niaba ya watu wengine bali hutaka kuonyesha watu hao wanajitegemea au wanastahili kuwajibikia

matendo yao; matumizi ya *sisi*, huonyesha ushirika katika jukumu fulani yaani mzungumzaji anaonyesha umuhimu wa ushirikiano baina yake na hadhira yake. Aidha, matumizi ya kiwakilishi nafsi *wao* huonyesha hali ya mzungumzaji kujitenga na watu wengine au kikundi fulani. Utafiti pia ulionyesha kuwa uchaguzi wa viwakilishi na yule ambaye viwakilishi hivyo hurejelea, hubadilikabadilika kutegemea miktadha ya hotuba. Matokeo ya utafiti huu yalitufaidi katika kubaini matumizi ya viwakilishi mbalimbali katika hotuba za wanasiasa teule wanaporejelea suala la ufisadi nchini Kenya. Utafiti huu ingawa unahusiana na wetu, ni tofauti kwani ulilenga tu matumizi ya viwakilishi nafsi ilhali wetu ulihakiki na kulinganisha matumizi ya vipashio kadhaa vya lugha katika matini za hotuba za kisiasa na jinsi vinavyoangazia suala la ufisadi.

Sarfo & Krampa (2013) walishughulikia uchanganuzi matini katika hotuba za Bush na Obama kuhusu uhalifu. Kutokana na hotuba sita walizochanganua, ilibainika kuwa hotuba hizi zilikuwa na wingi wa maneno na vishazi vilivyolenga uhalifu. Lugha iliyotumika ilijaa misamiati, vishazi, virai na sentensi mbalimbali ambazo zilisawiri uhalifu kama vitendo vya kikatili na hivyo basi ni adui wa binadamu. Kwa upande mwingine walitumia lugha kusawiri juhudi za kukabiliana na ugaidi kama tendo zuri na la kuhimizwa. Utafiti huu ulitufaa sana katika kuchunguza jinsi lugha katika hotuba za wanasiasa inavyodhihirisha vita dhidi ya ufisadi. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa kuangazia uchanganuzi wa hotuba za kisiasa kwa kulenga mada maalum japo tofauti ni kuwa, wetu unalenga viongozi wa kisiasa wa nchi ya Kenya wala si Marekani na pia mada lengwa ni ufisadi wala si uhalifu.

Baada ya mapitio haya ya kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu mada tuliyolenga kufanyia utafiti, ilibainika kuwa kulikuwa na pengo ambalo lilistahili kuzibwa na utafiti huu kwani hakuna aliyekuwa ameshughulikia uchanganuzi wa matini katika hotuba za kisiasa kuhusu suala la ufisadi.

**1.7 Misingi ya Kinadharia**

Kwa kuwa utafiti huu unalenga kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa, nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (UUH) ya Fairclough (1989) ilitumiwa ili kuafikia malengo yake. Fairclough (keshatajwa) anaeleza kwamba nadharia hii inaitwa uchanganuzi usemi hakiki kwa sababu lengo lake ni kuonyesha mwingiliano na mahusiano ambayo yanaweza kuwa yamefichwa yasionekane na watu, kwa mfano mwingiliano baina ya lugha na mamlaka. Nadharia hii inajihusisha na mahusiano kati ya matumizi ya lugha na uwezo. Kwa kuhakiki vipashio mbalimbali vya lugha katika matini ya hotuba za kisiasa, tuliweza kubaini uwezo wa hotuba hizi katika kupambana na ufisadi nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Crystal (1997), UUH ni dhana ya kuonyesha uhusiano kati ya matukio ya kiusemi, siasa, jamii na utamaduni; hasa kuambatana na vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii. Fairclough (1989) anadai kuwa uwezo ndani ya usemi hutokana na washiriki walio na uwezo wa kudhibiti mchango wa washiriki ambao hawana uwezo. Van Dijk (1993) akikubaliana na Fairclough (1989) anaeleza kuwa watu wenye ushawishi katika jamii hulenga kuathiri imani za kijamii na maadili kupitia vigezo wanavyoviweka kuhusu kile ambacho wanaamini kinakubalika au hakikubaliki katika jamii. Kwa misingi hii, tulihakiki na kulinganisha matini za hotuba

za baadhi ya wanasiasa kuhusu ufisadi ili kubaini ni kwa kiwango gani semi zao zinaathiri vita dhidi ya ufisadi nchini Kenya. Kadhalika, katika kuhakiki mielekeo na athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi, tulitumia maelezo ya Nesler na wengine (1993) wanaodai kuwa hadhira hukubali imani (maarifa na maoni) kupitia matini zinazoaminiwa zinatoka kwa watu walio na mamlaka, wanaoaminika au kutoka kwa vyanzo vingine vinavyoaminika kama vile wasomi, wataalamu au vyanzo vinginevyo.

Van Dijk (1998), anaeleza kuwa nadharia hii inahusiana na kusaili mielekeo ya usemi inayohusu kutawala, matumizi mabaya ya uongozi na ukosefu wa usawa; juhudi za kuuzalisha na kuustawisha utawala na pia kukataliwa kwake kupitia kwa matini yaliyoandikwa na maongezi katika miktadha mbalimbali ya kijamii na kisiasa. Anaongeza kuwa nadharia hii huangazia sana matumizi mabaya ya uongozi hasa watawala wanavyotumia hotuba kutawala imani za watu na matendo yao ili kuafikiana na ilhamu za kundi tawala kinyume na ilhamu za wasio na nguvu katika jamii. Anasema kuwa hotuba hutawaliwa na wale walio uongozini na kutawala akili ya watu ni njia mojawapo ya kuendeleza uongozi. Aidha anaeleza kuwa imani yetu kuhusu dunia inatokana na hotuba tunazozisikia. Mhimili huu ulituwezesha kubaini mielekeo ya umma kuhusu hotuba za wanasiasa zinazoangazia suala la ufisadi. Majibu katika hojaji zilizojazwa na wananchi yalitumika katika kubaini iwapo wana imani kuwa hotuba za wanasiasa teule zinalenga kuendeleza utawala wao tu au zinalenga vita dhidi ya ufisadi.

Kwa mujibu wa Scotton (1993), lugha huweza kutumiwa kuonyesha hadhi ya mtu kwa mfano, wazungumzaji wakiwa katika mazingira tofauti wanaweza kubadili msimbo ili

kukidhi mahitaji yao, na pia lugha inaweza kutumiwa kama kigezo cha kupimia mamlaka waliyo nayo watu. Mhimili huu ulikuwa muhimu katika juhudi za kutambua mamlaka waliyo nayo viongozi wa kisiasa katika kuukabili ufisadi nchini Kenya kupitia hotuba zao. Mamlaka haya yalibainishwa kwa kuhakiki na kulinganisha vipashio mbalimbali vya lugha katika matini za hotuba zao.

UUH hufafanua sababu za watu kusema wanachosema na nia zao. Ili kushughulikia maswali haya, Fairclough (1995) anafafanua kuwa, nadharia ya UUH huchukulia usemi kama tukio la kijamii na huhakiki athari za kijamii, kisiasa na miktadha ya kitamaduni kwa usemi; hasa vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii. Mhimili huu ulitusaidia kubaini athari za kijamii, siasa na miktadha kwa hotuba za wanasiasa kuhusu suala la ufisadi hivyo basi kubaini nafasi ya hotuba hizi katika vita dhidi ya ufisadi. Aidha, kwa mujibu wa Fairclough (keshatajwa), UUH huchukulia kuwa usemi huzaliwa na kukuzwa na itikadi, hivyo basi hutilia mkazo sifa za kimsingi za kiisimu za mahusiano ya kijamii, miundo ya kijamii na mgawanyo wa uongozi miongoni mwao.

Fairclough (1989, 1995) aliibua mtindo wa UUH ambao alisema una vipengele vitatu vya uhakiki. Kipengele cha kwanza ni matini yanayohakikiwa ambayo hujumuisha maongezi, picha au mseto wa matini za sauti na picha. Kipengele cha pili ni mchakato unaohusu jinsi matini zinavyozalishwa na binadamu kwa mfano kupitia kuandika, kuongea, kusikiliza au kutazama. Nacho kipengele cha mwisho ni hali za kijamii na kihistoria zinazoongoza michakato hii.

Fairclough (1995) anasema kuwa kila kipengele kilichotajwa hapo juu huhitaji mtindo wake wa uhakiki. Mtindo wa kwanza ni uhakiki wa matini (uchanganuzi) ambapo sifa za matini husika hutambuliwa na kuainishwa. Mhimili huu tuliutumia kutambua, kueleza na kulinganisha vipashio mbalimbali vya lugha (maneno, virai, sentensi na aya) katika matini za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi ili kubaini jinsi ufisadi ulivyoshughulikiwa katika hotuba za wanasiasa teule. Mtindo wa pili ni mchakato wa uhakiki wenyewe (ufafanuzi) ambapo uhusiano baina ya matini na uwasilishaji hushughulikiwa. Kwa kuhakiki maoni ya wananchi kuhusu hotuba za viongozi teule kuhusu ufisadi, tulitumia mhimili huu kubaini athari za hotuba hizi kwa wananchi kwani uwasilishaji wa hotuba huathiri mapokezi ya ujumbe lengwa kwa hadhira. Mwisho ni uhakiki wa kijamii (maelezo) ambapo uhusiano baina ya utendaji na miktadha ya kijamii huelezwa. Kwa kuwa mtindo huu hufafanua athari za usemi kwa jamii, tuliutumia katika utafiti huu kubaini mielekeo ya umma kuhusu hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi na pia athari zake kwao kwa kuhakiki maoni yao kuhusu hotuba hizi.

**Ifuatayo ni mihimili ya nadharia hii iliyotumiwa katika utafiti huu**

(i) Kuna uhusiano kati ya matukio ya kiusemi, siasa, jamii na utamaduni; hasa vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii.

(ii) Watu wenye ushawishi katika jamii hulenga kuathiri imani za kijamii na maadili kupitia vigezo wanavyoviweka kuhusu kile ambacho wanaamini kinakubalika au hakikubaliki katika jamii.

(iii) Hadhira hukubali imani (maarifa na maoni) kupitia matini yanayoaminiwa yanatoka kwa watu walio na mamlaka, wanaoaminika au kutoka kwa vyanzo vingine vinavyoaminika kama vile wasomi, wataalamu au vyanzo vinginevyo.

(iv) Imani yetu kuhusu dunia inatokana na hotuba tunazozisikia.

(v) Usemi ni tukio la kijamii. Aidha, athari za kijamii, kisiasa na miktadha ya kitamaduni kwa usemi huhakikiwa.

(vi) Katika uchanganuzi wa matini, sifa za matini husika hutambuliwa na kuainishwa.

(vii) Mahusiano kati ya matumizi ya lugha na uwezo hutathminiwa.

(viii) Hotuba hutawaliwa na wale walio uongozini kwa nia ya kutawala imani za watu na matendo yao.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Katika sehemu hii, tumeangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti wetu, uteuzi wa sampuli, idadi ya sampuli, masuala ya kimaadili, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchanganuzi wa data na kisha mbinu za kuwasilisha matokeo.

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Kothari (2007) anafafanua muundo wa utafiti kama mwongozo wa kutimiza malengo na kupata majibu ya maswali ya utafiti. Kwa hivyo, muundo wa utafiti ni namna ya kufanya utafiti kwa kufuata utaratibu maalum. Ili kuafikia malengo yote, utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo na muundo wa kisoroveya. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa kutoa ufafanuzi na ulinganisho wa vipashio mbalimbali vya lugha katika matini ya hotuba za wanasiasa teule ili kubainisha wanavyoangazia suala la ufisadi katika hotuba zao. Kwa

mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), utafiti wa kimaelezo hutoa ripoti ya jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani na hueleza tabia, mielekeo, itikadi na hali mbalimbali za watu. Nao muundo wa kisoroveya, kwa mujibu wa Gray (2009), ni utaratibu wa kukusanya data kwa kutumia hojaji ama mahojiano kutoka kwa sampuli ili kupata data. Akiunga mkono maelezo ya Gray, Schilling (2013) anaeleza kuwa, jukumu la muundo wa kisoroveya ni kukusanya data kuhusu mielekeo ya watu, maoni yao na tabia zao miongoni mwa masuala mengine. Kwa mujibu wa maelezo haya, utafiti huu ulitumia muundo huu wa kisoroveya kukusanya data ambayo ilichanganuliwa ili kubaini mielekeo ya wananchi wa Kenya kuhusu hotuba za kisiasa zinazolenga mada ya ufisadi na pia athari za hotuba hizo kwao.

### 1.8.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Makatabani tulipata baadhi ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwenye mtandao wa YouTube. Tulipata pia makala muhimu kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada, maelezo zaidi kuhusu nadharia ya UUH na matini mengineyo muhumu kwa utafiti huu. Utafiti wa nyanjani ulifanyika nchini Kenya katika kaunti ya Kakamega mjini Mumias. Mji huu ulitupa data tuliyolenga kwa sababu ni eneo mojawapo ambalo lina wafuasi wa takribani vyama vyote vya kisiasa nchini hasa vyama vya *Jubilee* na *Orange Democratic Movement* (ODM) ambapo hotuba za viongozi wa vyama hivi ndizo zilizolengwa katika utafiti huu. Nyanjani, tulipata data za kimsingi na za moja kwa moja kwa kuwahoji wananchi wa mji wa Mumias ili kupata maoni yao kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi ili kubaini zinavyowaathiri na pia kubaini mielekeo yao kuzihusu hotuba hizi.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Kothari (2007), sampuli ni sehemu ya kitu au watu fulani ambao huteuliwa na kutumiwa kwa minajili ya kufanya maamuzi yanayohusu kundi zima. Tutatumia sampuli kusudio ambapo tutawachagua viongozi wawili wa kisiasa ambao wameliangazia sana suala hili; Rais wa tano wa nchi ya Kenya, Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga. Kwa kuwa waliangazia sana suala hili katika hotuba zao na walikuwa viongozi wakuu wa kisiasa nchini, data iliyopatikana kutokana na hotuba zao ilitosheleza mahitaji ya utafiti huu. Aidha, wanasiasa hawa wawili walikuwa viongozi wa vyama vikuu vya kisiasa nchini Kenya na hivyo basi walikuwa na wafuasi wengi sana nchini ambao waliwategemea kutoa suluhu la tatizo hili la ufisadi.

Hotuba tulizolenga ni za maongezi wala sio zilizosomewa hadhira kwani tulidhamiria kupata uhalisi wa mitazamo yao kuhusu suala la ufisadi. Kipindi cha hotuba tulizohakiki ni kati ya mwaka wa 2015 na 2020. Hotuba lengwa ni zilizoangazia sakata ya ufisadi katika shirika la huduma kwa vijana la NYS kuanzia mwaka wa 2015 na sakata ya ufisadi katika mradi wa maji katika mabwawa ya Arror na Kimwarer iliyoripotiwa mwaka wa 2019. Hotuba tulizoangazia ni za kipindi cha kabla na baada ya maafikiano ya wanasiasa hawa wawili.

Kwa mujibu wa Citizen Digital (2018), takriban shilingi bilioni 10 ziliibwa katika sakata ya NYS II, mwaka mmoja baada ya shilingi milioni 791 kuibwa katika sakata ya NYS I. Kwa upande mwingine, shilingi bilioni 27.7 ziliibwa katika sakata ya mabwawa ya Arror

na Kimwarer (The Standard, 2019). Sakata hizi ni miongoni mwa sakata kuu za ufisadi nchini Kenya kuanzia mwaka wa 2013 kwa mujibu wa The Youth Cafe (2020).

Baada ya kusikilizwa na kuandikwa, data ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi ilisimbwa kama ifuatavyo; RO1, RO2, RO3, UK1, UK2 na UK3 ili kuweza kurejelewa kwa wepesi. RO1 na RO2 ni hotuba za Raila Odinga zilizoangazia sakata ya NYS na RO3 ni ile ambayo iliyoangazia sakata ya ufisadi ya mabwawa ya Arror na Kimwarer. Kwa upande mwingine, UK1 na UK2 zilitumiwa kurejelea hotuba za Uhuru Kenyatta kuhusu sakata ya NYS nayo UK3 ikarejelea ile ya sakata ya mabwawa ya Arror na Kimwarer.

Katika utafiti wa nyanjani, sampuli iliteuliwa kimakusudi ili kupata wananchi katika mji wa Mumias ambao wanaelewa hotuba za kisiasa zinazohusu ufisadi. Wananchi wa mji huu waliteuliwa kwa kuwa una wafuasi wa vyama vingi vya kisiasa hasa vyama viwili vikuu; Jubilee na ODM ambavyo hotuba za viongozi wao ndizo zilizolengwa katika utafiti huu. Mtafiti alilenga vijana na watu wa umri wa makamo kwa kuwa hao ndio wenye uelewa mzuri wa masuala ya kisiasa, ni washiriki wakuu katika mikutano ya kisiasa na pia ni wahanga wa matendo ya ufisadi. Hotuba zilizochanganuliwa zilikuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa hivyo ilibidi wasailiwa wawe na umilisi wa lugha hizi mbili.

### 1.8.4 Idadi ya Sampuli

Hotuba 6 ziliteuliwa kimakusudi kuchanganuliwa katika utafiti huu. Hotuba hizi zilitupa data ya kutosha tuliyohitaji katika utafiti huu. Nchi ya Kenya ina jumla ya watu 47,564,296 na mji wa Mumias una idadi ya watu 41,942 kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya mwaka

2019. Utafiti huu uliteua wasailiwa 76 kimakusudi kuwakilisha maoni ya Wakenya wote. Wanawake walioteuliwa ni 38 na wanaume 38 pia. Kwa mujibu wa Lune na wengineo (2010), mbinu kusudio haizingatii ukubwa wa sampuli, kilicho muhimu ni kama sampuli inamwezesha mtafiti kupata data ya kutosha itakayomwezesha kushughulikia maswali ya utafiti. Aidha, Ngechu (2004) anadai kuwa idadi ya sampuli ipimwe kimaeneo. Anaeleza kuwa iwapo eneo la utafiti ni nchi nzima, sampuli isipungue wahusika 1000 ilhali iwapo eneo lengwa ni dogo kama vile wilaya, idadi ya sampuli yafaa kuwa na wahusika 50 au zaidi.

### 1.8.5 Masuala ya Kimaadili

Kabla ya mtafiti kuenda nyanjani, aliomba kibali kutoka Chuo kikuu cha Kenyatta kupitia shule kuu ya Sayansi za Kijamii kisha akaomba na kukabidhiwa cheti kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Uvumbuzi na Teknolojia (NACOSTI). Aidha, aliomba idhini kutoka kwa chifu wa kata ya Nabongo mjini Mumias kabla ya kuanza utafiti. Waliohojiwa pia walitakiwa kutoandika majina yao kwenye hojaji walizojaza ili kuwahakikishia usiri wa ujumbe waliotoa. Isitoshe, walihakikishiwa na mtafiti kuwa data waliotakiwa kutoa ingehifadhiwa vyema na kutumiwa kwa shughuli za kiusomi pekee.

### 1.8.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Ukusanyaji wa data ulihusisha utafiti wa nyanjani na wa maktabani. Mbinu hizi mbili zilituwezesha kupata data iliyohitajika.

### 1.8.6.1 Kusoma, Kusikiliza na Kudondoa Ujumbe

Data ya hotuba za kisiasa ilikusanywa maktabani. Video za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kutoka mtandao wa YouTube zilipakuliwa na kisha kuhifadhiwa katika diski mweko ili kuzisikiliza, kuziandika na kisha kutafsiri zile ambazo zipo katika lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili kwa madhumuni ya kuchanganuliwa baadaye. Aidha, tulisoma kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada ya uchanganuzi wa hotuba za kisiasa, nadharia ya UUH na pia kuhusu suala la ufisadi hasa nchini Kenya.

### 1.8.6.2 Hojaji

Maoni ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia ufisadi ambayo ndiyo data lengwa, yalikusanywa kwa kutumia hojaji funge za likati na vilevile hojaji wazi ili kupokea maoni yao katika maandishi ambayo tuliyahakiki baadaye ili kubaini mielekeo yao kuhusu mada lengwa. Kwa mujibu wa Kothari (2004), hojaji funge za likati ziliasisiwa na mwanasaikolojia Rensis Likert mwaka wa 1972 kwa lengo la kupima mielekeo ya watu. Hojaji likati huwa na kauli tano hadi saba ambazo huonyesha mitazamo kubalifu au isiyo kubalifu kuhusu utafiti husika. Wasailiwa walipewa hojaji hizi funge za likati zenye kauli tano ambapo kila jawabu lilipewa alama kuanzia 1-5 kama anavyoeleza Mcleod (2019). Baada ya kupokea data, data ili changanuliwa kwa kutumia fomyula maalum ifuatayo ili kubaini alama wastani kwa mujibu wa Mcleod (keshatajwa).

$$\text{Alama wastani} = \frac{\Sigma(fi \times alamakatikalikati)}{\textit{Jumla ya watafitiwa}}$$

Alama hizi wastani ndizo zilizotumiwa kubainisha mielekeo ya wananchi kwa kufuata mwongozo wa Mcleod (2019) ufuatao:

Alama 1.0 - 2.4 = mwelekeo hasi

Alama 2.5 -3.4 = mwelekeo wastani (wa katikati)

Alama 3.5 – 5.0 = mwelekeo chanya

Aidha, kwa sababu ya mapungufu ya hojaji funge ya likati ambapo msailiwa huenda akakosa kujieleza vyema; tuliwapa wasailiwa hojaji wazi pia ili kufidia mapungufu hayo.

Baadaye mtafiti alijumuisha alama. Kwa mujibu wa Mcleod (2019) fomyula ya kujumuisha alama ni:

Jumla ya alama = $\Sigma\ (fi \times alama\ katika\ likati)$

Ambapo $fi$ ni jumla ya alama katika kila likati (idadi jumla ya wahojiwa)

Kwa mujibu wa utafiti huu $fi$= 76

$i$ =ni alama katika likati; yaani 'Nimekataa kabisa' NTK (1), 'Nimekataa' NT(2), 'Sikatai wala kukubali' STK(3), 'Nimekubali' NK(4) na 'nimekubali kabisa'NKK(5)

Ili kupata alama wastani, fomyula ifuatayo hutumiwa:

Alama wastani = $\underline{\Sigma\ (fi \times alamakatikalikati)}$

*Jumla ya watafitiwa*

Kwa mujibu wa Mcleod (keshatajwa), mielekeo hubainishwa kwa kuhakiki alama wastani za kila kauli iliyo kwenye hojaji ya likati ambapo:

1.0 - 2.4 = mwelekeo hasi

2.5 -3.4 = mwelekeo wastani (wa katikati)

3.5 – 5.0 = mwelekeo chanya

### 1.8.7 Uchanganuzi wa Data

Data kutokana na matini ya hotuba mbalimbali za wanasiasa teule ilichanganuliwa, ikalinganishwa na kulinganuliwa kwa mwongozo wa nadhadira ya UUH. Hotuba katika lugha ya Kiingereza zilitafsiriwa kabla ya kuchanganuliwa na kulinganishwa. Vipengee mbalimbali vya kimatini kwenye hotuba za wanasiasa teule kuhusu ufisadi vilibainishwa na kupangwa katika kategoria mbalimbali ili kueleza vilivyotumiwa kuangazia suala la ufisadi. Kadhalika, majedwali yalitumiwa ili kulinganisha vipengee mbalimbali vya kimatini vilivyobainika kwenye hotuba za wanasiasa teule. Majedwali pia yalitumika kupanga na kulinganisha data kuhusu maoni ya wananchi kuhusu hotuba za wanasiasa teule kuhusu ufisadi na kisha baada ya kuhakiki maoni yao, maelezo yalitumiwa kufafanua namna hotuba hizi zinavyowaathiri wananchi wa Kenya na vilevile kufafanua mielekeo yao kuzihusu.

### 1.8.8 Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyopatikana iliwasilishwa kwa maelezo, takwimu na majedwali ili kufafanua na kulinganisha jinsi matini katika hotuba za wanasiasa teule yalivyoangazia suala la ufisadi, kubainisha athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya na pia kubaini mielekeo yao kuhusu hotuba za wanasiasa teule zinazolenga kuupiga ufisadi vita kwa kuyahakiki maoni yao. Majedwali yalitumiwa kuwasilisha ulinganisho wa vipengee mbalimbali vya kimatini vilivyobainika kwenye matini za hotuba za kimazungumzo za wanasiasa teule kuhusu ufisadi na pia kulinganisha maoni ya wananchi kuhusu hotuba hizo. Tulitumia majedwali pia kuwasilisha ulinganisho wa vigezo mbalimbali katika hotuba za wanasiasa teule na maoni ya wananchi kuhusu nafasi ya hotuba hizi.

### 1.9.0 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia utangulizi wa tasnifu. Imeangazia usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti. Masuala haya yameweza kujadiliwa kwa kina ili kuupa utafiti huu mwelekeo unaofaa. Isitoshe, masuala yaliyojadiliwa katika sura hii yaliweka msingi wa masuala mengine yaliyoshughulikiwa katika sura nyingine hususan sura ya pili ambayo iliangazia kwa kina zaidi suala la matini ya hotuba za kisiasa na ufisadi.

# SURA YA PILI

# MATINI YA HOTUBA ZA KISIASA NA UFISADI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, ilibainika kuwa lugha ni kigezo muhimu katika kufanikisha mawasiliano yoyote. Wanasiasa hutumia lugha kwa njia ya kipekee katika hotuba zao kuangazia masuala mbalimbali. Hotuba za kisiasa zimetumiwa kukemea mafisadi kwa muda mrefu nchini Kenya japo mchango wake katika vita dhidi ya ufisadi haubainiki. Kwa

mujibu wa wataalamu Beaugrande na Dressler (1981), mshikamano, muwala, muktadha, kusudio, ukubalifu, ufahamishwaji na mwingiliano wa matini huchukuliwa kama tukio la kimawasiliano. Aidha walibainisha aina mbili za matini; matini ya mawasiliano ya kimazungumzo na ya kimaandishi.

Kwa kuwa kipengele cha lugha ni muhimu katika uhakiki wa matini, sura hii imeshughulikia kwa kina dhana ya lugha ambapo maana na dhima ya lugha katika mawasiliano kwa jumla na katika hotuba za kisiasa imehakikiwa. Aidha maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu sifa mbalimbali za matini za hotuba za kisiasa na majukumu yake zimehakikiwa pia. Mbali na hayo, uwezo wa lugha katika kufanikisha matamanio, itikadi na sera za wanasiasa imeweza kujadiliwa kwa kina. Isitoshe, dhana ya hotuba za kisiasa imefafanuliwa pia ambapo sifa za hotuba za kisiasa na uwezo wake katika kutekeleza matakwa ya wanasiasa katika jamii imefafanuliwa. Hali kadhalika, kwa sababu hotuba za kisiasa lengwa katika utafiti huu ni kuhusu suala la ufisadi, imekuwa muhimu pia kujadili japo kwa ufupi uhusiano uliopo kati ya hotuba za kisiasa na suala la ufisadi. Kwa kushughulikia haya yote, mtafiti ameweza kufafanua zaidi suala la utafiti huu. Tunaanza kwa kufafanua dhana ya lugha na matini.

## 2.1 Dhana ya Lugha na Matini

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu na ishara zinazokubalika kutumiwa na wanajamii kwa ajili ya mawasiliano. Wanaisimu wengi wanakubaliana na ufafanuzi wa Cook (1969) kuwa, lugha ni mfumo wa sauti nasibu na ishara za kisarufi ambazo watu wa jamii fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao.

Nkwera (1978) anafafanua dhima kuu ya lugha kama chombo cha mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa matokeo ya kuwasiliana huku ni kuafikiana au kufarakana, kujenga au kubomoa, kuleta vita au amani. Aidha, anafafanua kuwa matokeo hayo hutegemea taarifa na kauli zinazotolewa na namna taarifa zenyewe zilivyowasilishwa; yaani, vizuri au vibaya. Maelezo haya yanaipa uzito njia za uwasilishaji wa ujumbe kando na lugha; yaani jinsi lugha inavyotumiwa katika juhudi za kuwasilisha ujumbe lengwa. Hii ina maana kuwa ili kuwasilisha ujumbe ifaavyo ni lazima lugha itumiwe vyema na msemaji. Maelezo haya yaliupa utafiti huu msingi mwafaka wa kutathmini namna lugha ilivyotumiwa katika hotuba za wanasiasa teule wakiwa na lengo la kuangazia vita dhidi ya ufisadi. Kuna uwezekano wa ama kufaulu au kutofaulu kulingana na jinsi wanavyotumia lugha.

Coates (1993) naye anafafanua kuwa watu hutumia lugha kujitambulisha. Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, wanasiasa hutumia lugha kujitambulisha na kutambulisha sera zao na misimamo yao kuhusu masuala mbalimbali yanayotendeka katika jamii. Aidha, Ogechi (2002) anashikilia kuwa lugha ndiyo nyenzo muhimu inayofanikisha mawasiliano kwa kupitisha ujumbe kati ya mtu mmoja na mwingine na kati ya taifa moja na jingine. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza hotuba za kisiasa ambazo huangazia suala la ufisadi kwa hadhira tofautitofauti, basi maelezo haya kuhusu dhima ya lugha yalikuwa na umuhimu katika kutathmini nafasi ya hotuba za kisiasa katika vita dhidi ya ufisadi.

Mercer (1977) anakubaliana na wasomi wengine kama vile Coates (1993) kuwa, mazungumzo ni muhimu katika shughuli za kupata elimu. Aidha, anadai kuwa bila ya mazungumzo ni vigumu kwa binadamu kuelewa, kufafanua na hata kuendeleza mawazo yake. Hivyo basi, anasisitiza kuwa binadamu ni lazima atumie lugha kwa madhumuni ya kuwasilisha mawazo yake kwani lugha ndio msingi wa mawazo ya binadamu. Hali kadhalika, anadai kuwa lugha huongozwa na mtazamo wa mwelekeo wa utamaduni na siasa za nchi kwa jumla. Hii ina maana kuwa lugha na hisia za kisiasa huenda sambamba na huathiri mtu binafsi pamoja na mtazamo wake kwa mazingira. Ufafanuzi huu ulielekeza utafiti huu katika kuchanganua hotuba za kisiasa na kulinganisha mawazo ya wanasiasa kuhusu suala la vita dhidi ya ufisadi.

Halliday (1987) anadai kuwa aina ya lugha hubainishwa kwa kutegemea dhima ambayo lugha hiyo imepewa katika kipindi fulani. Maelezo haya yanadokeza dhana ya sajili katika lugha ambapo lugha hutumika kwa namna tofautitofauti kulingana na miktadha maalum. Kwa maelezo haya ya Halliday (keshatajwa) utafiti huu ulihakiki hotuba za kisiasa kwa kuzingatia majukumu ya lugha katika sajili hiyo.

Kwa mujibu wa Brown na Yule (1993), dhana ya matini hufafanuliwa kiisimu kama matumizi ya lugha. Rodgers na wengine (2005) wanakubaliana na madai haya ya Brown na Yule na kuongezea kuwa matini hudhihirisha namna lugha inavyoanzisha mahusiano ya kijamii, inanvyojenga utambulisho na imani. Aidha, Fairclough (1992) anashikilia kuwa matini ndio huunda na kujenga maana; yaani, kupitia matini, binadamu huweza kuelewa jinsi jamii inavyotenda kazi kwa sababu lugha ni mfumo ambao huchangia uzalishaji wa

mahusiano ya kiuwezo katika jamii. Maelezo ya wasomi hawa yalitumiwa katika utafiti huu kuchunguza na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi hasa katika kubainisha uwezo wa matini ya hotuba teule za wanasiasa katika juhudi za kupambana na ufisadi.

Aidha, wataalamu wengi wanakubaliana kuwa uchanganuzi wa matini ni uhakiki wa jinsi vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumiwa katika matini ya maongezi au yaliyoandikwa. Stubbs (1983) anaifafanua dhana hii kama matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii hasa baina ya wanenaji. Naye Johnstone (2008) anasisitiza kuwa katika uchanganuzi wa matini, matini huchunguzwa kwa undani ili kubainisha sababu ya matini kuwa jinsi yalivyo. Madai haya yanawiana na ya Martin na Rose (2003) ambao wanasisitizia uchunguzi wa maana fiche kwenye matini. Kwa mujibu wa maelezo ya wasomi hawa, utafiti huu uliweza kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kwa kuhakiki kwa undani vipengele mbalimbali vya lugha ili kubainisha maana na nafasi zake katika vita dhidi ya ufisadi.Kando na uhusiano kati ya lugha na matini, kuna uhusiano kati ya lugha na siasa.

**2.2 Lugha na Siasa**

Wanasiasa huwasilisha mawazo yao na itikadi zao kwa jamii kupitia lugha. Fairclough (1989) anafafanua kuwa mwanasiasa anaweza kueleza matatizo yaliyoko katika jamii na pia kuwasilisha itikadi anazoziamini kwa kutumia lugha. Itikadi huwa na misingi katika jamii husika kwa mujibu wa Van Djik (1998). Akikubaliana na madai haya, Woofffit (2005) anafafanua dhana ya itikadi kama mpangilio wa imani ambazo huhamasisha desturi na mitazamo ambayo huendeleza utabaka katika jamii. Kama wanavyoeleza wataalamu

hawa kuwa wanasiasa wana uwezo wa kutumia lugha kuangazia matatizo katika jamii na kuendeleza itikadi wanazoziamini, mtafiti alidhamiria kuchanganua na kulinganisha jinsi wanasiasa wanavyotumia lugha katika hotuba zao kuangazia tatizo la ufisadi katika nchi ya Kenya na athari zake kwa hadhira.

Aidha, Obeng (2002) anadai kuwa, uwezo wa mwanasiasa wa kuhutubu humfanya kuwa na mamlaka fulani kwa vile lugha ndio nyenzo ya kuwasilisha uwezo wake wa kisiasa. Uwezo huu wa wanasiasa katika hotuba huwafanya wengi kuangazia masuala mbalimbali katika jamii kwa nia ya kuhimiza wanayoyaunga mkono na kukashifu wasiyoyaunga mkono. Madai haya ya Obeng yanadhihirisha kuwa lugha ni chombo muhimu sana katika siasa kwani ndiyo hutumiwa na mwanasiasa kujijenga mwenyewe kisiasa na kuendeleza sera zake kwa wananchi. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matumizi ya hotuba za kisiasa katika kuangazia suala la ufisadi, maelezo haya yalikuwa ya umuhimu sana kwani yanaeleza uwezo wa lugha ya kisiasa katika kuangazia masuala yanayoathiri jamii kwa madhumuni mbalimbali.

Lugha huathiri matendo ya watu katika jamii. Kwa mujibu wa Austin (1975), lugha hutenda matendo mbalimbali katika jamii mhutubu anapotumia maneno kuonya, kuuliza, kulazimisha, kushawishi, kukejeli, kusuta, kuaibisha na kutia au kuvunja moyo. Wanasiasa huteua maneno kwa uangalifu mkubwa ili kuathiri matendo kulingana na mtazamo na matamanio yao kuhusu suala husika. Maelezo haya ya Austin (keshatajwa) yalitumiwa katika utafiti huu kuchunguza maneno yaliyotumiwa katika hotuba za wanasiasa teule katika hotuba zao kuhusu suala la ufisadi ili kubainisha uwezo wa lugha wanayoitumia

katika kupiga vita ufisadi nchini Kenya. Aidha maelezo haya yalikuwa muhimu pia katika ubainishaji wa athari za hotuba za wanasiasa hawa kwa wananchi ambao ndio hadhira yao.

Adero (2005) anakubaliana na maelezo ya Obeng (2002) na kuongezea kuwa, kwa kutumia lugha, wanasiasa hunyang'anyana uwezo na mamlaka baina yao na vilevile hunyakua mamlaka hayo kutoka kwa wananchi na huiweka katika ukiritimba wa uongozi pale ambapo watu wachache huhusika. Hali kadhalika, anadai kuwa wanasiasa wana njia tofauti za kutumia lugha bila wao kutaja wazi na hivyo huweza kuhimili maongezi ya kisiasa. Maelezo haya yanaungwa mkono na Joseph (2006) ambaye anasisitiza kuwa lugha ya wanasiasa hutofautiana na lugha ya kawaida kwa sababu wanasiasa hutumia vipengele fulani maalum vya lugha kufikisha ujumbe wao kwa jamii. Baadhi ya vipengele hivi kwa mujibu wa Sovu (2018) ni; matumizi ya istilahi na msamiati maalum, matumizi ya nafsi ya kwanza umoja na wingi, ubadilishaji msimbo, matumizi ya misemo, uradidi wa maneno, lugha yenye kutoa matumaini, matumizi ya lugha yenye takwimu, matumizi ya maswali balagha na mzaha, lugha ya mshikamano na matumizi ya lafudhi kulingana na muktadha. Madai ya wataalamu hawa yalikuwa muhimu katika utafiti huu hasa katika kuchanganua jinsi hotuba za kisiasa zilivyoangazia suala la ufisadi. Tuliweza kutambua matumizi ya baadhi ya vipengele hivi vya lugha vilivyobainishwa na Sovu (keshatajwa) katika baadhi ya hotuba.

Brown na Yule (1983) wanadai kuwa katika isimu, usemi huangaliwa kama matumizi ya lugha. Hii ina maana kuwa katika uhakiki wa hotuba za kisiasa, ni lazima matumizi ya lugha kutathminiwa. Kama wataalamu hawa wanavyosisitizia umuhimu wa kuhakiki

matumizi ya lugha katika hotuba za kisiasa ili kutathmini malengo ya hotuba, utafiti huu ulichunguza na kulinganisha namna lugha ilivyotumiwa katika matini ya hotuba za kisiasa teule ili kutathmini nafasi yake katika vita dhidi ya ufisadi.Kando na hayo, ni vyema kufafanua dhana ya hotuba za kisiasa.

## 2.3 Dhana ya Hotuba za Kisiasa

Hotuba ya kisiasa ni mawasiliano yanayotolewa na wanasiasa katika miktadha mbalimbali kwa dhima ya kuendeleza ushawishi wa kisiasa kwa kuangazia masuala mbalimbali yanayoathiri jamii. Mulokozi (1996:48), anafafanua hotuba ya kisiasa kama mazungumzo rasmi ambayo huwasilishwa kwenye vikao rasmi vya kimila, kisiasa, kidini na kadhalika. Hotuba hizo hupangwa kimantiki na hutolewa kisanaa: methali, nyimbo, michapo hutumika kwa wingi; mtoaji hutumia mbinu za ulumbi kwa mfano, kurudiarudia vipashio fulani vya lugha ili kuvuta hisia za sanaa ya maonyesho. Kama anavyoeleza Mulokozi, tulibainisha uradidi kama mbinu mojawapo za ulumbi katika hotuba teule za wanasiasa kuhusu suala la ufisadi na kuhakiki zinavyotumiwa kuwasilisha suala la vita dhidi ya ufisadi.

Wilson (2001) anafafanua hotuba za kisiasa kama lugha (aidha rasmi au isiyo rasmi) inayotumiwa na wanasiasa katika ulingo wa siasa wakiwa na lengo la kisiasa. Randy (2021) akikubaliana na madai haya ya Wilson, anazidi kufafanua hotuba za kisiasa kama mkakati wa mawasiliano unaotegemea uundaji wa ujumbe kupitia raslimali za maneno, raslimali zisizo za maneno na za kimapenzi kwa nia ya kumshawishi mtu binafsi au hata kikundi cha watu. Kwa misingi ya maelezo haya ya Randy, tulichanganua raslimali za

maneno yaliyotumiwa na wanasiasa teule katika hotuba zao kuhusu ufisadi na kutathmini uwezo wake wa kushawishi wananchi kuunga mkono maoni na harakati zao katika vita dhidi ya ufisadi.

Ingawa Wilson (2001) anasisitiza kuwa hotuba za kisiasa hutolewa katika ulingo wa kisiasa, Adero (2005) anadai kuwa mawasiliano ya kisiasa hutawala katika hotuba za Rais, majadiliano ya bunge, mikutano ya kisiasa, propaganda na hata wakati mwingine, katika shughuli za kijamii kama vile mazishi, ndoa, misa na tohara. Hii ina maana kuwa hotuba za kisiasa hutolewa popote palipo na hadhira lengwa ya mwanasiasa. Utafiti huu pia uliangazia hotuba za kisiasa zilizotolewa na wanasiasa katika miktadha tofautitofauti.

Kwa mujibu wa Seidel (1985) hotuba ya kisiasa huweza kujikita katika vipera, tanzu au taaluma mbalimbali. Anafafanua kuwa kama hotuba nyingine, hotuba za kisiasa huwa na vipengele vitatu; mhutubu, mhutubiwa na hotuba yenyewe. Madai haya yanashikiliwa pia na Van Dijk (1997) anayedai kuwa ili kuchanganua matini ya siasa kama vile hotuba za kisiasa, mhakiki anastahili kuzingatia vipengele vitatu vifuatavyo: wanasiasa au waandishi wa hotuba za kisiasa, wapokezi wa hotuba hizo/hadhira lengwa na kisha matini ya hotuba za kisiasa yenyewe. Vipengele hivi vitatu vilikuwa muhimu katika utafiti huu. Kwa kuzingatia kipengele cha kwanza tulihakiki wanasiasa teule ambao hotuba zao zilichanganuliwa katika utafiti huu na kubaini kuwa wana ushawishi mkubwa nchini. Tulitathmini uwezo wao pamoja na matini yao katika kuangazia vita dhidi ya ufisadi nchini. Kwa mujibu wa kipengele cha pili, utafiti huu ulichunguza athari za hotuba za

wanasiasa hawa kuhusu suala la ufisadi kwa wananchi wa Kenya ambao ndio hadhira yao lengwa.

Aidha, kwa mujibu wa Ngure (2020), hotuba za kisiasa huwa na ukwasi wa tamathali za usemi. Anaeleza kuwa tamathali nzuri za usemi huyakinisha na kuipa uhai zaidi dhana inayoelezwa na mhutubu. Tamathali hizi huzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisia na mawazo yake. Kando na hayo, anaeleza kuwa tamathali za usemi ni chombo cha kutolea mawazo ya jamii; yaani huhamasisha umma ili uone hali halisi ya mambo ilivyo. Tamathali za ufananisho kama tashbihi, sitiari, jazanda na tabaini hutumiwa sana katika hotuba za kisiasa kusawiri mienendo na tabia za wanasiasa. Kwa mfano, kinyonga hutumiwa kulinganisha tabia ya wanasiasa ya kutokuwa na msimamo thabiti na kinyonga ambaye hujigeuza rangi kila mara. Anaeleza pia kuwa mafumbo hutumiwa katika hotuba hizi kuelimisha umma vilevile kuhusu hulka za wanasiasa. Kwa mfano, 'Msitu umebadilika lakini nyani ni wale wale,' ni fumbo lenye maana ya kuwa wanasiasa huwa na hulka sawa; yaani hata utawala ukibadilika wanaochukua mamlaka huenda wasiwe tofauti na waliong'atuka mamlakani. Maelezo haya ya Ngure yalikuwa muhimu kwa utafiti huu kwani tamathali za lugha ziliweza kubainika katika hotuba teule ambazo zilihakikiwa na kulinganisha namna zilivyotumiwa kuangazia suala la ufisadi, athari zake kwa umma na mielekeo ya umma kuzihusu.

Aidha, wataalamu wengi wanakiri kuwa dhima ya hotuba za kisiasa ni kujenga ushawishi miongoni mwa wanasiasa na kujipatia au kudhirisha mamlaka yao. Klebanov na wengine (2008; Niedrich 2011) wanaeleza kuwa, hotuba ya kisiasa huweza kuchukuliwa kama njia

ya kimsingi ya kushawishi wengine kwa kutumia lugha shawishi, kuwabembeleza, kuwafurahisha na kujipa mamlaka. Hali kadhalika, Chilton (2004); Chilton, Tian & Wodak (2012) na Wodak (2015) wanashikilia madai hayo hayo kuwa, hotuba za kisiasa ni mojawapo ya hotuba ambamo mamlaka huweza kudhihirika. Wanadai kuwa njia mojawapo ya kutathmini mawasiliano ya kisiasa ni kuchunguza hotuba za kisiasa za wanasiasa mbalimbali. Wataalamu hawa wanakiri kuwa lugha ya kisiasa hulenga kushawishi hadhira husika kwa madhumuni ya kudhihirisha mamlaka waliyo nayo au kujipa mamlaka. Madai haya yalitumiwa katika utafiti huu katika uchanganuzi na ulinganishi wa namna hotuba teule za kisiasa zilivyoangazia suala la ufisadi. Hapa uwezo wa wanasiasa hawa kushawishi umma na kudhihirisha mamlaka waliyo nayo katika vita dhidi ya ufisadi yaliweza kuchunguzwa kupitia uhakiki wa hotuba zao.

Al-Majali (2015) anakubaliana na madai ya wataalamu hawa na kuongezea kuwa kwa kutumia mbinu kama ufafanuzi na uchanganuzi, hotuba za kisiasa hutumiwa kuwashawishi wapokezi wa ujumbe kuunga mkono mtazamo wa mnenaji kwa upande mmoja na kwa upande mwingine kuficha, kubadilisha na kuimarisha jambo fulani. Ni kwa misingi hii ambapo tulichanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi na kubainisha jinsi ambavyo wanasiasa teule walivyotumia lugha katika hotuba zao kushawishi umma dhidi ya matendo ya ufisadi na vilevile walivyodhihirisha uwezo na mamlaka waliyo nayo katika juhudi za kupiga vita ufisadi. Ili kufafanua zaidi dhana ya hotuba za kisiasa, tumejadili sifa na mamlaka ya hotuba za kisiasa. Sifa za hotuba za kisiasa zimejadiliwa kwanza.

### 2.3.1 Sifa za Hotuba za Kisiasa

Kwa mujibu wa Randy (2021) hotuba za kisiasa zina sifa tano bainifu. Ya kwanza ni kuwepo kwa hoja ambazo hubeba taarifa za mhutubu. Mhutubu huzitetea hoja zake kwa njia ya kuzidhihirisha kuwa ni ukweli halisi. Sifa ya pili ni mkakati, yaani hushughulikia malengo ya hotuba, mbinu ya kuafikia na vizuizi ambavyo vinaweza kujitokeza. Sifa ya tatu ni utata. Hapa, mhutubu huzua utata kwa kumuingiza mpinzani wake katika suala husika ili kuamsha hisia fulani miongoni mwa wafuasi wake za kuona haja ya kujiunga naye ili kuikabili hatari iliyopo. Ya nne ni kutoa msimamo. Mwanasiasa huwa na msimamo fulani kuhusu suala husika ambalo hujitolea kulitetea au kufuata. Sifa ya tano ni ushawishi ambapo mhutubu wa kisiasa hulenga kuwashawishi wafuasi wake wala si adui zake kisiasa. Maelezo haya kuhusu sifa bainifu za hotuba za kisiasa yalikuwa ya umuhimu katika utafiti huu ambapo tulichanganua na kulinganisha jinsi hotuba za wanasiasa teule zilivyoangazia suala la ufisadi. Sifa hizi bainifu ziliweza kujitokeza katika baadhi ya hotuba mathalani, kuwepo kwa taarifa ambapo tulitambua kuwepo kwa hoja muhimu kuhusu vita dhidi ya ufisadi, kuibuliwa kwa utata kwa kuwaingiza wapinzani wao katika suala hili na kisha kutoa kwa misimamo yao.

Suala la uamuzi kuhusu hotuba nzuri ya kisiasa au mbaya hutofautiana miongoni mwa watu kwa mujibu wa Geiger (2016). Anadai kuwa hotuba moja iliyotolewa kwa hadhira moja huweza kufasiriwa kuwili; kuna wale wataiona kama hali ya kujidumaza kisiasa na wengine wakaiona kama hotuba nzuri ambayo ni nguzo muhimu ya kimaadili. Madai haya ya Geiger yalikuwa muhimu katika utafiti huu ambapo athari na mielekeo ya umma kuhusu

hotuba za wanasiasa teule kuhusu ufisadi zilichunguzwa kwa kuhakiki ufasiri wao wa hotuba hizo.

Aidha, Geiger (2016) anaeleza sifa tatu za hotuba nzuri. Sifa ya kwanza ni hadhira kumwamini mhutubu. Anafafanua kuwa ili ujumbe upokelewe vyema na hadhira, ni lazima mhutubu aaminiwe na hadhira yake. Kwa mfano, ujumbe sawa ukiwasilishwa na wahutubu wawili tofauti, ule uliowasilishwa na mhutubu anayeaminiwa utamakinikiwa na kupokelewa vyema na hadhira lakini ujumbe huo ukiwasilishwa na yule asiyeaminiwa hadhira itaupuuza. Sifa hii ilizingatiwa katika utafiti huu ambapo wanasiasa teule ambao hutuba zao ziliteuliwa ni wale ambao wanaaminiwa na wananchi sana. Sifa ya pili ni hali ya ujumbe kuwa wenye ukweli na kuaminika. Hotuba itahakikiwa kuwa nzuri iwapo inaangazia masuala yenye ukweli na ya kimantiki.

Kando na hayo, Geiger (2016) anadai kuwa, hotuba nzuri ni ile ambayo hutolewa kwa wakati na muktadha mwafaka na faafu. Ujumbe lazima ulenge uhalisia wa yale yanayotendeka katika jamii wakati huo. Sifa hii ya hotuba ilizingatiwa katika utafiti huu kwani hotuba lengwa ni zile ambazo ziliangazia suala la ufisadi nchini Kenya ambalo ni mojawapo ya masuala makuu yanayoathiri jamii ya Kenya kwa sasa.

Sifa ya mwisho ya hotuba nzuri ni hali ya mhutubu kuwa na shauku kuu kuhusu anachohutubu na wale anaowahutubia. Anasisitiza kuwa mhutubu ambaye anadhihirisha shauku kuhusu anachosema huifanya hadhira yake kumsikiliza kwa makini na kuupokea vyema ujumbe wake kwani yeye hudhihirisha kuwa anaamini anachokisema na

anawapenda pia. Sifa hii ilizingatiwa katika utafiti huu katika kuchanganua na kulinganisha namna hotuba za kisiasa zilivyoangazia suala la ufisadi kwa kurejelea hotuba za wanasiasa teule. Katika lengo hili, shauku ya mwanasiasa kuhusu anachoangazia katika hotuba yake ilihakikiwa kwa kuchunguza uteuzi wake wa maneno na sifa nyinginezo za ulumbi alizobainisha. Aidha, utafiti huu pia ulifaidi kutokana na sifa hii katika kuchunguza athari na mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi. Kando na sifa, sehemu ifuatayo inafafanua mamlaka katika hotuba hizi.

### 2.3.2 Mamlaka katika Hotuba za Kisiasa

Dhana ya mamlaka imefafanuliwa tofautitofauti na wataalamu katika taaluma mbalimbali; kwa mfano katika sosholojia, Giddens (2009) anafafanua mamlaka kama uwezo wa mtu au kikundi cha watu kutekeleza matakwa yao hata wanapopingwa na wenzao na pia kama uwezo wa kudhibiti tabia za wengine hata ikiwa ni kinyume na matakwa yao. Hapa anaonyesha kuwa mamlaka huibadili hali fulani inayoshuhudiwa kwa faida ya mwenye mamlaka katika jamii. Kwa upande mwingine, Wang (2006) anafafanua mamlaka katika matini kama uwezo wa kuongoza na kudhibiti wengine; uwezo wa kupata ulicholenga; uhuru wa kuafikia malengo yako na uwezo wa kuwafanya wengine kutenda au kutimiza matakwa yako. Ufafanuzi huu wa mamlaka ulifaidi utafiti huu katika kuchunguza na kulinganisha namna matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi yanavyoangazia suala la vita dhidi ya ufisadi. Hapa, mamlaka ya wanasiasa teule kupitia matini ya hotuba zao yalitathminiwa katika juhudi zao za kupambana na ufisadi nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Fairclough (1989), mamlaka hujikita katika mifumo mbalimbali. Mifumo hii ni matumizi ya nguvu au vurugu na mfumo wa makubaliano. Anadai kuwa mfumo ulio mgumu zaidi kufafanua au kutambua ni ule wa mamlaka yanayojengwa kwa makubaliano au unaoelekeza makubaliano. Anazidi kueleza kuwa lugha ni mojawapo ya mbinu ambazo huchangia na kuendeleza ukosefu wa usawa katika mamlaka na pia ni mbinu mojawapo inayoweza kutumiwa kutatua hali hii kwa sababu, kwa kutumia lugha hasa katika taasisi mbalimbali, mikataba huundwa na inapotumika kwa muda mrefu huamua tabia fulani ambazo zinaaminiwa kuwa sawa katika jamii. Maelezo haya ya Fairclough yaliufaidi utafiti huu kubaini nafasi ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa kutathmini lugha iliyotumiwa katika hotuba hizi. Hotuba za kisiasa zilichanganuliwa na kulinganishwa jinsi zilivyotumia lugha kuwarai wananchi kushirikiana katika vita dhidi ya ufisadi.

Uvehammer (2005) katika utafiti wake wa mbinu za kiisimu zinazotumiwa katika hotuba za kisiasa na namna zinavyotekeleza lengo la kushawishi wapiga kura; alibaini mbinu kadhaa ambazo wanasiasa hutumia kuafikia malengo yao. Baadhi ya hizi mbinu ni; maswali balagha, ulumbi, upole na propaganda. Anakubaliana na Mesthrie na wenzake (2000) kuwa lugha ya propaganda ni lugha ya ushawishi, ya kujenga mahusiano, uradidi na ya kuwasilisha uhalisia kwa njia rahisi. Hizi mbinu za kiisimu kama anavyoeleza Uvehammer zinalenga kuwashawishi wanaohutubiwa na wanasiasa kuwapigia kura. Ingawa katika utafiti huu hatukulenga kuchunguza ushawishi wa wanasiasa kwa dhima ya kupigiwa kura, mbinu za lugha zilizobainishwa na wataalamu hawa zilihakikiwa na kulinganishwa katika juhudi za kutathmini nafasi yake katika kushawishi umma kupiga vita ufisadi.

Randy (2021) anaeleza kuwa mazungumzo ya kisiasa yameamua hatima ya ubinadamu katika nyakati zinazochukuliwa kuwa za kihistoria leo. Anaongezea kuwa, hotuba za kisiasa ni zana muhimu kwa utendaji wa kisiasa kwa vile inatumiwa na wanasiasa kuelezea jinsi wanavyoona shida fulani, kuwaunganisha wapiga kura na malengo yao, kudadisi kuhusu matumizi ya mamlaka au kuipa hadhira yao matumaini. Huu uwezo wa hotuba za kisiasa unaoelezwa na Randy ni mojawapo wa malengo ya utafiti huu. Mtazamo wa wanasiasa teule kuhusu suala la ufisadi nchini Kenya na vita dhidi yake ulibainishwa na kulinganishwa kwa kuhakiki matini ya hotuba zao teule.

Kwa mujibu wa Wanyama (2022), wanasiasa katika hotuba zao hutumia uyahe na ragba ya kijinsia kama mkakati wa propaganda. Katika utafiti wake alibaini kuwa wanasiasa wengi hujihusisha na watu wenye mapato ya chini kwa kueleza kuhusu asili yao ambayo hudai kuwa ni duni. Kwa kufanya hivyo, hadhira yao ambayo asilimia kubwa ni maskini, huanza kujinasibisha nao kwani wanawaona kama maskini mwenzao. Kwa njia hii, maskini huanza kumpenda na kumwamini. Wanapomwamini wanamkubali na hivyo kuridhia yote anayowaambia. Maelezo haya ya Wanyama ya jinsi hotuba za kisiasa zinavyotumiwa kushawishi umma kuunga mkono wanayopendekeza kufanywa yalikuwa muhimu katika kutathmini jinsi wanasiasa wanavyohakikisha kuwa wanaaminiwa na wananchi ili waweze kuunga mkono juhudi zao za kupambana na ufisadi nchini Kenya.

Kwa misingi ya maelezo ya wataalamu mbalimbali tuliyojadili hapo juu, ni dhahiri kuwa lugha ina nafasi kubwa katika kujenga na kuendeleza mamlaka ya wanaohutubu. Katika

hotuba za kisiasa, wanasiasa hutumia lugha kujenga mamlaka yao katika jamii kwa kuendeleza itikadi zao. Ili kuweza kuchanganua vyema mwingiliano baina ya hotuba za kisiasa na suala la ufisadi, sehemu inayofuata inafafanua dhana ya hotuba za kisiasa na suala la ufisadi. Ili kubainisha nafasi ya hotuba za kisiasa katika jamii, sehemu ifuatayo inafafanua mielekeo na athari za hotuba za kisiasa.

## 2.4 Mielekeo na Athari za Hotuba za Kisiasa

Dhana ya mielekeo imeweza kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali ambao wanaibua mitazamo miwili mikuu. Mtazamo wa kwanza ni kuwa, mielekeo ni tukio la kiakili nao wa pili unafafanua mielekeo kama kitu kinachoweza kudhihirika kivitendo. Thomas (1971) akikubaliana na Agheyisi na Fishman (1970), anashikilia kuwa mwelekeo ni hali ya mtu kuwa tayari kutenda kitu fulani wala sio kitu kinachoweza kuonekana. Anasisitiza kuwa ili kubainisha mwelekeo wa mtu kuhusu kitu au jambo fulani, inambidi mtafiti kuelewa fikra za mtu huyo kupitia mbinu kama vile kuuliza maswali. Wataalamu hawa wanashikilia kuwa, hatuwezi kuchukulia anachofanya mtu kila mara kuwa ndicho anachoamini kwani watu hufanya mambo fulani kwa sababu tofauti. Kwa hivyo, njia bora zaidi ya kutambua mielekeo ya watu ni kupitia uelewaji wa fikra zao badala ya kutegemea vitendo wanavyofanya. Kwa misingi hii basi, mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi iliweza kubainishwa kupitia maswali kwenye hojaji ya likati ambayo yalisaidia kubainisha fikra zao kuzihusu.

Kwa upande mwingine, tamko la mzungumzaji huwa na athari (chanya au hasi) juu ya mawazo na hisia za hadhira. Hili hutokea tu iwapo hadhira itaelewa nia ya mzungumzaji

(Brown na Yule, 1993). Ingawa Crystal (1997) anakubaliana kwa kiasi fulani na madai haya, anashikilia kuwa kitendo dhamiriwa na kitendo athari huenda visipatane. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa hotuba inapotolewa huweza kuibua athari mbalimbali kwa hadhira lengwa ambazo zinawiana na dhamira ya mhutubu au zikakosa kuwiana.

Kwa mujibu wa Haji (2018), hotuba za kisiasa huibua athari mbalimbali miongoni mwa hadhira yake. Baadhi ya athari hizo ni; kushawishika kwa hadhira kuhusu suala fulani, kuhamasika ili kuchukua hatua fulani, kupuuza yanayostahili kupuuzwa, kufarijika kuwa hali itaimarika na kuwa sawa, kukasirika na kuudhika na maovu yanayotendeka, kujenga matumaini, kuzinduka, kuungama, kumakinika,kufurahika na kujiamini. Athari hizi za hotuba za kisiasa kwa mujibu wa Haji (keshatajwa) ziliweza kuzingatiwa katika utafiti huu kuhakiki athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya.Kwa sababu maudhui ya ufisadi pekee ndio yaliyolengwa katika hotuba za wanasiasa teule, uhusiano kati ya hotuba za kisiasa na ufisadi umeelezwa katika sehemu ifuatayo.

## 2.5 Hotuba za Kisiasa na Ufisadi

Ufisadi ni matumizi mabaya ya mamlaka kwa faida za kibinafsi kwa mujibu wa Benki Kuu ya Dunia (World Bank), Transparency International (T.I)[1] na shirika la maadili na kupambana na ufisadi nchini Kenya (EACC)[2].[3] Kwa kuzingatia kigezo cha kiwango cha

---

[1] Transparency International (T.I) ni shirika la kimataifa linaloongoza vita dhidi ya ufisadi duniani.
[2] Ethics and Anti Corruption Commission (EACC) ni shirika la maadili na kupambana na ufisadi nchini Kenya.
[3] Ufisadi ni matumizi mabaya ya mamlaka kwa faida za kibinafsi. Katika (World Bank, 1997; T.I, 2019; EACC, 2017).

pesa zilizopotea, T.I wanaweka ufisadi katika makundi matatu: ufisadi mkuu, ufisadi mdogo na ufisadi wa kisiasa.

Ufisadi nchini Kenya ni suala linaloangaziwa nchini na hata kimataifa kwa maana umeathiri watu wengi sana. Ni dhahiri kuwa ufisadi umekita mizizi na kuenea katika jamii pana ya ulimwengu na hivyo basi haihalisi kusema kuwa ufisadi nchini unahusishwa tu na viongozi wachache wasio waadilifu ambao wana mamlaka makuu nchini (Mogeni, 2009). Akirejelea maoni ya Wakenya, Wrong (2014) anakubaliana na madai haya ya Mogeni (keshatajwa) na kusisitiza kuwa kila mtu nchini Kenya ni fisadi; hata kina mama wakongwe zaidi. Anaongezea kuwa, huku kuenea sana kwa ufisadi nchini Kenya kunadhihirisha kuwa uongozi wa nchi umekumbwa na dosari. Kwa kauli hii ya Wrong, ni dhahiri kuwa wanasiasa wa upinzani na serikali lazima waangazie suala la vita dhidi ya ufisadi na hiyo ndio maana lengo la kwanza la utafiti huu ni kuchanganua na kulinganisha namna wanasiasa wanavyoangazia suala hili katika hotuba zao.

Licha ya kuwepo kwa tume ya kupambana na ufisadi nchini (EACC) na hatua nyingine nyingi ambazo zimechukuliwa ili kukabiliana na ufisadi, nchi ya Kenya bado imeorodheshwa miongoni mwa nchi fisadi sana duniani (TI, 2019). Hali hii basi ndio inawafanya viongozi wengi wa kisiasa kuangazia suala hili katika hotuba zao. Hivyo basi, mtafiti aliona ni muhimu kuweza kuchanganua na kulinganisha baadhi ya hotuba hizi ili kulinganisha zinavyoshughulikia suala la ufisadi pamoja na athari na mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba hizi.

Aidha, kwa kuwa ufisadi umekuwa donda ndugu katika nchi nyingi, suala hili halikosi kuangaziwa katika hotuba za wanasiasa hasa marais wa nchi mbalimbali katika hotuba zao kwa wananchi wa mataifa yao. Kwa mfano, rais wa Uchina Xi Jinping katika hotuba yake ya kwanza kwa taifa baada ya kuchukua mamlaka hakukosa kutoa ahadi yake kwa wananchi kuwa atapambana na ufisadi (DW Idhaa ya Kiswahili, 2013). Uchina ni taifa lenye nguvu za kiuchumi duniani lakini wao pia wanakabiliwa na tatizo la ufisadi na hii ndio sababu ya rais wao kuliangazia katika hotuba yake ya kwanza kwa taifa.

Hali kadhalika, katika mataifa mbalimbali, wananchi wanaamini ni lazima viongozi wao wa kisiasa hasa marais kuliangazia katika hotuba zao kwa taifa. Wanapokosa kufanya hivyo, wengi hukosa kuridhika na hotuba zao. Kwa mfano, nchini Ghana, wananchi walidai kutoridhika na hotuba ya rais Akufo Addo kwa kutogusia suala la ufisadi katika hotuba yake kwa taifa (The Fourth Estate, 2021)[4]. Nchini Kenya pia, hali ni ile ile; wananchi katika mitandao ya kijamii walimtaka Rais Uhuru Kenyatta kufafanua hatua madhubuti ambazo alikuwa amepanga kuchukua dhidi ya ufisadi katika hotuba yake bungeni kuhusu hali ya mambo nchini mwaka wa 2019 (BBC News Swahili, 2019)[5]. Baadaye, katika hotuba yake, Uhuru Kenyatta aliahidi kumtimua kazini waziri yeyote ambaye angepatikana na kesi ya kujibu kuhusiana na suala la ufisadi (Kenyans.co.ke, 2019).

[4] Wananchi wa Ghana wakosa kuridhika na hotuba ya Rais Addo kwa kukosa kuangazia suala la ufisadi. Katika The Fourth Estate (2021).

[5] Wananchi wamtaka rais Uhuru kutangaza hatua madhubuti za vita dhidi ya ufisadi katika hotuba yake bungeni. Katika BBC News Shwahili (2019).

### 2.6 Hitimisho

Sura hii ililenga kueleza kwa kina dhana ya matini ya hotuba za kisiasa ili kufafanua zaidi suala la utafiti. Imebainika kuwa kiisimu, matini ni matumizi ya lugha na ndio huunda na kujenga maana (Fairclough, 1992; Brown na Yule, 1993; Rodgers, 2005). Kwa sababu hii, dhana ya lugha, sifa, majukumu na uwezo wake umejadililiwa kwa kina.

Hotuba za kisiasa zimeweza kubainishwa katika vipengele vitatu; mhutubu, mhutubiwa na hotuba yenyewe. Aidha, imebainika kuwa katika uchanganuzi wa matini ya hotuba za kisiasa, ni lazima wanasiasa husika, wapokezi wa hotuba na matini ya hotuba yenyewe yaweze kuhakikiwa (Seidel, 1985; Van Dijk, 1997). Malengo ya utafiti huu yameweza kuangazia uchanganuzi wa vipengele vyote vitatu vya hotuba za kisiasa kwa mujibu wa wataalamu hawa. Hali kadhalika, sifa 5 bainifu za hotuba za kisiasa zimeweza pia kufafanuliwa kwa mujibu wa Randy (2021) kama ifuatavyo; kuwepo kwa taarifa, malengo, utata, msimamo na ushawishi. Anasisitiza kuwa dhima kuu ya hotuba za kisiasa ni kushawishi hadhira kuhusu suala fulani. Madai haya yanawiana na ya Ngure (2020) ambaye anashikilia kuwa hotuba za kisiasa hulenga kushawishi wanaohutubiwa na anasisitiza kuwa, ili hotuba iweze kutekeleza jukumu hili vyema ni lazima iwe na ukwasi wa tamathali za usemi. Sifa hizi bainifu zimetumiwa na mtafiti kikamilifu katika uchanganuzi na ulinganisho wa matini ya hotuba za kisiasa katika sura ya tatu na ya nne.

Aidha, mamlaka ya hotuba hizi za kisiasa yameweza kutathminiwa ambapo wataalamu mbalimbali wanaafikiana kuwa wanasiasa hutumia hotuba za kisiasa kujenga mamlaka yao katika jamii, kuendeleza itikadi zao na kueleza jinsi wanavyoona shida fulani na

kuwasilisha malengo yao kwa hadhira. Kwa sababu hii tatizo liwapo katika jamii, ni lazima wanasiasa waliangazie katika hotuba zao na wasipofanya hivyo wananchi hukerwa sana kama ilivyokuwa nchini Ghana. Kwa ujumla, maelezo haya ya kina kuhusu matini ya hotuba za kisiasa na ufisadi yalimpa mtafiti uwezo wa kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kuanzia mwaka wa 2015 hadi 2020 ili kubainisha namna wanasiasa wanavyoangazia tatizo la ufisadi katika nchi ya Kenya na kubainisha malengo yao.

# SURA YA TATU

# ULINGANISHAJI WA NAMNA MATINI ZA HOTUBA ZA KISIASA ZINAVYOSHUGHULIKIA UFISADI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, dhana ya matini ya hotuba za kisiasa ilijadiliwa kwa kina. Katika sura hiyo, ilibainika kuwa dhima kuu ya hotuba za kisiasa ni kushawishi hadhira lengwa. Ili kutekeleza jukumu hili ifaavyo, hotuba hizi huwa na ukwasi wa tamathali za usemi (Ngure, 2020, Randy, 2021). Hii ina maana kuwa, wanasiasa hutumia tamathali za lugha

miongoni mwa mbinu nyingine za ulumbi katika juhudi za kushawishi hadhira yao kuhusu itikadi zao au kufuata mtazamo wanaoushikilia kuhusu masuala mbalimbali katika jamii.

Katika sura ya kwanza, ilibainika kuwa miktadha ya matukio ni muhimu katika ufasiri wa maana katika matini. Ufasiri wa matini hufanywa kwa njia mbili muhimu. Njia ya kwanza ni ufasiri wa kawaida ambapo uchambuzi huzingatia wakati fulani maalum, mahali, na muktadha wa usemi. Njia ya pili ni ufasiri wa kiulinganishi ambapo kitu fulani kinalinganishwa na muktadha fulani. Uchanganuzi wa data katika sura hii uliegemea maoni haya. Ulinganishaji wa matini za hotuba za kisiasa baina ya rais wa nne wa Kenya, Uhuru Kenyatta na aliyekuwa waziri mkuu, Raila Odinga uliwezesha ufasiri wa ujumbe na ulidhihirisha matumizi ya istilahi maalum, viwakilishi vya nafsi, usawiri wa wananchi kama wenye mamlaka makuu, matumizi ya toni ya kejeli, lugha yenye takwimu, lugha yenye matumaini, toni ya kukashifu, kuchanganya msimbo, matumizi ya kinaya, matumizi ya takriri, matumizi ya maswali balagha na matumizi ya virai shawishi. Tutaanza kwa kulinganisha matumizi ya istilahi maalum katika matini za hotuba teule za viongozi hawa.

### 3.1 Istilahi Maalumu

Maneno ni mojawapo wa vipashio vya kimsingi vya lugha ambayo hubeba ujumbe muhimu wa mhutubu. Yeye huteua istilahi mwafaka kwa uzingatifu mkubwa ili kuibua athari iliyokusudiwa (Sekyi-Baidoo, 2002). Istilahi mbalimbali huweza kueleweka zikiwa pweke au kwa kuzingatia miktadha husika. Aidha, kwa mujibu wa Mills (1984), wanasiasa hutumia istilahi au msamiati unaowakilisha dhana fulani katika kampeni maalumu. Kwa kuzingatia misingi hii, tulihakiki istilahi mbalimbali zilizotumika kurejelea suala la ufisadi

na vita dhidi yake katika hotuba teule za kisiasa. Istilahi zilizohakikiwa zinajikita katika aina nane za maneno katika lugha ya Kiswahili. Zifuatazo ni baadhi ya istilahi zilizotumiwa kwenye hotuba teule za rais wa nne Uhuru Kenyatta na aliyekuwa waziri mkuu Raila Odinga kurejelea ufisadi na vita dhidi yake:

**Jedwali 3.1: Istilahi Maalumu**

| | **MANENO** | **HOTUBA** |
|---|---|---|
| 1. | ***Wizi:***<br>*Wakenya wanasema wale wote ambao walihusika na* ***wizi*** *hii, washikwe na washtakiwe*<br>*Mara ile nyingine niliongea juu ya mambo ya* ***wizi*** *katika idara ya NYS* | RO1<br><br>RO2 |
| 2. | **Wezi:**<br>wao ndio wa kwanza walianza kusafisha ***wezi***<br>Na mbona ***wezi*** wa mabilioni hawahukumiwi? | RO1<br><br>UK3 |
| 3. | **Mwizi:**<br>Wewe ni ***mwizi***! Wewe ni ***mwizi***! Ni ***mwizi!*** | UK1 |
| 4. | **Msalaba:**<br>Chukua ***msalaba*** yako wako peke yako! | UK1 |
| 5. | **Washikwe; washtakiwe**<br>wote ambao walihusika na wizi hii, ***washikwe*** na ***washtakiwe*** | RO1 |
| 6. | **Tutapambana; tutapigana**<br>…tuungane pamoja na tuseme ya kwamba ***tutapambana*** na **tutapigana** na ufisadi | UK3 |

Katika Jedwali 3.1, Raila alitumia neno *wizi* kurejelea dhana ya ufisadi. Kwa mujibu wa kamusi sanifu ya Kiswahili TUKI toleo la tatu (2013), nomino wizi linatokana na kitenzi iba chenye maana ya kuchukua kitu cha mwingine kwa siri bila ya ruhusa au haki. Hii ina maana kuwa ufisadi hutekelezwa kwa siri na huwahini wananchi ambao ni wamiliki halisi wa raslimali za nchi haki ya kuendelea kuzimiliki.

Aidha, Viongozi hawa wote walitumia istilahi *wezi* katika hotuba zao kurejelea mafisadi. Kwa kuwarejelea mafisadi kama wezi wa mali ya umma wanalenga kuwafanya wananchi wachukie mafisadi na vitendo vya ufisadi. Uhuru pia ametumia neno *mwizi* mara tatu kudhihirisha jinsi anavyochukia mafisadi. Hali kadhalika, ameitumia istilahi *'msalaba'* kurejelea ufisadi pia ambapo alilinganisha tendo la ufisadi na msalaba ambao ni mzito na humchosha mwenye kuubeba. Hii ina maana kuwa vitendo vya ufisadi huwatia wahusika matatizoni.

Aidha, Raila alitumia istilahi, *Washikwe* na *Washtakiwe* kurejelea namna ya kuwakabili mafisadi. Uhuru naye pia anaporejelea sakata ya mabwawa, anatumia istilahi, *tutapambana!* na *tutapigana!* kurejelea vita dhidi ya mafisadi.

Kwa ujumla, viongozi hawa wote wanatumia lugha kali kurejelea vitendo vya ufisadi na waliohusika katika vitendo hivyo. Kama anavyodai Lyons (1981) kuwa maana na uamilifu wa neno hutokana na matumizi yake na kujua neno ni kujua matumizi yake bali sio kutafuta maana yake, imebainika wazi kuwa viongozi hawa waliteua msamiati maalum kurejelea suala la ufisadi ili kusawiri uharibifu unaotokana na matendo ya ufisadi nchini Kenya.

Wanasawiri ufisadi kama tendo haramu na wanaoshiriki ufisadi kama wahalifu. Kama anavyoeleza Van Dijk (1998), watu wenye ushawishi katika jamii hulenga kuathiri imani za kijamii na maadili kupitia vigezo wanavyoviweka kuhusu kile ambacho wanaamini kinakubalika au hakikubaliki katika jamii; viongozi hawa mbali na ushawishi wao, wanatumia lugha kali kurejelea ufisadi na kukashifu mafisadi ili kuishawishi jamii kuwa ufisadi ni matendo yaliyo kinyume na maadili ya kijamii hivyo basi inastahili kuunga mkono juhudi za kupambana nao.

### 3.2 Matumizi ya Viwakilishi vya Nafsi

Katika sura ya pili iliwekwa wazi kuwa uchanganuzi wa matini hujikita katika uhakiki wa jinsi vipengele mbalimbali vya lugha vilivyotumika katika matini ya maongezi au yaliyoandikwa. Vilevile, ilibainika kuwa, matini huchunguzwa kwa undani ili kubainisha sababu ya matini kuwa jinsi yalivyo na pia kubainisha maana fiche (Martin na Rose 2003; Johnstone 2008). Kutokana na misingi hii basi, ulinganishaji wa matini ya hotuba teule ulidhihirisha matumizi ya viwakilishi vya nafsi mbalimbali. Tutaanza kwa kulinganisha matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza katika umoja na wingi.

Viwakilishi vya nafsi katika umoja na wingi huweza kudhihirika kama viwakilishi nafsi huru (mimi /sisi) au viwakilishi nafsi ambata (viambishi ‘ni-’/ ‘tu-’). Kwa mujibu wa Obiero (2017), matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza katika umoja huibua msisitizo mkuu katika usemi wa mhutubu. Aidha, huashiria kujitolea kwa mnenaji kutekeleza jambo fulani peke yake au kujisifu kwa juhudi zake katika kutekeleza jambo fulani. Kwa upande mwingine, matumizi ya viwakilishi hivi katika wingi huashiria ushirikiano wa mnenaji na

wengine katika utekelezaji wa jambo fulani.Viwakilishi hivi vya nafsi ya kwanza vimetumiwa katika hotuba teule za viongozi hawa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.2: Matumizi ya Viwakilishi Nafsi ya Kwanza Umoja na Wingi**

| | **Sentensi** | **HOTUBA** |
|---|---|---|
| 1. | *Na* ***mimi nilisema*** *eti huyo bibi Waiguru jina yake ilikuwa katika list of shame ambayo Uhuru alipeleka kule bungeni.* | RO2 |
| 2. | ***Ni****lisimamisha mawaziri wawili kazi ili uchunguzi ifanyike.* | RO3 |
| 3. | ***Mimi nilisema*** *tu ikiwa kuna maneno ambayo wewe umetajwa, ukae kando.* | RO3 |
| 4. | ***Mimi nimesema*** *ikiwa kama kuna ufisadi, kama kuna wizi, ichunguzwe kila mahali.* | *RO3* |
| 5. | ***Na mimi nawauliza*** *Wakenya tusiweke siasa kwa hii safari.* | UK3 |
| 6. | ***Tumesema*** *ya kwamba kutoka sasa, hatutaki kusikia mtu akitetea mwenzake ati mtu akiiba anasema ni kabila langu, ni dini yangu inadhulumiwa.* | *UK1* |
| 7. | *Sisi siku ya leo kama Wakenya wenzetu* ***tuungane*** *pamoja na tuseme ya kwamba* ***tutapambana*** *na* ***tutapigana*** *na ufisadi* ***tukiwa kitu kimoja.*** | *UK3* |

Katika Jedwali 3.2, Raila anatumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja ‘mimi’ katika sentensi *Na mimi nilisema eti huyo bibi Waiguru jina yake ilikuwa katika list of shame ambayo Uhuru alipeleka kule bungeni,* kudhihirisha kuwa yeye ndiye mwenye ufahamu kuwa Waiguru alikuwa miongoni mwa wale waliohusika katika ufisadi. Hapa pia anaibua sifa ya utata katika hotuba za kisiasa kwa mujibu wa maelezo ya Randy (2021) anapomtaja Uhuru ambaye ni mpinzani wake kisiasa. Kama alivyodai Randy kuwa mwanasiasa anapotaja mpinzani wake, huwa anaibua utata ambao huamusha hisia za wafuasi wake; hapa Raila anamkosoa Uhuru ili kuamsha hisia za wafuasi wake dhidi ya hatua ambazo Uhuru alikuwa amechukua kukabiliana na ufisadi. Kwa kurejelea sakata ya mabwawa, Raila anatumia kiambishi ‘ni’ katika sentensi *Nilisimamisha mawaziri wawili kazi ili uchunguzi ifanyike*, kurejelea hali ilivyokuwa hapo awali alipokuwa waziri mkuu ambapo alitumia mamlaka yake kuwasimamisha kazi mawaziri waliotajwa kuhusika katika ufisadi kama mkakati wa kukabiliana na ufisadi nchini. Anajaribu kudhihirisha kuwa ana suluhu la jinsi ya kukabili washukiwa wa ufisadi ambayo ni kuwasimamisha kazi ili uchunguzi ufanyike. Hali hii pia inabainika katika sentensi zifuatazo aliporejelea sakata ya mabwawa; *Mimi nilisema tu ikiwa kuna maneno ambayo wewe umetajwa, ukae kando* na *Mimi nimesema ikiwa kama kuna ufisadi, kama kuna wizi, ichunguzwe kila mahali.*

Uhuru vilevile ametumia nafsi hii ya kwanza katika umoja kurejelea juhudi zake katika vita dhidi ya ufisadi kama ifuatavyo; *Na mimi nawauliza Wakenya tusiweke siasa kwa hii safari.* Hii ina maana kuwa anawasihi Wakenya wakubaliane na mpango wake.Kwa upande mwingine, nafsi ya kwanza katika wingi hutumiwa kuonyesha kuwa mnenaji ana nia ya kushirikiana na hadhira yake au kikundi kingine kwa ajili ya kutekeleza jambo

fulani. Katika hotuba teule, ni Uhuru pekee aliyedhihirisha kutumia nafsi ya pili wingi katika hotuba zake. Kwa mfano, *Na mimi nawauliza Wakenya tusiweke siasa kwa hii safari.* Hapa anatumia kiambishi 'tu' kuonyesha kuwa ni suala la Wakenya wote yeye akiwa miongoni mwao. Aidha anatumia pia kiambishi hiki katika, *Tumesema ya kwamba kutoka sasa, hatutaki kusikia mtu akitetea mwenzake ati mtu akiiba anasema ni kabila langu, ni dini yangu inadhulumiwa*, kwa dhima hiyo hiyo. Anatumia kiwakilishi nafsi huru 'sisi' katika kauli; *Sisi siku ya leo kama Wakenya wenzetu tuungane pamoja na tuseme ya kwamba tutapambana na tutapigana na ufisadi tukiwa kitu kimoja.*

Kutokana na mifano hii, imebainika kuwa viongozi hawa wawili wametumia viwakilishi vya nafsi ya kwanza katika umoja kwenye hotuba zao kutilia msisitizo mkuu kama anavyobaini Obiero (2017), hali ambayo inalenga kuendeleza udhibiti wa mamlaka kama anavyodai Van Dijk (1998) kwani wanasawiri mikakati yao kama iliyo faafu zaidi katika vita dhidi ya ufisadi na hivyo kutaka jamii kuwaunga mkono. Kando na nafsi ya kwanza, hotuba teule za viongozi hawa zilisheheni viwakilishi vya nafsi ya pili kama ifuatavyo.

Katika sura ya pili, ilibainika kuwa, hotuba za kisiasa ni mojawapo ya hotuba ambazo mamlaka huweza kudhihirika. Hii ni kwa sababu lugha ya kisiasa hulenga kushawishi hadhira husika kwa madhumuni ya kudhihirisha mamlaka waliyo nayo au kujipa mamlaka (Chilton 2004; Chilton, Tian & Wodak 2012; Wodak 2015). Ni kwa misingi ya maelezo haya tulibaini kuwa, matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya pili katika umoja na wingi hudhihirisha hali ya mnenaji kuwasilisha ujumbe moja kwa moja kwa hadhira lengwa kwa nia ya kuwataka wawajibikie suala fulani. Hali hii imeweza kuwasilishwa katika jedwali

lifuatalo ambapo matini ya hotuba za viongozi teule yalilinganishwa kwa kuzingatia kigezo hiki.

**Jedwali 3.3: Matumizi ya Nafsi ya Pili**

| | **Sentensi** | **HOTUBA** |
|---|---|---|
| 1. | *Wewe uliiba peke yako, chukua msalaba yako, wako peke yako!* | *UK1* |
| 2. | *Si mnaona mambo yameanza kujitokeza?* | *UK 3* |
| 3. | *Ikiwa kuna maneno ambayo wewe umetajwa, ukae kando.* | *RO3* |

Katika Jedwali 3.3, Uhuru alitumia kiwakilishi nafsi 'wewe' katika sentensi, *Wewe uliiba peke yako, chukua msalaba yako, wako peke yako!* kukashifu waliohusika katika ufisadi na kusisitiza kuwa walifanya matendo ya ufisadi kibinafsi na wala si kama kikundi. Ili kuonyesha hali ya kuridhika na juhudi alizofanya, Uhuru anasema; *Si mnaona mambo yameanza kujitokeza?* Hapa anatumia kiambishi 'm-' katika neno 'mnaona' kulenga wananchi ambao alikuwa anawahutubia wakati huo. Hapa anadhihirisha shauku kuu kuhusu anachokisema kwa mujibu wa Geiger (2016) katika juhudi za kuwashawishi wananchi kusadiki kuwa hatua alizochukua kupambana na ufisadi zimeanza kuzaa matunda.

Raila pia anatumia hii nafsi ya pili anaposema, *Ikiwa kuna maneno ambayo wewe umetajwa, ukae kando,* akilenga kuwashutumu wale wote waliokuwa wametajwa kwa kuhusika katika sakata ya mabwawa kuwa watakabiliana na mkono wa sheria.

Ingawa Uhuru pekee ndiye aliyetumia nafsi ya pili katika wingi kurejelea wananchi wa Kenya, imebainika kuwa wanasiasa hawa wote wametumia viwakilishi vya nafsi ya pili katika umoja kukemea kila mmoja aliyehusika katika sakata za ufisadi na kuwataka

kupokea adhabu kwa mujibu wa sheria kama anavyodai Hakansson (2012) kuwa, matumizi ya kiwakilishi nafsi 'wewe' hudhihirisha kuwa mhutubu anawataka warejelewa kuwajibikia matendo yao. Kama anavyodai Van Dijk (1998) kuwa watu wenye ushawishi katika jamii hutumia uwezo wao kuamua kinachokubalika na kisichokubalika katika jamii, viongozi hawa wamekashifu mafisadi hadharani kama mkakati wa kudhihirishia umma kuwa ufisadi haufai katika jamii na vilevile kuwashawishi kuamini juhudi zao katika vita dhidi ya ufisadi.

Kando na viwakilishi vya nafsi ya pili, matini ya hotuba za viongozi hawa yalisheheni viwakilishi vya nafsi ya tatu kwa kiasi fulani. Matumizi ya Viwakilishi vya nafsi ya tatu huonyesha kuwa mnenaji haathiriki moja kwa moja na matendo ya mtu au watu hao. Yeye hujaribu kujitenga na kundi husika kama anavyodai Hakansson (2012). Katika hotuba teule, wanasiasa hawa wametumia mbinu hii kama ifuatavyo.

**Jedwali 3.4: Matumizi ya Nafsi ya Tatu Wingi**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| ***1.*** | *Siku zao zimehesabika na shida watapata.* | *UK1* |
| ***2.*** | *Wale wote ambao walihusika na wizi hii washikwe na washtakiwe* | *RO1* |
| ***3.*** | *Mawaziri watano walikuwa wameachishwa kazi, waliambiwa wakae kando.* | *RO2* |

Katika Jedwali 3.4, Uhuru akirejelea sakata ya NYS anatumia kiambishi cha nafsi ya tatu 'wa-' katika sentensi; *Siku zao zimehesabika na shida <u>wa</u>tapata*, kujitenga na washukiwa wa matendo ya ufisadi. Raila naye pia anatumia kiambishi hiki katika sentensi zifuatazo; ya kwanza ni, *<u>Wa</u>le wote ambao walihusika na wizi hii <u>wa</u>shikwe na <u>wa</u>shtakiwe.* Sentensi ya pili ni, *Mawaziri watano <u>wa</u>likuwa <u>wa</u>meachishwa kazi, <u>wa</u>liambiwa wakae kando,*

ambapo anatumia kiambishi cha nafsi ya tatu 'wa-'. Katika sentensi hizi mbili, kama alivyofanya Uhuru, Raila anatumia nafsi ya tatu kujitenga na matendo ya wahusika anaowarejelea katika hotuba yake.

Kwa ujumla, wanasiasa hawa wote walitumia nafsi ya tatu ili kuwasuta mafisadi kuubeba msalaba wao kwa kujihusisha na matendo haramu ya wizi wa mali ya umma. Walidhihirisha kuwa wao hawakuwa na uhusiano wowote na wezi wa mali ya umma na hivyo basi mafisadi walionywa dhidi ya kutarajia wao kuwakomboa wanapokabiliwa kwa mujibu wa sheria. Sehemu ifuatayo italinganisha matumizi ya mtindo wa kuwasawiri wananchi kama watu walio na mamlaka makuu ya kujiamulia wanayotaka katika jamii yao.

### 3.3 Kuwasawiri Wananchi kama wenye Mamlaka Makuu

Dhana ya mamlaka ilifafanuliwa katika sura ya pili kama uwezo wa mtu au kikundi cha watu kutekeleza matakwa yao kwa kuwadhibiti wengine au kuwafanya wengine kutenda jambo fulani ili kutimiza matakwa yao (Giddens 2009; Wang 2006). Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, ulinganishaji wa matini ya hotuba ulibainisha mtindo wa wanasiasa kuwasawiri wananchi kama wenye mamlaka makuu katika jamii. Kwa kutumia mtindo huu, wanasiasa hujitafutia mamlaka kwa kuwashawishi wananchi kuamini kuwa wao ndio waamuzi wa mustakabali wa maisha yao wenyewe. Katika hotuba teule za wanasiasa hawa, ilibainika kuwa walitumia mbinu hii kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.5 Usawiri wa Wananchi kama wenye Mamlaka Makuu**

| | Sentensi | Hotuba |
|---|---|---|
| 1. | *Wakenya wanasema wale wote ambao walihusika na wizi hii washikwe na washtakiwe.* | *RO1* |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini. Wewe unatoka unaendelea kuzunguka kuharibu ma cases huko. Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you!* | UK3 |

Katika Jedwali 3.5, Raila akirejelea sakata ya NYS anasema kuwa, *Wakenya wanasema wale wote ambao walihusika na wizi hii washikwe na washtakiwe.* Hapa anatumia neno *Wakenya* kumaanisha kuwa huo ndio uamuzi wa wananchi wote na hivyo basi unastahili kutiliwa maanani. Aidha, Uhuru anasema, *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini. Wewe unatoka unaendelea kuzunguka kuharibu ma cases huko. Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you!* Kwa kutumia *Wakenya* katika kauli hizi, anadhihirisha vilevile kuwa wananchi wanataka kuona utekelezaji wa haki mahakamani; hawataki tena kuendelea kushuhudia utepetevu katika taasisi hii. Anasisitiza kauli hii anaposema *Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you! (*Wakenya wamechoka! Na Wakenya wanawatazama! Wakenya wanawatazama!).

Imebainika kuwa viongozi hawa wote walitumia kauli *Wakenya* kama mbinu ya kuwafanya wananchi kuonekana kuwa wenye usemi zaidi kuhusu masuala yanayohusu vita dhidi ya ufisadi. Aidha, wanatumia mbinu hii kushawishi umma kuwaunga mkono kama wanavyodai Klebanov na wengine (2008) na Niedrich (2011) kuwa hotuba ya kisiasa kimsingi hutumiwa kuwashawishi watu, kuwabembeleza, kuwafurahisha na kujipa mamlaka. Isitoshe, kwa mujibu ya madai ya Crystal (1997) kuwa usemi hunuiwa kuathiri matukio katika jamii, kauli za wanasiasa hawa zinalenga kuwazindua na kuwachochea

wananchi kujitokeza na kuunga mkono vita dhidi ya ufisadi. Kando na mbinu ya kuwarejelea wananchi kama wenye mamlaka makuu, toni ya mazungumzo katika matini ya hotuba teule ilichunguzwa. Toni ya kejeli iliweza kulinganishwa katika sehemu ifuatayo.

### 3.4 Matumizi ya Toni ya Kejeli

Kwa mujibu wa Roberts (1995), toni ni neno linalorejelea mbinu ambazo waandishi na wazungumzaji hutumia ili kuonyesha mitazamo au hisia zao kuhusu kitu, jambo au hali fulani. Gray (1984) naye anasisitiza kuwa toni hutokana na aina za sentensi na msamiati anaotumia mzungumzaji au mwandishi. Kejeli ni tendo au hali ambayo ni kinyume ya matarajio (Wamitila, 2003b). Hivyo basi, toni ya kejeli ni matumizi ya kauli, msamiati au sentensi ambazo zinadhihirisha hisia zinazoonyesha kuwa jambo limetendeka kinyume na matarajio ya jamii. Viongozi hawa wametumia mbinu hii katika hotuba teule wakiangazia jinsi vita dhidi ya ufisadi vinatekelezwa na taasisi zinazostahili kuhakikishia wananchi haki kama inavyodhihirika katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.6: Matumizi ya Toni ya Kejeli**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.* | UK3 |
| 2. | *Lakini ile tume ya Anti- Corruption Commission yenyewe yatakikana isafishwe. Maanake wao ndio wa kwanza walianza kusafisha wezi. Walisema wezi walikuwa hawana hatia.* | RO1 |

Katika Jedwali 3.6, Uhuru anasema, *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu*

*hamsini*. Kauli hii inakejeli utepetevu wa mahakama kwa kukosa kuwapa wananchi haki wanapopelekewa washukiwa wa wizi wa mali ya umma. Raila naye vilevile anakejeli tume ya maadili na kupambana na ufisadi nchini Kenya (EACC) katika kifungu hiki cha maneno; '*Lakini ile tume ya Anti- Corrupion Commission yenyewe yatakikana isafishwe. Maanake wao ndio wa kwanza walianza kusafisha wezi. Walisema wezi walikuwa hawana hatia.* Anakejeli tume hii kwa kuwaondolea mashtaka washukiwa wakuu wa ufisadi anaposema kuwa, …*walianza kusafisha wezi. Walisema wezi hawana hatia.*Hapa kwa toni ya kejeli anasisitiza kuwa ni muhimu tume hii kupigwa msasa kwani hawatekelezi majukumu yao ipasavyo.

Kama anavyodai Ngure (2020) kuwa tamathali za usemi huzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisia na mawazo yake na pia kumfanya aone hali halisi ya mambo, viongozi hawa wote waliitumia tamathali hii ya usemi kuwazindua wananchi kujua hali ilivyo katika taasisi hizi. Aidha, walilenga kuwasuta wanaohudumu katika taasisi husika kwa utepetevu ili kuhimiza uwajibikaji. Kwa njia hii wanatumia uwezo wao katika jamii kuathiri hali ya utendakazi wa taasisi hizi na hivyo kuafikiana na madai ya Van Djik (1998) kuhusu udhibiti wa mamlaka kupitia matini. Mbinu nyingine muhimu ambayo ililinganishwa katika matini ya hotuba za kisiasa ni matumizi ya lugha yenye takwimu katika ufafanuzi wa masuala mbalimbali.

### 3.5 Lugha yenye Takwimu

Lugha ya takwimu ni lugha yenye data zinazoelezea na kufafanua masuala mbalimbali kwa mahesabu (Sovu, 2018). Kwa mujibu wa Van Dijk (1988) takwimu hutumiwa

kuonyesha usahihi na umuhimu wa ujumbe unaowasilishwa. Hii ina maana kuwa maalezo hupata uzito zaidi yanapoambatana na takwimu. Kwa kurejelea hotuba teule, viongozi hawa wametumia takwimu kama ilivyowasilishwa kwenye jedwali lifuatalo:

**Jedwali 3.7: Lugha yenye Takwimu**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Milioni 800 imeibwa* | *RO2* |
| 2. | *Wameiba zaidi ya shilingi bilioni moja* | *RO2* |
| 3. | *Kandarasi ilikuwa igharimu shilingi bilioni 27 na ukiweka pamoja 61 na tiyari bilioni 20 imeshalipwa na hata jembe haijagusa mchanga* | *RO3.* |
| 4. | *FBI wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. 800 bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka! Bilioni laki nane!* | *RO 3* |
| 5. | *Mbona wezi wa mabilioni hawahukumiwi?* | UK3 |
| 6. | *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.* | UK 3 |

Katika Jedwali 3.7, takwimu za kiasi cha pesa zilizoibwa zimetajwa na wanasiasa hawa hasa Raila katika, kauli; *Milioni 800 imeibwa* na *Wameiba zaidi ya shilingi bilioni moja.*

Anatoa kauli hizi kuweka wazi pesa za umma zilizoibwa katika shirika la huduma kwa vijana la NYS. Hali kadhalika, kuhusu sakata ya mabwawa ya Arror na Kimwarer anaeleza, *Kandarasi ilikuwa igharimu shilingi bilioni 27 na ukiweka pamoja 61 na tayari bilioni 20 imeshalipwa na hata jembe haijagusa mchanga*. Hapa pia anatumia takwimu kuweka wazi kiasi cha pesa zilizoibwa ili wananchi waweze kuelewa uzito wa madai anayotoa. Aidha, anaeleza faida za kuangamiza ufisadi anaposema, *FBI wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. 800 bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka! Bilioni laki nane!* Ingawa katika kauli hii anajaribu kuonyesha kuwa huenda wananchi wakapata mbivu iwapo ufisadi utakabiliwa, ni dhahiri kuwa takwimu anazotumia zinaonyesha kuwa wananchi wanapoteza fedha nyingi sana kupitia ufisadi kila mwaka- *shilingi bilioni laki nane*.

Uhuru pia anatumia takwimu katika kifungu, *Mbona wezi wa mabilioni hawahukumiwi? Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba* ***bilioni moja*** *akienda anapatiwa bail ya* ***shilingi elfu hamsini,*** kukejeli hali ya utepetevu wa mahakama katika kukabili mafisadi wakuu nchini. Wanaachiliwa kwa kutoa dhamana kidogo sana kama shilingi elfu hamsini pekee ilhali wameiba kiasi kikubwa cha pesa kama vile shilingi bilioni moja.

Kutokana na kauli zilizoangaziwa hapo juu, ni dhahiri kuwa viongozi hawa bila shaka wanatumia takwimu kujenga taswira halisi ya msiba unaowakabili Wakenya kutokana na ufisadi. Isitoshe, kama anavyodai Van Djik (1988) wanatumia takwimu kuonyesha usahihi na umuhimu wa ujumbe wanaotoa kwa wananchi. Kwa kufanya hivyo, wanapania kuwapa

wananchi msukumo wa kuwaunga mkono katika mapambano dhidi ya ufisadi hivyo basi kudhibiti mamlaka kupitia matini kwa misingi ya madai ya Van Djik (1998). Hata hivyo, kando na lugha ya takwimu na toni ya kejeli, lugha ya matumaini na ahadi iliweza kulinganishwa katika matini ya hotuba teule.

### 3.6 Lugha yenye Matumaini

Kwa sababu ya hali ya kutamausha ambayo wananchi wanakabiliwa nayo kutokana na kuibiwa kwa mali ya umma na mafisadi, viongozi hawa wanatumia lugha ya ahadi ili kuwapa matumaini kuwa wezi watakabiliwa na mabadiliko kushuhudiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.8: Matumizi ya Lugha yenye Matumaini**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Na tumesema hiyo mali yote ambayo watu wamenyakua, tutahakikisha imerudishwa, ndio itusaidie kujenga barabara na kupatia watu maji kulingana na vile tulikuwa tumepanga.* | UK1 |
| 2. | *Mimi nilipokuwa waziri mkuu ile wakati ingine. Unaweza kukumbuka nilisimamisha mawaziri wawili kazi ili uchunguzi ifanyike.* | RO3 |

Katika Jedwali 3.8, Uhuru akirejelea sakata ya NYS anasema, *Na tumesema hiyo mali yote ambayo watu wamenyakua, tutahakikisha imerudishwa, ndio itusaidie kujenga barabara na kupatia watu maji kulingana na vile tulikuwa tumepanga.* Raila naye pia anaonekana kuwapa wananchi matumaini kuwa mafisadi watakabiliwa kwa mujibu wa sheria iwapo watafuata hatua alizochukua dhidi ya mafisadi alipokuwa waziri mkuu. Anasema, *Mimi nilipokuwa waziri mkuu ile wakati ingine. Unaweza kukumbuka nilisimamisha mawaziri*

*wawili kazi ili uchunguzi ifanyike.* Anatumia kauli hizi kusisitiza kuwa mtindo huu ndio faafu kukabiliana na suala hili.

Ni dhahiri kuwa wanasiasa hawa wawili wanatumia lugha yenye matumaini kwa wananchi kuwa, wanayo mikakati ya kuhakikisha kuwa vita dhidi ya ufisadi vinafaulu. Kwa kufanya hivyo, wanalenga kuifanya hadhira yao kuwaamini ndiposa ujumbe wao upokelewe vyema kama aanavyodai Geiger (2016) kuwa ni lazima mhutubu aaminiwe na hadhira ndipo ujumbe wake upokelewe vyema. Aidha, kama anavyodai Van Djik (1998) kuwa imani za watu kuhusu ulimwengu inatokana na matini, wanasiasa hawa wanatumia matini ya hotuba zao kuwapa wananchi matumaini kuwa ufisadi unakabiliwa kupitia juhudi zao. Kwa njia hii basi, wanapania kudhibiti mamlaka. Licha ya hotuba hizi kusheheni lugha ya matumaini na ahadi kwa wananchi, matumizi ya toni ya kukashifu iliweza kulinganishwa pia.

## 3.7 Toni ya Kukashifu

Huu ni mtindo ambao mnenaji hukemea watu/kikundi cha watu au matendo fulani katika jamii. Ni kawaida kwa matendo yasiyofaa katika jamii kukashifiwa na viongozi kama njia ya kukosoa hali hiyo. Kwa mujibu wa utafiti huu, viongozi hawa wamedhihirisha toni ya kukashifu katika kauli zifuatazo kwenye jedwali:

**Jedwali 3.9: Toni ya Kukashifu**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Lakini ile tume ya Anti- Corruption Commission yenyewe yatakikana isafishwe! Maanake wao ndio wa kwanza walianza kusafisha wezi. Walisema wezi walikuwa hawana hatia.* | *RO1* |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini. Wewe unatoka unaendelea kuzunguka kuharibu ma cases huko. Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you! Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching!* | *UK3* |

Katika Jedwali 3.9, Viongozi hawa wanakashifu taasisi muhimu katika vita dhidi ya ufisadi kwa utepetevu wake. Raila anakashifu tume ya kupambana na ufisadi (EACC) kuwa ni watepetevu kazini anaposema *walianza kusafisha wezi. Walisema wezi walikuwa hawana hatia* naye Uhuru anakashifu idara ya mahakama kwa kuachilia washukiwa wa ufisadi. Kwa kukashifu taasisi hizi, viongozi hawa wanalenga kudhihirishia umma kuwa taasisi hizi ndizo zinazohujumu vita dhidi ya ufisadi. Kwa kufanya hivyo wanaamini kuwa taasisi hizi zitajizatiti ili kuepuka kuendelea kulaumiwa na viongozi hawa na Wakenya kwa ujumla. Hii inadhihirisha kuwa kuna mamlaka katika matini ya viongozi kwa jamii kama anavyodai Crystal (1997).Sehemu ifuatayo imejadili na kulinganisha mbinu ya kuchanganya na kubadili msimbo katika hotuba teule.

### 3.8 Kuchanganya Msimbo

Kuchanganya msimbo ni mbinu ya kutumia maneno ya lugha tofauti katika maelezo ambayo mnenaji anayatoa kwa lugha fulani. Kwa mfano kuingiza maneno ya Kiingereza katika maelezo ya Kiswahili (Areba, 2017). Hivyo basi, kuchanganya msimbo ni mbinu ya kuchopeka maneno ya lugha nyingine katika usemi ulio katika lugha tofauti. Dhima ya mtindo huu ni kutaka kueleweka vyema, kusisitiza ujumbe, kutaka kujitambulisha na hadhira husika au kufidia msamiati wakati mhutubu anakosa msamiati mwafaka katika

lugha husika. Jedwali lifuatalo, linawasilisha baadhi ya mifano ya mbinu za kuchanganya msimbo iliyotumiwa kwenye matini za hotuba teule.

**Jedwali 3.10: Kuchanganya Msimbo**

| | Sentensi | Hotuba |
|---|---|---|
| *1.* | *FBI, wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. Eight hundred bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka! Bilioni laki nane!* | *RO3* |
| *2.* | *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa* ***bail*** *ya shilingi elfu hamsini. Wewe unatoka unaendelea kuzunguka kuharibu ma* ***cases*** *huko.* | *UK3* |

Katika Jedwali 3.10, uchanganyaji msimbo katika matini za hotuba teule ulihusisha matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika kufanikisha mawasiliano. Raila alitumia mbinu ya kuchanganya msimbo katika kauli, '*FBI wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. Eight hundred bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka! Bilioni laki nane!'* Alitumia lugha ya Kiingereza kutaja kiasi cha pesa zinazoibwa (*Eight hundred bilion shillings)* baada ya kutaja kwa lugha ya Kiswahili ili kuhakikisha kuwa kiwango cha pesa alichokirejelea kimeeleweka vyema zaidi na hadhira yake. Hali kadhalika, Uhuru anatumia mtindo huu kwa kupachika neno *bail* katika sentensi ya Kiswahili. *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa* ***bail*** *ya shilingi elfu hamsini.* Kwa mujibu wa kauli hii, Uhuru anachanganya msimbo kwa kutumia neno *bail* ama kwa kukosa msamiati mwafaka kama wanavyodai Odeo na Maina

(2008) au kwa kutaka kueleweka vyema zaidi kwa maana neno hili linaeleweka vyema na wengi katika lugha ya Kiingereza.

Kwa ujumla, imebainika kuwa viongozi hawa wote wametumia mbinu ya kuchanganya msimbo katika hotuba zao kuhusu suala la ufisadi ili kusisitiza ujumbe wao na kutaka kueleweka vyema zaidi. Walilenga kuwafanya wananchi kuelewa jinsi ufisadi unavyoathiri nchi yao ili wawaunge mkono katika juhudi zao za kuukabili. Kwa njia hii wanadhihirisha udhibiti wa mamlaka kwa mujibu wa Van Dijk (1998). Mbinu ya kinaya pia iliweza kulinganishwa katika matini za hotuba teule.

### 3.9 Matumizi ya Kinaya

Kinaya ni mbinu ambayo matukio hudhihirika kuwa kinyume na matarajio. Kwa mujibu wa Wamitila (2008), mbinu hii hujengwa kwenye msigano au mgongano kati ya hali halisi na matarajio ya wanaohusika. Mbinu hii hulenga kumfanya msikilizaji au msomaji kufikiria kuhusu jambo fulani ili kubaini kuwa limetekelezwa kinyume na inavyostahiki. Mbinu hii imetumiwa katika hotuba teule za viongozi hawa wa kisiasa ili kusuta taasisi zinazohusika na vita dhidi ya ufisadi kwa utepetevu kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.11: Matumizi ya Mbinu ya Kinaya**

| | **Sentensi** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Walisema wezi walikuwa hawana hatia*’ na ‘*Wao ndio kwanza walianza kusafisha wezi.* | RO1 |
| 2. | *Mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.* | UK3 |

Katika Jedwali 3.11, Raila akirejelea utepetevu wa EACC katika sakata ya NYS anaeleza kuwa, *Walisema wezi walikuwa hawana hatia* na *Wao ndio kwanza walianza kusafisha wezi.* Hapa, anasema kuwa EACC walidai kuwa walioiba pesa za umma hawana hatia. Kwa kutumia kauli hii, anakejeli utendakazi wa EACC na hivyo kuwasuta wawe wawajibifu. Uhuru naye pia anatumia mbinu ii hii kukejeli utendakazi wa mahakama anapoeleza, *Mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.* Kwa kauli hii, anadhihirishia mahakama kuwa wananchi wanatarajia kuona mahakama ikiadhibu wezi wakuu kwa njia inayostahili na wala si kuwahukumu wanyonge tu na kutoshughulikia wezi wakuu.

Imebainika kuwa wanasiasa hawa wawili walitumia mtindo wa kinaya kusuta utepetevu katika taasisi zinazohusika na vita dhidi ya ufisadi. Kwa kutumia mbinu hii, wamesawiri tabia za wanaohudumu katika taasisi husika kama wasiowajibikia vita dhidi ya ufisadi. Aidha, wameweza kuwazindua wananchi katika kubaini hali halisi ya mambo kama anavyodai Ngure (2020). Matumizi ya mbinu ya takriri iliweza pia kubainika katika matini za hotuba teule na kulinganishwa kwa kina katika sehemu inayofuata.

### 3.10 Matumizi ya Takriri

Kwa mujibu wa Wamitila (2004), takriri ni urudiaji wa silabi, neno, vifungu au mistari. Tannen (1989) anaeleza kuwa takriri katika matini humsaidia mzungumzaji kuendeleza usemi kama bado anafikiria jambo la kusema. Mara nyingi ukariri unatokea pale ambapo msikilizaji hajaelewa hoja fulani. Aidha, Atieno (2016) anaeleza kuwa takriri hutumiwa kusisitiza au kutilia mkazo hoja fulani ili ieleweke vyema.

Viongozi hawa wawili wameitumia mbinu hii ya kimtindo kufanikisha mawasiliano yao kama ifuatavyo.

**Jedwali 3.12: Matumizi ya Takriri**

| | **Takriri** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Si nilisema? Si nilisema?* | *RO1* |
| 2. | *FBI, wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. Eight hundred bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka! Bilioni laki nane!* | *RO3* |
| 3. | *Wewe ni mwizi! Ni mwizi!* | *UK1* |
| 4. | *Wewe unatoka unaendelea kuzunguka kuharibu ma cases huko. Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you!* | *UK3* |

Kwa mujibu wa Jedwali 3.12, Raila anatumia mbinu hii anaposema, *Si nilisema? Si nilisema?* Kusisitiza kuwa alikuwa amekwisha taja washukiwa wakuu wa wizi katika shirika la huduma kwa vijana la NYS hapo awali japo hawakumwamini lakini sasa wengi wamesadiki aliyowaambia. Swali hili linanuiwa kuwafanya wananchi kumuamini kwani aliyoyasema yamebainika wazi kwao. Vilevile, katika kifungu, *FBI, wamesema Wakenya wakiweza kuzuia ufisadi wanaweza kusave shilingi bilioni laki nane. Eight hundred bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi. Kila mwaka!Bilioni laki nane!* Ametumia mbinu hii ya takriri kama ilivyobainika katika kauli zilizopigiwa mstari kwa nia ya kusisitiza hali ya nchi kupoteza fedha nyingi sana kupitia ufisadi kila mwaka.

Aidha, Uhuru ametumia mbinu hii ya takriri anaposema, *Wewe ni mwizi! Ni mwizi!* kusisitiza kuwa mafisadi ni wezi wa mali ya umma. Akirejelea sakata ya mabwawa ya

Arror na Kimwarer anatumia pia mbinu hii anaposema, …*Kenyans are tired! And Kenyans are watching you! Kenyans are watching you!* ili kuwanyooshea kidole cha lawama majaji katika mahakama kwa utepetevu. Kwa kufanya hivyo pia ni mkakati wa kujiondolea lawama ili wananchi wajue kosa si lake bali ni la mahakama.

Kutokana na uchanganuzi wa matini hapo juu, ni bayana kuwa wanasiasa hawa hutumia mbinu ya takriri kusisitiza kuwa ufisadi upo nchini na kuna haja ya kuwajibika kwa taasisi mbalimbali ili kuukomesha. Isitoshe, kutokana na matumizi ya mbinu hii, imebainika kuwa wanasiasa hawa wanatumia mbinu hii kujiondolea lawama ili kuwafanya wananchi kuwaamini ili ujumbe wao ukubalike kama anavyodai Geiger (2016). Aidha, kwa kuwa viongozi hawa ni watu wenye ushawishi katika jamii, wanalenga kushawishi imani ya wanajamii kuwa ufisadi ni adui wa Wakenya. Kwa njia hii wanadhibiti mamlaka kwa mujibu wa wa Van Dijk (1998). Mbali na takriri, maswali balagha yalipewa nafasi katika hotuba teule za viongozi hawa. Sehemu ifuatayo imelinganisha matumizi yake katika hotuba za viongozi teule.

### 3.11 Matumizi ya Maswali Balagha

Maswali balagha ni maswali ya kawaida ambayo hayahitaji majibu (Mogambi, 2012). Anazidi kufafanua kuwa nia ya maswali haya huwa ni kuzindua wasikilizaji au wasomaji ili kufikiria zaidi kuhusu yanayorejelewa. Wamitila (2008) naye anafafanua maswali balagha kama mbinu ya kutumia maswali yasiyohitaji majibu kwa vile majibu yake yako wazi. Katika hotuba teule, maswali balagha yafuatayo yalitumiwa:

**Jedwali 3.13: Matumizi ya Maswali Balagha**

| | **Maswali Balagha** | **Hotuba** |
|---|---|---|
| 1. | *Kandarasi ilikuwa igharimu shilingi bilioni 27 na ukiweka pamoja 61 na tiyari bilioni 20 imeshalipwa na hata jembe haijagusa mchanga. Pesa ambayo imelipwa imeenda kufanya kazi gani?* | *RO3* |
| 2. | *Si mpaka tu uchunguzi ifanywe?* | *RO3* |
| 3. | *Maanake kama wewe ni waziri wa maji si ndio unahusika? Si wewe ndio ulilipa? Wewe ndio unajua ulilipa kwa sababu gani? Ulilipa kiasi gani?* | *RO3* |
| 4. | *Mali hii yote ametoa wapi?* | *UK3* |
| 5. | *Mbona wezi wa mabilioni hawahukumiwi?* | *UK3* |
| 6. | *Si mnaona mambo yameanza kujitokeza?* | *UK3* |
| 7. | *Chukua msalaba yako wako peke yako! Au namna gani wenzangu?* | *UK1* |

Katika Jedwali 3.13, Raila akirejelea ubadhirifu wa pesa katika sakata ya mabwawa ya Arror na Kimwarer anasema, *Kandarasi ilikuwa igharimu shilingi bilioni 27 na ukiweka pamoja 61 na tiyari bilioni 20 imeshalipwa na hata jembe haijagusa mchanga. Pesa ambayo imelipwa imeenda kufanya kazi gani?* Hapa alikuwa akirejelea shilingi bilioni ishirini ambazo zilikuwa zimekwisha lipwa kwa mwanakandarasi katika sakata ya mabwawa japo hakuna kazi aliyokuwa amefanya baada ya kupewa pesa hizo. Anataka wananchi kuelewa kuwa pesa za umma zimeibwa. Anaeleza pia *Si mpaka tu uchunguzi ifanywe?* akiwataka wananchi kushawishika kuwa waliotajwa katika sakata hii wanastahili kuchunguzwa ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Aidha, katika maswali *Maanake kama wewe ni waziri wa maji si ndio unahusika? Si wewe ndio ulilipa? Wewe ndio unajua ulilipa kwa sababu gani? Ulilipa kiasi gani?*Anawataka wananchi kuelewa kuwa ni muhimu kwa waziri wa maji kuchunguzwa kwa sababu ni wizara yake ilihusishwa na wizi wa pesa za umma.

Vilevile, Rais mstaafu Uhuru Kenyatta naye katika sakata hii, anaibua maswali balagha kama vile *Mali hii yote ametoa wapi?* na *Mbona wezi wa mabilioni hawahukumiwi?* Swali la kwanza lililenga kuwafanya wananchi kutafakari na kutambua kuwa kuna wale ambao mali waliyo nayo waliipata kwa njia ya wizi. Swali la pili nalo lililenga kuwajuza wananchi kuwa mafisadi wakuu hawahukumiwi mahakamani ila wezi wadogo tu ndio wanaoadhibiwa. Kwa upande mwingine, anaonekana kufurahia jinsi baadhi ya taasisi za serikali zinazohusiana na upelelezi zinavyofanya kazi anapouliza swali balagha; *Si mnaona mambo yameanza kujitokeza?* Swali hili pia linachochea wananchi kuamini kuwa serikali inafanya kazi yake barabara katika vita dhidi ya ufisadi. Aidha, katika swali hili, *Chukua msalaba yako wako peke yako! Au namna gani wenzangu?* alilenga kuwashawishi wananchi kusadiki kuwa wezi hawastahili kuhurumiwa wanapokabiliana na mkono wa sheria. Wanastahili kupokea adhabu yao peke yao bila kuwahusisha wengine ambao hawakushirikiana nao katika wizi.

Maswali haya ya balagha yalitumiwa na wanasiasa hawa katika hotuba zao kwa dhima kuu ya kuchochea hisia za wasikilizaji kuhusu suala la ufisadi kama anavyoeleza Wamitila (2008) kuwa, maswali balagha huchochea fikra au hisia za wasikilizaji kuhusu suala husika. Walilenga kuwachochea wawazie kwa kina hali inayowawakabili ili waone nia ya kuwaunga wao mkono katika juhudi zao za kukabiliana na hali hii na kwa kufanya hivyo wanadhibiti mamlaka waliyo nayo kama anavyodai Van Dijk (1998). Ulinganisho zaidi wa jinsi suala la ufisadi limeshughulikiwa katika matini za hotuba za kisiasa uliweza kuangaziwa katika matumizi ya virai shawishi katika sehemu ifuatayo.

### 3.12 Matumizi ya Virai Shawishi

Hivi ni virai ambavyo hutumiwa na mhutubu akiwa na lengo la kushawishi hadhira yake kuunga mkono kauli zake. Kwa mujibu wa Holmes (1984), virai hivi ni vya aina mbili: virai shawishi vinavyoashiria ustaha na vile vya kujitendekeza. Virai vinavyoashiria ustaha hutumiwa na mnenaji anayetafuta maoni yake kuitikiwa na hadhira yake na vilevile kupata habari fulani. Kwa upande mwingine, virai shawishi vinavyoashiria kujitendekeza vinamlenga msikilizaji, ambapo mnenaji huvitumia ili kueleza hisia zake kwa msikilizaji na pia kwa kumuunga mkono ili kupunguza ukali katika mazungumzo au kulainisha uneni ulio na ukali. Virai hivi vimetumiwa na wanasiasa hawa katika hotuba teule kama ifuatavyo:

**Jedwali 3.14: Virai Shawishi**

| | Virai Shawishi | Hotuba |
|---|---|---|
| 1. | *Mara ile nyingine niliongea juu ya mambo ya wizi katika idara ya NYS.* ***Si nilisema? Si nilisema?*** | RO2 |
| 2. | ***Si mpaka tu uchunguzi ifanywe?*** | RO3 |
| 3. | *Chukua msalaba yako wako peke yako!* ***Au namna gani wenzangu?*** | UK1 |

Katika Jedwali 3.14, Raila akirejelea sakata ya NYS anasema *Mara ile nyingine niliongea juu ya mambo ya wizi katika idara ya NYS.* ***Si nilisema? Si nilisema?*** Ametumia kirai shawishi *Si nilisema?* kushawishi wasikilizaji wake kuamini anayoyasema kwani ni kana kwamba aliyoyasema hapo awali yamebainika wazi. Aidha, viongozi hawa wote wanatumia virai shawishi kutaka maoni yao kuwa mafisadi lazima waadhibiwe kisheria yaungwe mkono na wasikilizaji wao kama ifuatavyo. Raila anasema, *Si mpaka tu uchunguzi ifanywe?* naye Uhuru anasema, '*Chukua msalaba yako wako peke yako!* ***Au namna gani wenzangu?*** Kando na kuwataka wananchi kuunga mkono mtazamo wao,

viongozi hawa hasa Uhuru anatumia kirai hiki shawishi kulainisha uneni wake ambao unaonekana kuwa wenye ukali wa maneno kwa washukiwa wa ufisadi kama anavyoeleza Holmes (1984). Aidha, wanalenga kuwajumuisha wanaohutubiwa katika hotuba zao kama mojawapo ya mbinu za kuhutubu anazoeleza Van Leeuwen (2008). Kando na hayo, wanalenga kushawishi umma kuhusu sera zao na pia kujipa mamlaka kama inavyoelezwa na Klebanov na wengine (2008) na Niedrich (2011) kuwa hotuba ya kisiasa kimsingi hutumiwa kuwashawishi watu, kuwabembeleza, kuwafurahisha na kujipa mamlaka. Ulinganishaji wa mbinu mbalimbali ambazo zilitumiwa katika matini ya hotuba teule za kisiasa kuangazia suala la ufisadi, umedhihirisha jinsi uwezo na mamlaka ya wanasiasa yanavyojengwa kwa kutumia lugha kiufundi kushawishi umma.

## 3.3 Hitimisho

Katika sura hii, matini za hotuba teule za kisiasa kuhusu ufisadi zimechanganuliwa na kulinganishwa kwa mujibu wa nadharia ya UUH. Data ya hotuba za kisiasa ilipakuliwa mtandaoni, ikasimbwa ili kurejelewa kwa wepesi kisha ikapangwa kwenye makundi kwa kutumia majedwali kabla ya kuichanganua na kuilinganisha kwa kutumia maelezo.

Data ilipangwa katika makundi mbalimbali kwenye majedwali kwa kuzingatia muundo na sifa zake za kiisimu na kisha kuchanganuliwa na kulinganishwa kwa kielelezo cha nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (UUH). Kwa jumla, houba 6 za wanasiasa wawili teule zimehakikiwa. Hotuba hizi ni zile zinazoangazia suala la ufisadi katika sakata za NYS na mabwawa ya Arror na Kimwarer. Mtafiti alianza kwa kutambua na kuainisha sifa mbalimbali za matini katika hotuba teule kama hatua ya kwanza ya uhakiki wa matini kwa

mujibu wa Fairclough (1995). Baadaye akazichanganua na kuzilinganisha kwa mwongozo wa nadharia ya UUH.

Vipengele vitatu vya uhakiki wa matini kwa mujibu wa Fairclough (keshatajwa) vilizingatiwa katika uchanganuzi wa data. Kipengele cha kwanza ni matini yanayohakikiwa ambapo katika utafiti huu, video na sauti za hotuba teule za kisiasa kuhusu ufisadi zilipakuliwa kwenye mtandao wa Youtube, zikasikilizwa na kutazamwa kisha baadaye kuandikwa. Kipengele cha pili ni jinsi matini yalivyozalishwa ambapo tulihakiki namna maneno, virai, sentensi na sifa nyingine za kiisimu zilizotumiwa katika hotuba teule. Hapa, tulitumia majedwali kupanga na kulinganisha vipengele mbalimbali vya kiisimu katika matini ya hotuba teule. Kwa kuzingatia kipengele cha tatu ambacho ni uhakiki wa hali za kijamii na kihistoria zinazoongoza michakato hii, mtafiti ameeleza na kulinganisha sifa za kiisimu katika matini husika kwa kuzingatia miktadha au masuala ya kihistoria yaliyochochea kauli zilizotolewa na wanasiasa husika.

Imebainika kuwa matini za hotuba teule za kisiasa kuhusu ufisadi husheheni mbinu kadhaa za kimtindo kama alivyodai Ngure (2020) kuwa, hotuba za kisiasa zina ukwasi wa tamathali za usemi. Baadhi ya mbinu zilizobainika katika utafiti huu ni; matumizi ya istilahi maalum, matumizi ya viwakilishi vya nafsi, kuwasawiri wananchi kama wenye mamlaka makuu, matumizi ya toni ya kejeli, lugha yenye takwimu, lugha yenye matumaini, toni ya kukashifu, kuchanganya msimbo, matumizi ya kinaya, matumizi ya takriri, matumizi ya maswali balagha na matumizi ya virai shawishi.

Baada ya kuchanganua na kulinganisha, mtafiti alibaini kuwa viongozi hawa wote walitumia mbinu hizi katika hotuba zao walipokuwa wakiangazia suala la ufisadi nchini Kenya. Dhima ya kutumia mbinu hizi zote ilibainika kuwa ni kuusawiri ufisadi kama uozo katika jamii, kukemea mafisadi, kukemea utepetevu katika taasisi zinazohusiana na vita dhidi ya ufisadi na pia kuwashawishi wananchi kuunga mkono hatua wanazopendekeza kuchukuliwa katika vita dhidi ya ufisadi. Kwa kufanya hivyo, wanaafikiana na mtazamo wa Crystal (1997) kuwa usemi huweza kuathiri matukio katika jamii. Isitoshe, dhima yao ya kupambana na ufisadi nchini inawiana na madai ya Van Dijk (1998) kuwa wenye mamlaka katika jamii huwa na uwezo wa kuamulia jamii na kuishawishi dhidi ya kile wanachokiona kuwa kinyume na maadili ya jamii.

Aidha, kama wanavyodai Seidel (1985) na Van Dijk (1997) kuwa katika uchanganuzi wa matini ya hotuba za kisiasa ni lazima mtafiti ahakiki wanasiasa husika, matini za hotuba zenyewe na wapokezi wa hotuba; katika sura ya nne mtafiti atahakiki wapokezi wa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi (wananchi) kwa kuchanganua athari na mielekeo yao kuhusu hotuba hizi.

# SURA YA NNE

# ATHARI NA MIELEKEO YA WANANCHI KUHUSU HOTUBA ZA KISIASA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu, kwa mwongozo wa nadharia ya UUH, mtafiti alilinganisha hotuba za wanasiasa wawili kuhusu ufisadi kwa kuhakiki sifa za lugha iliyotumiwa katika hotuba teule. Ilibainika kuwa wanasiasa hutumia mitindo mbalimbali katika hotuba zao ili kukemea, kujisifia, kuzindua na kushawishi umma kuunga mkono juhudi zao za kupambana na ufisadi nchini Kenya. Mbinu walizotumia ni; matumizi ya istilahi maalum, matumizi ya viwakilishi vya nafsi, kuwasawiri wananchi kama wenye mamlaka makuu, matumizi ya toni ya kejeli, lugha yenye takwimu, lugha yenye matumaini, toni ya kukashifu, kuchanganya msimbo, matumizi ya kinaya, matumizi ya takriri, matumizi ya maswali balagha na matumizi ya virai shawishi. Katika sura hii, athari na mielekeo ya hotuba za kisiasa miongoni mwa wananchi wa Kenya imechanganuliwa na kulinganishwa. Athari zimechanganuliwa kwanza.

## 4.1 Athari za Hotuba za Kisiasa kwa Wananchi wa Kenya

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 2.4, hotuba inapotolewa huibua athari mbalimbali kwa hadhira lengwa ambazo huenda zikawiana na dhamira ya mhutubu au zikakosa kuwiana ((Brown na Yule, 1993; Crystal, 1997). Aidha, Wanjugu (2010) anadai kuwa kila

tendo huwa na ama athari hasi au chanya ambazo hufuata baada ya kitendo kutendeka. Haji (2018) akikubaliana na madai ya wataalamu hawa, alibainisha athari mbalimbali za hotuba za kisiasa kwa hadhira kama vile; kushawishika, kuhamasika, kupuuza, kufarijika, kukasirika na kuudhika, kujenga matumaini, kuzinduka, kuungama, kumakinika, kufurahika na kujiamini. Kwa kuzingatia misingi hii iliyowekwa na wataalamu hawa, mtafiti alichanganua maoni ya watafitiwa kuhusu hotuba za kisiasa zilizolenga suala la ufisadi kwa kielelezo cha nadharia ya UUH na kubainisha athari mbalimbali za hotuba hizi kwa wananchi. Athari hizi zimejadiliwa katika makundi matatu: athari kwa wafisadi; athari kwawenye nia ya kushiriki ufisadi na athari kwa wananchi wanaopiga vita ufisadi. Athari kwa wafisadi zimejadiliwa kwanza.

### 4.1.1 Athari kwa Wafisadi

Mtafiti kupitia hojaji, aliwauliza watafitiwa kutoa maoni kuhusu namna hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi zinavyoathiri wafisadi katika jamii. Maoni yao yalijikita katika vitengo vitatu kama ilivyowasilishwa na kulinganishwa katika jedwali 4.1 lifuatalo.


**Jedwali 4.1 Athari za Hotuba kwa Wafisadi**

| **Athari** | **Idadi** |
|---|---|
| Huwachochea kuendelea na ufisadi | 10 |
| Hazina athari yoyote kwao | 19 |
| Huwafanya mafisadi kuogopa | 47 |
| **Jumla** | 76 |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.1, wahojiwa 47 walidai kuwa hotuba za wanasiasa kuhusu suala la ufisadi huwafanya mafisadi kuogopa kuendelea na ufisadi. Wahojiwa 10 walihisi kuwa hotuba hizi huwafanya mafisadi kuendelea na ufisadi zaidi badala ya kuzuia. Wahojiwa 19

nao walishikilia msimamo kuwa hotuba hizi hazina athari zozote kwa mafisadi. Pai chati ifuatayo inawasilisha maoni haya ya wananchi kiasilimia.

**Pai chati 4.1 Athari za Hotuba kwa Wafisadi**




Kwa mujibu wa pai- chati 4.1, asilimia 13.2 wanaamini kuwa hotuba hizi huwachochea kuendelea na ufisadi; asilimia 25 wakidai kuwa hazina athari yoyote huku kubwa zaidi ya 61.8% ya Wakenya wakiamini kuwa mafisadi huogopa kauli za wanasiasa kuhusu ufisadi katika hotuba zao hasa wanapotumia lugha kali. Kutokana na data hii na maelezo waliotoa watafitiwa, athari mbalimbali zilibainishwa. Athari hizi zimefafanuliwa katika aya zifuatazo kuanzia zile zinazoathiri wananchi wachache na kuhitimisha na zile zinazowaathiri wananchi wengi. Ya kwanza ni kuwa, hotuba hizi huchochea ufisadi kuendelea.

Kama ilivyobainika katika jedwali 4.1 na pai chati 4.1, wahojiwa 10 (13.2%) walidai kuwa hotuba hizi huwachochea wafisadi kuendelea na ufisadi hata zaidi. Kulingana na maoni

yao, wanasiasa wamekuwa na mazoea ya kutumia vitisho japo hakuna wanalofanya hivyo basi wanapokemea mafisadi, wao hujua kuwa njia walizokuwa wakitumia zimejulikana na hivyo wanastahili kubuni nyingine ili kuendelea kuiba zaidi. Aidha, walidai kuwa wanapotajwa, wao hutumia milungula kunyamazisha wanasiasa wanaoangazia matendo yao na kwa kufanya hivyo visa vya ufisadi vinazidi kushuhudiwa. Hii ina maana kuwa hotuba hizi huibua athari ya kuchochea ufisadi kuendelea ambayo ni athari chanya kwa wafisadi. Athari ya pili ni hotuba kuwafanya wananchi kuwa na mapuuza.

Imebainika kuwa, wahojiwa 19 (25%) kwa mujibu wa Jedwali 4.1 na pai chati 4.1 wanaamini kuwa hotuba hizi haziathiri kwa vyovyote vile mapambano dhidi ya ufisadi. Watafitiwa walidai kuwa wamezoea hali ya wanasiasa kuangazia suala hili ila hawachukui hatua yoyote. Wengine walieleza kuwa wengi wanaoshiriki katika matendo ya ufisadi huwa na viongozi wa kuwatetea wanaposhambuliwa kwa sababu ya kushiriki katika ufisadi. Maoni haya yanabainsha kuwa hotuba hizi zimewafanya baadhi ya wananchi wanaoshiriki ufisadi kuwa na mapuuza.Licha ya baadhi ya wafisadi kuwa na mapuuza, asilimia kubwa hutishika na kuogopeshwa na hotuba hizi.

Kwa mujibu wa jedwali 4.1 na pai chati 4.1, ilibainika kuwa wahojiwa 47 (61.8 %) walikiri kuwa hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi huwaogofya wafisadi. Hii ina maana kuwa wananchi wengi wanaamini kuwa wafisadi hutishika wanaposikia matendo yao ya ufisadi yakiangaziwa kwenye hotuba hizi. Wengi wao walieleza kuwa lugha kali inayotumiwa na wanasiasa huwatishia sana mafisadi kiasi cha kuwafanya kupunguza matendo ya ufisadi kwa kiwango fulani. Aidha, wengine walidai kuwa kauli za wanasiasa huwafanya mafisadi

kushawishika kuwa matendo yao yamegunduliwa na watakabiliwa na mkono wa sheria. Kutokana na maoni haya, ilibainika kuwa asilimia kubwa ya wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi huathiri wafisadi kwa namna mbili; ya kwanza ni kuwa, huwafanya wafisadi kutishika kutokana na lugha kali inayotumiwa na ya pili ni kuogopa kuwa maovu yao yamegunduliwa hivyo basi wataadhibiwa. Hili ni thibitisho la madai ya Van Dijk (1998) kuwa watu wenye mamlaka katika jamii huwa na uwezo wa kuamulia jamii na kuishawishi dhidi ya kile wanachokiona kuwa ni kinyume na maadili ya jamii. Kando na athari za hotuba hizi kwa wafisadi, sehemu ifuatayo inashughulikia athari zake kwa wananchi wenye nia ya kushiriki matendo ya ufisadi.

### 4.1.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi


Watafitiwa walipoulizwa iwapo hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi zingeweza kuwafanya kubadili nia yao ya kushiriki katika matendo ya ufisadi, walitoa maoni mbalimbali kama yalivyowasilishwa katika jedwali na pai chati ifuatayo.

**Jedwali 4.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi**

| **Kauli** | **Ndio** | **La** |
|---|---|---|
| | Idadi | Idadi |
| Hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi zinaweza kukufanya ubadili nia ya kushiriki ufisadi? | 41 | 35 |

Kutokana na Jedwali 4.2, wahojiwa 41 walikiri kuwa hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi zingewafanya kubadili nia ya kushiriki ufisadi huku 35 wakikana hali hii. Hii ina maana kuwa hotuba hizi zina uwezo wa kuwashawishi kuacha uovu huu. Pai-chati ifuatayo inawasilisha ujumbe huu kiasilimia.

**Pai-chati 4.2 Athari kwa Wenye Nia ya Kushiriki Ufisadi**




Pai-chati 4.2 inaonyesha kuwa, 53.9% ya wahojiwa wanaamini hotuba hizi zina uwezo wa kubadili maamuzi ya wale ambao walikuwa na nia ya kushiriki ufisadi. Kwa upande mwingine, asilimia 46.1 walikiri kutoathiriwa na hotuba hizi. Asilimia hizi hazitofautiani pakubwa. Kando na watafitiwa kukiri au kukataa kubadili nia ya kushiriki ufisadi kutokana na hotuba hizi, walieleza sababu zao. Baadhi ya sababu hizi zimewasilishwa kwenye majedwali yafuatayo. Sababu za kubadili nia ya kushiriki ufisadi na athari zake zimewasilishwa kwanza.

**Jedwali 4.3 Sababu za Kubadili Nia**

| | **Baadhi ya maoni ya watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Kwa mujibu wa hotuba hizi adhabu ni kali sana kwa mafisadi hivyo naogopa kujipata katika hali hii.* |
| ii) | *Madhara yanayoangaziwa ni mengi kwangu na kwa taifa nzima.* |
| iii) | *Naogopa mkono wa sheria kwa maana wanasiasa wana mamlaka.* |

Kutokana na data kwenye majedwali 4.2, 4.3 na pai chati 4.2, imebainika kwamba asilimia kubwa (53.9) ya wananchi wanaogopa kauli za wanasiasa kuhusu ufisadi hasa wanapoangazia adhabu kali kwa mafisadi na madhara ya ufisadi kwa nchi nzima. Kutokana na maoni haya ya watafitiwa, imebainika kuwa Wakenya wengi huhamasika, hushawishika

na huogopeshwa na hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi.  Kwa misingi hii basi, wanaafikiana na mtazamo wa Van Dijk (1998) kuwa watu wenye mamlaka wana uwezo wa kushawishi jamii dhidi ya kile wanachoamini ni kinyume cha maadili ya kijamii.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wahojiwa (46.1%) walieleza kuwa hotuba hizi haziwezi kuwazuia kushiriki matendo ya ufisadi. Baadhi ya maoni yao yamewasilishwa kwenye jedwali lifuatalo na kisha athari zake kubainishwa na kufafanuliwa.

**Jedwali 4.4 Sababu za Kutobadili Nia**

| | **Baadhi ya maoni ya watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Hotuba hizi huniogopesha kiasi tu lakini siwezi kuacha* |
| ii) | *Wanaoshiriki ufisadi hutajirika haraka ikilinganishwa na wasioshiriki katika matendo ya ufisadi. Mimi pia nataka kutajirika haraka* |
| iii) | *Wanasiasa wenyewe ndio wamezidi katika ufisadi kwa hivyo ni muhali zaidi kunizuia mimi kushiriki katika ufisadi pia.* |
| iv) | *Bora ufanye urafiki na wanasiasa utaiba tu bila wasiwasi.* |
| v) | *Mafisadi hukemewa tu iwapo ni wa mrengo pinzani hivyo bora niwe upande wa serikali siwezi kuogopa.* |

Kutokana na maoni haya kwenye Jedwali 4.4, ilibainika kuwa sababu kuu ya baadhi ya wananchi wa Kenya (46.1%) kukosa imani katika uwezo wa hotuba za wanasiasa kuzuia watu kushiriki ufisadi ni kuwa, wanasiasa hukemea ufisadi tu miongoni mwa wapinzani wao kisiasa. Hii ina maana kuwa semi zao huathiriwa na mahusiano yao katika jamii na hivyo kuafikiana na mhimili wa 5 ambapo Fairclough (1995) anadai kuwa usemi huweza kuathiriwa kijamii na kisiasa.Aidha maoni ya wananchi hawa yamebainisha kuwa hotuba hizi zimejenga hali ya mapuuza katika baadhi ya wananchi kwani hawana imani na yale yanayosemwa na wanasiasa katika hotuba hizo. Kando na athari za hotuba hizi kwa

wananchi wenye nia ya kushiriki ufisadi, mtafiti pia alihakiki athari kwa wananchi wanaopiga vita ufisadi ambazo zimewasilishwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.1.3 Athari kwa Wananchi Wanaopiga Vita Ufisadi

Kwa kuzingatia kigezo hiki,mtafiti aliandaa maswali matatuambayo yalitumiwa kubainisha jinsi hotuba hizi zinavyoathiri wananchi. Swali la kwanza lilihusu kuendelea au kutoendelea kutumiwa kwa hotuba hizikatika kuangazia suala la ufisadi; la pili likawataka kutoa maoni kuhusu hali ya wanasiasa kuamua kutoangazia ufisadi kabisa katika hotuba zao na la mwisho liliwataka kueleza kinachowafurahisha au kuwachukiza katika hotuba hizi. Athari kutokana na swali lililohusu kuendelea au kutoendelea kuangazia ufisadi katika hotuba hizi zimeshughulikiwa kwanza.


Mtafiti aliwauliza watafitiwa iwapo wangependa wanasiasa waendelee kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao kwa umma kama mkakati wa kupiga vita ufisadi au la. Matokeo yake yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.5 Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi**

| **Swali** | **Ndio** | **La** |
|---|---|---|
| | **Idadi** | **Idadi** |
| Ni muhimu kwa wanasiasa kuendelea kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao? | 52 | 24 |

Kutokana na data katika Jedwali 4.5, wahojiwa 52 walihisi kuwa hotuba hizi ziendelee kutumiwa katika juhudi za kupambana na ufisadi huku 24 wakishikilia kuwa si muhimu kwao kuendelea kuzitumia kuangazia suala hili. Matokeo hayayamewasilishwa kiasilimia katika pai chati ifuatayo.

**Pai-chati 4.3 Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi**




Kwa mujibu wa pai-chati 4.3, 68.4% ya wahojiwa waliwataka wanasiasa waendelee kutumia hotuba hizi huku 31.6% wakipinga Matokeo haya pamoja na sababu zake yaliweza kutumiwa kubainisha athari mbambali za hotuba hizi kwa wananchi wa Kenya. Athari kutokana na maoni ya wanaoshikilia kuwa hotuba hizi ziendelee kuangazia ufisadi zimejadiliwa kwanza. Baadhi ya sababu walizotoa zimewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.6 Sababu za Hotuba Kuendelea Kuangazia Ufisadi**

| | **Baadhi ya maoni ya watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Hotuba hizo huhamasisha wananchi kuhusu madhara ya ufisadi.* |
| ii) | *Nyingi ya hotuba hizi ndizo hupuliza firimbi kuwa wizi umetendeka na hivyo husaidia taasisi husika kuanzisha uchunguzi.* |
| iii) | *Zinawafanya kuelewa kuwa ufisadi una athari mbaya kwa uchumi na maendeleo ya nchi.* |
| iv) | *Huwafanya mafisadi kuogopa kiasi na hivyo husaidia katika vita dhidi ya ufisadi. Kuna wale waliobadilika kutokana nazo.* |
| v) | *Wanasiasa wakiendelea kukemea ufisadi utaisha au kupunguka.* |
| vi) | *Wanapoangazia suala hili, wananchi huamini kuwa viongozi hawaungi mkono ufisadi.* |

Kutokana na maoni ya watafitiwa katika jedwali 4.6, wengi wa watafitiwa walisisitiza kuwa kando na hotuba hizi kusaidia kupunguza visa vya ufisadi, zinatumiwa kuwazindua na kuwahamasisha wananchi kuwa ufisadi umetokea. Aidha, madhara yake hubainishwa

kupitia kwazo. Kwa sababu hizi, wangependa ziendelee kutumika. Hii ina maana kuwa, hotuba hizi huibua athari mbili kwa wananchi; kuwahamasisha na kuwazindua. Matokeo haya yanawiana na madai ya Van Dijk (1998) kuwa watu wenye mamlaka katika jamii huwa na uwezo wa kuamulia jamii na kuishawishi dhidi ya kile wanachokiona kuwa ni kinyume na maadili ya jamii. Kwa upande mwingine, baadhi ya sababu za waliopinga suala la hotuba hizi kuangazia ufisadi zimewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.7 Sababu za Kupinga Hotuba Zisiangazie Ufisadi**

| | **Baadhi ya Sababu za Watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Wanasiasa ni mafisadi kwa hivyo wao kuangazia suala hili ni unafiki mkubwa.* |
| ii) | *Baadhi ya watu fisadi wameteuliwa na hao hao wanasiasa katika nyadhifa mbalimbali hivyo basi kuangazia suala hili katika hotuba zao hakuna umuhimu wowote.* |
| iii) | *Kuangazia kwao huwafanya mafisadi kuficha ushahidi. Kwa sababu hii, ni vyema wao kutoangazia.* |
| iv) | *Wao hutoa maneno matupu bila vitendo na hivyo haisaidii katika vita dhidi ya ufisadi.* |
| v) | *Kuna taasisi zinazohusika na vita dhidi ya ufisadi ambazo zinastahili kupewa nafasi ya kutekeleza jukumu lao.* |

Wengi wa waliopinga matumizi ya hotuba hizi kwa mujibu wa Jedwali 4.7, walieleza kuwa walizichukulia kama gumzo tupu kwa sababu waliamini kuwa wanasiasa pia ni fisadi. Kwa sababu hii, ilibainika kuwa hotuba hizi huchimuza hali ya mapuuza miongoni mwa wananchi wanaoshikilia mtazamo huu. Swali la pili ambalo liliwataka wahojiwa kutoa maoni kuhusu hali ya wanasiasa kuacha kuangazia ufisadi katika hotuba zao, limeshughulikiwa pia.

Katika juhudi za kubainisha athari zaidi za hotuba za kisiasa kwa wananchi wanaopiga vita ufisadi, mtafiti aliwahoji watafitiwa kuhusu namna ambavyo wangehisi iwapo wanasiasa

wangeamua kutoangazia suala la ufisadi katika hotuba zao. Maoni mseto yaliweza kutolewa. Kuna wale walioeleza kutoridhika kwao na hali hiyo na wale walioonyesha kufurahishwa na hali hiyo. Jedwali lifuatalo linalinganisha idadi na asilimia za watafitiwa katika vitengo hivi viwili:

**Jedwali 4.8 Hali ya Wanasiasa Kutoangazia Ufisadi**

| **Ambao Hawataridhika** Idadi | Asilimia (%) | **Ambao Wataridhika** Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 48 | 63 | 28 | 37 |
| Jumla 76 | | | |

Kulingana na data katika jedwali 4.8, watafitiwa 48 ambao ni 63% walieleza kutoridhika kwao na hatua hiyo huku 28 (37%) wakieleza kuridhika kwao. Athari kutokana na wasioridhika na hali hii zimeshughulikiwa kwanza. Jedwali lifuatalo linawasilisha baadhi ya sababu wahojiwa walitoa kutetea mtazamo huu:

**Jedwali 4.9 Sababu za Kutoridhika**

| | **Baadhi ya Sababu za Watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Hali hiyo itadhihirisha kutowajibika kwa viongozi kwani ni jukumu lao kukemea maovu katika jamii ili kuwe na jamii yenye maadili. Hii itamaanisha kuwa wameamua kuachana na vita dhidi ya ufisadi.* |
| ii) | *Itakuwa bayana kuwa wanasiasa wameamua kuungana na mafisadi kuiba mali ya umma.* |
| iii) | *Itaonyesha hali ya wao kuridhika na hali ya wizi wa mali ya umma na kutojali athari za ufisadi kwa taifa lao.* |
| iv) | *Utakuwa ni usaliti mkubwa kwani bila wao kukemea hali hizi, ufisadi utaongezeka sana.* |

Kutokana na maoni ya watafitiwa hawa kwenye Jedwali 4.9, ilibainika kwamba Wakenya wengi hushawishika na kufarijika kuwa vita dhidi ya ufisadi viko imara wakati wanasiasa wanaangazia ufisadi katika hotuba zao.Hii ina maana kuwa hotuba hizi hushawishi na kufariji Wakenya wengi (63%). Isitoshe, wanaamini kuwa ni jukumu la wanasiasa kukemea suala la ufisadi nchini sawa na maovu mengine katika jamii. Maoni haya yanawiana na mhimili wa 3 ambao unaeleza kuwa hadhira hukubali imani (maarifa na maoni) kupitia matini yanayoaminiwa yanatoka kwa watu walio na mamlaka. Isitoshe, hali hii inalingana na ya wananchi wa Uchina kwa mujibu wa DW Idhaa ya Kiswahili (2013) ambapo wananchi walifurahi sana wakati rais wao Xi Jinping alitoa ahadi ya kupambana na ufisadi katika hotuba yake ya kwanza kwa taifa baada ya kuchukua mamlaka. Kwa upande mwingine, baadhi ya sababu za wale ambao walikiri kuridhika na hali ya wanasiasa kutoangazia ufisadi kwenye hotuba zao zimewasilishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.10 Sababu za Kuridhika**

| | **Baadhi ya Maoni ya Watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Kauli zao hazina matendo.* |
| ii) | *Kuangazia kwao ni kinaya tu.* |
| iii) | Heri waache, hotuba zao zinaongeza ufisadi nchini. |
| iv) | *Hali hii ingesaidia taasisi zinazohusika kufanya uchunguzi kisiri na hivyo kufaulu kuwanasa mafisadi.* |
| v) | Hali hii italeta utulivu kwani itaaminika kuwa ufisadi hautendeki nchini. |

Kutokana na maoni ya watafitiwa kwenye majedwali 4.8 na 4.10 hapo juu, ilibainika kuwa asilimia 37 ya Wakenya wangependa wanasiasa waache kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao. Baadhi ya sababu kuu zilizotajwa ni kuwa, iwapo wataacha kuangazia, kutakuwa na utulivu kwani hotuba zao ni gumzo tupu lisilo na matendo na pia ingeaminika kuwa ufisadi hauendelei nchini. Hii ina maana kuwa hotuba hizi huwatia watu kiherehere hivyo kufanya nchi kukosa utulivu. Madai haya ya kuamini kuwa ufisadi hauendelei wakati

wanasiasa hawaangazii katika hotuba zao, yanawiana na mhimili wa 4 ambapo Van Dijk (1998) anadai kuwa imani yetu kuhusu ulimwengu hutokana na hotuba tunazosikiliza. Swali la mwisho ambalo liliwataka watafitiwa kueleza kile kinachowafurahisha au kuwachukiza katika hotuba hizi liliweza kuibua yafuatayo.

**Jedwali 4.11Ulinganisho wa Mitazamo kuhusu Hotuba za Kisiasa**

| Wanaofurahishwa | | Wanaochukizwa | |
|---|---|---|---|
| **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| 52 | 68 | 24 | 32 |

Kutokana na uchanganuzi wa data katika Jedwali 4.11, ilibainika kuwa wahojiwa ambao walipendezwa na hotuba ni 52 (68% ) huku waliochukizwa wakiwa 24 ( 32%). Kutokana na data hii pamoja na maoni ya wahojiwa kuhusu sababu za kufurahishwa au kuchukizwa na hotuba hizi, athari mbalimbali za hotuba hizi zilibainishwa. Athari za hotuba hizi kwa wale ambao wanazifurahia zilibainishwa kwanza baada ya kuhakiki maoni yao kuhusu kinachowafurahisha kwenye hotuba hizo. Baadhi ya sababu hizo zimewasilishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.12 Sababu za Kufurahishwa na Hotuba za Kisiasa**

| | **Maoni ya Wahojiwa** |
|---|---|
| i) | *Lugha kali dhidi ya mafisadi na vitendo vya ufisadi.* |
| ii) | *Ukakamavu wao katika juhudi za kukabiliana na ufisadi.* |
| iii) | *Kufichuana miongoni mwa wanasiasa fisadi.* |
| iv) | *Kutaja kwa majina ya wale waliohusika na ufisadi bila uoga.* |
| v) | *Ueledi wao wa uteuzi wa maneno katika kukemea mafisadi na kusawiri hali ya ufisadi nchini.* |
| vi) | *Wanavyoshawishi umma kuamini kuwa wao wana uwezo wa kupambana na ufisadi.* |

Kutokana na uchanganuzi wa maoni ya wahojiwa katika Jedwali 4.12, imebainika kuwa kando na hotuba hizi kuwafurahisha kutokana na uteuzi mzuri wa istilahi, pia huwapa matumaini kuwa wafisadi watakabiliwa barabara na hivyo hali itabadilika. Hii pia ina maana kuwa, wao hufarijika wanaposikiliza hotuba hizi kwa kuwa wanahisi tatizo la ufisadi linashughulikiwa. Aidha, hali hii huwapa wananchi matumaini kuwa mali yao haitazidi kufujwa na wafisadi. Kando na athari hizi kwa wanaozipenda hotuba hizi, maoni ya wasiozipenda kwenye jedwali lifuatalo yalitumiwa kubainisha athari ya hotuba hizi kwao.

**Jedwali 4.13 Sababu za Kuchukizwa na Hotuba za Kisiasa**

| | **Baadhi ya Maoni ya watafitiwa** |
|---|---|
| i) | *Wanasiasa huwakashifu tu wapinzani wao kisiasa lakini walio nao kwenye mrengo mmoja wa kisiasa hawakashifiwi.* |
| ii) | *Hali ya kutochukuliwa hatua kwa wale wanaotajwa kuwa mafisadi katika hotuba hizi. Hili linafanya hotuba hizi kukosa maana.* |
| iii) | *Wanasiasa wanadai kupigana na ufisadi lakini wao ndio wanakabiliwa na kesi nyingi za ufisadi dhidi yao.* |
| iv) | *Hali ya wao kutetea mafisadi wa kabila lao au mirengo yao ya kisiasa.* |

Kutokana na maoni ya watafitiwa katika Jedwali 4.13, imebainika kuwa baadhi ya wananchi huudhika wasikizapo hotuba hizi kwa sababu wanasiasa hutenda kinyume na matarajio ya jamii. Isitoshe, wanadai kuwa wanasiasa ni fisadi zaidi hivyo hawana uwezo

wa kukemea maovu ambayo wanayashiriki. Isitoshe, wao huegemea mirengo ya kisiasa na kikabila ambapo huwatetea wandani wao na kukashifu wapinzani wao. Mtazamo huu wa baadhi ya wananchi unadhihirisha madai kuwa semi huathiriwa kisiasa na kijamii kama anavyodai Fairclough (1995).

Uchanganuzi na ulinganishi wa data katika sehemu hii uliongozwa na mihimili mitatu ya nadharia ya UUH. Mihimili hii kwa mujibu wa sura ya 1.7 ni; mhimili wa 3 unaosema,*'Hadhira hukubali imani (maarifa na maoni) kupitia matini yanayoaminiwa yanatoka kwa watu walio na mamlaka, wanaoaminika au kutoka kwa vyanzo vingine vinavyoaminika kama vile wasomi, wataalamu au vyanzo vinginevyo,'* mhimili wa 4 unaodai, '*Imani yetu kuhusu dunia inatokana na hotuba tunazozisikia*' na wa mwisho ni mhimili wa 5 unaosisitiza kuwa '*Usemi ni tukio la kijamii. Aidha, athari za kijamii, kisiasa na miktadha ya kitamaduni kwa usemi huhakikiwa*.' Kama anavyodai Lasswell (1948) kuwa ni lazima athari za matini kwa hadhira zihakikiwe katika uchanganuzi wa matini ya hotuba, tulihakiki maoni ya wananchi na kubainisha athari mbalimbali. Isitoshe, baadhi ya athari ambazo utafiti huu umeweza kubainisha zinalingana na zile alizobainisha Haji (2018) ambazo mtafiti amezirejelea katika sehemu ya 2.4.

Baadhi ya athari hizi zilibainika kuwa chanya ilhali nyingine nihasi kama wanavyodai Brown na Yule (1993). Athari chanya kadhaa zilibainika: ya kwanza ni kushawishika kwa wananchi kuwa ufisadi unakabiliwa; kuhamasika na kuzinduka kwa kutambulisha hali ya ufisadi inayoendelea na athari zake kwa nchi ili kuwakanya watu wasishiriki;kufarijika na kuwapa matumaini kuwa ufisadi utaisha na mwisho ni kufurahishakutokana na jinsi

wanavyokemea wafisadi na kuwatia uoga. Kwa upande mwingine, athari hasi zifuatazo zilibainika: kwanza ni kutisha na kuogofya wananchi fisadi kutokana na lugha kali; kuudhika kwa wananchi kutokana na hali ya wanasiasa kukemea ufisadi ilhali wao pia wanashiriki au wanatetea wandani wao; kuchochea ufisadi zaidi ambapo wafisadi hutafuta mbinu mpya za wizi; kusababisha kiherehere miongoni mwa wananchi kwa kuwafanya kuhisi wapo taabani kutokana na ufisadina mwisho ni hali ya mapuuza ambapo wanasiasa hukemea ufisadi na kuahidi kupigana nao ila hakuna matendo yanayoambatana na ahadi hizi. Mbali na athari zilizoelezwa katika sehemu hii, maoni ya wahojiwa kuhusu hotuba za kisiasa yalitumiwa kubainisha mielekeo yao kuzihusu. Mielekeo hii imechanganuliwa na kuelezwa katika sehemu ifuatayo.

## 4.2 Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa

Dhana ya mielekeo kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya 2.4, ni hali ya mtu kuwa tayari kutenda kitu fulani wala sio kitu kinachoweza kuonekana (Agheyisi na Fishman, 1970; Thomas, 1971). Ili kubainisha mwelekeo wa mtu kuhusu kitu au jambo fulani, wataalamu hawa wanasisitiza matumizi ya mbinu ya kuuliza maswali.Kwa misingi ya maelezo ya wataalamu hawa, mtafiti aliandaa maswali maalum katika hojaji funge ya Likati ili kubainisha mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia ufisadi.Swali la kwanza lilihusu usikilizaji wa hotuba za kisiasa.

### 4.2.1 Mielekeo kuhusu Usikilizaji wa Hotuba za Kisiasa

Katika juhudi za kubainisha mielekeo ya wananchi kuhusu usikilizaji wa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi, mtafiti kupitia hojaji ya Likati aliwauliza watafitiwa kueleza iwapo wao husikiliza hotuba hizo. Jedwali lifuatalo linawasilisha ulinganisho wa mielekeo yao.

**Jedwali 4.14 Mielekeo kuhusu Usikilizaji wa Hotuba za Kisiasa**

| **Jinsia** | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | F | % | | |
| Wanawake | 2 | 5.3 | 5 | 13.2 | - | - | 20 | 52.6 | 11 | 28.9 | 3.86 | Chanya |
| Wanaume | - | - | 1 | 2.6 | - | - | 25 | 65.7 | 12 | 31.6 | 4.26 | Chanya |
| **Jumla** | 2 | | 6 | | | | 45 | | 23 | | 4.06 | **Chanya** |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.14, wahojiwa wa jinsia ya kiume wana alama wastani 4.26 huku wa kike wakiwa na 3.86 na kwa jumla ni 4.06. Hii inadhihirisha kuwa wananchi wa jinsia hizi mbili wana mielekeo chanya kuhusu usikilizaji wa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi. Ilibainika pia kuwa wanaume husikiza sana hotuba hizi kuliko wanawake. Hali hii ya wananchi kuthamini usikilizaji wa hotuba za viongozi wao zinazoangazia suala hili la ufisadi nchini, inaafikiana na mhimili wa pili wa nadharia ya UUH ambapo Van Dijk (1998) anaeleza kuwa watu wenye mamlaka katika jamii huwa na uwezo wa kuamulia jamii na kuishawishi dhidi ya kile wanachokiona kuwa kinyume na maadili ya jamii.. Swali la pili liliangazia umuhimu wa hotuba hizi kuangazia ufisadi kila mara.

### 4.2.2 Mielekeo kuhusu Hali ya Ufisadi Kuangaziwa Kila Mara

Wahojiwa walitakiwa kuelezaiwapo wanaamini kuwa, ni vyema kwa wanasiasa kuangazia suala la ufisadi kila mara katika hotuba zao. Maoni yao yalitumiwa kubainisha mielekeo yao kuhusu suala hili kama ilivyowasilishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.15 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kuangaziwa Kila Mara**

| **Jinsia** | 1<br>F | % | 2<br>F | % | 3<br>F | % | 4<br>F | % | 5<br>F | % | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 4 | 11 | 4 | 11 | 1 | 3 | 10 | 26 | 19 | 50 | 3.95 | Chanya |
| Wanaume | 5 | 13 | 10 | 26 | 2 | 5 | 9 | 24 | 12 | 32 | 3.34 | Wastani |
| **Jumla** | 9 | | 14 | | 3 | | 19 | | 21 | | 3.65 | **Chanya** |

Kutokana na Jedwali 4.15, watafitiwa wa kike wana alama za wastani 3.95 ambazo kwa mujibu wa hojaji ya likati zinaashiria mwelekeo chanya ilhali watafitiwa wa kiume wana alama wastani 3.34 ambazo zinaashiria mwelekeo wa wastani kuhusu suala hili. Ulinganisho wa jinsia zote kwa ujumla, unaonyesha alama 3.65 ambazo zinadhihirisha kuwa Wakenya wana mwelekeo chanya kuhusu hali ya wanasiasa kutumia hotuba zao kila mara kuangazia ufisadi nchini. Hii ina maana kuwa wananchi wameshawishika kuwa viongozi wao wa kisiasa kupitia hotuba hizi wana mchango katika vita dhidi ya ufisadi.

### 4.2.3 Mielekeo kuhusu Ufanisi wa Hotuba za Kisiasa

Kwa lengo la kubaini mielekeo ya wananchi kuhusu ufanisi wa hotuba za kisiasa katika vita dhidi ya ufisadi; mtafiti aliwauliza wahojiwa kueleza iwapo hotuba hizi zinasaidia pakubwa katika vita hivi nchini. Majibu waliyotoa yalitumiwa kubainisha mielekeo yao kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.16 Mielekeo kuhusu Ufanisi wa Hotuba za Kisiasa**

| **Jinsia** | 1<br>F | % | 2<br>F | % | 3<br>F | % | 4<br>F | % | 5<br>F | % | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 7 | 18.4 | 14 | 36.8 | - | - | 12 | 31.6 | 5 | 13.2 | 2.84 | Wastani |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 21 | 55.3 | - | - | 5 | 13.2 | 10 | 26.3 | 2 | 5.2 | 2.26 | Hasi |
| **Jumla** | | | | | | | | | | | 2.55 | **Wastani** |

Kwa kuzingatia matokeo kwenye Jedwali 4.16, wanawake wana alama wastani 2.84 ambazo zinadhihirisha kuwa wana mwelekeo wastani kuhusu suala hili. Kwa upande mwingine, wanaume wana alama wastani 2.26 ambazo zinazowakilisha mtazamo hasi ingawa kwa ujumla watafitiwa wote wana mwelekeo wastani kwa kuwa alama za wastani ni 2.55. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wananchi wa Kenya wana mwelekeo wa wastani kuhusu imani kuwa hotuba za kisiasa zina mchango mkubwa sana katika vita dhidi ya ufisadi nchini. Hii ina maana kuwa wanathamini mchango wake japo si mkubwa sana kama ilivyosawiriwa katika kauli ya mtafiti.

### 4.2.4 Mielekeo kuhusu Athari za Hotuba kwa Wafisadi

Watafitiwa waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu athari ya hotuba za kisiasa kwa wafisadi. Walitakiwa kusema iwapo wanaamini kuwa mafisadi huogopa wanapotajwa au matendo yao yanapotajwa na wanasiasa katika hotuba zao au la. Maoni yao yalitumiwa kupima mielekeo ya wafisadi kuhusu hotuba hizi kama ilivyowasilishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.17 Mielekeo kuhusu Athari za Hotuba kwa Wafisadi**

| **Jinsia** | 1 F | % | 2 F | % | 3 F | % | 4 F | % | 5 F | % | **Alama wastani** | **mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 10 | 26.3 | 11 | 31.25 | 1 | 2.6 | 15 | 39.5 | 1 | 2.6 | 2.53 | Wastani |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 14 | 36.8 | 3 | 7.9 | 4 | 10.5 | 11 | 28.9 | 6 | 15.8 | 2.7 | Wastani |
| **Jumla** | | | | | | | | | | | 2.62 | **Wastani** |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.17, wanawake wana alama wastani za 2.53 ambazo zinaonyesha kuwa mwelekeo wao ni wa wastani. Wanaume nao wana alama wastani 2.7 ambazo pia zinadhihirisha kuwa wana mwelekeo wa wastani kuhusu suala hili. Kwa ujumla, imebainika kuwa wananchi wana mielekeo ya wastani kuhusu imani kuwa hotuba za kisiasa huwaogofya mafisadi. Hii ina maana kuwa idadi ya wanaoshikilia mtazamo huu na idadi ya wanaopinga inaelekea kuwa sawa.

### 4.2.5 Mielekeo kuhusu Namna Ufisadi Unavyoangaziwa

Katika kutathmini mielekeo ya wananchi kuhusu namna viongozi wao wa kisiasa wanaangazia suala la ufisadi katika hotuba zao, mtafiti aliwataka watafitiwa kueleza iwapo wao hufurahia jinsi wanasiasa wanavyoangazia suala hili. Maoni yao yalitumiwa kubainisha mielekeo yao kuhusu suala hili kama ilivyowasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.18 Mielekeo kuhusu namna Ufisadi Unavyoangaziwa**

| **Jinsia** | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | | **Alama wastani** | **mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | F | % | | |
| Wanawake | 3 | 7.9 | 9 | 23.7 | 2 | 5.2 | 12 | 31.6 | 12 | 31.6 | 3.55 | Chanya |
| Wanaume | 9 | 23.7 | 5 | 13.2 | 7 | 18.4 | 10 | 26.3 | 7 | 18.4 | 3.02 | Wastani |
| **Jumla** | 12 | | 14 | | 9 | | 22 | | 19 | | 3.28 | **Wastani** |

Jedwali 4.18 linaonyesha kuwa wanawake wana alama wastani 3.55. Hii inadhihirisha kuwa, wana mwelekeo chanya kuhusu suala hili. Kwa upande mwingine, wanaume nao wana alama wastani 3.02 ambazo zinaonyesha kuwa mwelekeo wao ni wa wastani. Kwa ujumla, wana alama wastani 3.28 ambazo zinabainisha kuwa wananchi wotewana mwelekeo wa wastani kuhusu imani kuwa, wananchi hufurahia jinsi wanasiasa wanavyoangazia ufisadi katika hotuba zao.

### 4.2.6 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kutokemewa Nchini

Watafitiwa walitakiwa kueleza iwapo waliamini kuwa visa vya ufisadi nchini vingeongezeka iwapo wanasiasa wangeacha kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao. Maoni yao yalitumiwa kubainisha mielekeo yao kuhusu suala hili kama ilivyowasilishwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.19 Mielekeo kuhusu Ufisadi Kutokemewa Nchini**

| **Jinsia** | 1 F | % | 2 F | % | 3 F | % | 4 F | % | 5 F | % | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | - | - | 6 | 15.8 | 6 | 15.8 | 12 | 31.6 | 14 | 36.8 | 3.89 | Chanya |
| Wanaume | 3 | 7.9 | 8 | 21.1 | 10 | 26.3 | 7 | 18.4 | 10 | 26.3 | 3.34 | Wastani |
| **Jumla** | 3 | | 14 | | 16 | | 19 | | 24 | | 3.62 | **Chanya** |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.19, wanawake wana alama wastani 3.89 ambazo zinaonyesha kuwa wana mwelekeo chanya kuhusu suala hili. Wanaume nao wana alama wastani 3.34 ambazo zinabainisha kuwa mwelekeo wao ni wa wastani. Kwa ujumla, wana alama wastani 3.62 ambazo zinabainisha kuwa wananchi wa Kenya wana mwelekeo chanya

kuhusu imani kuwa iwapo hotuba za kisiasa zikikoma kuangazia ufisadi, visa hivyo vitaongezeka. Hii ina maana kuwa wanathamini mchango wa viongozi wao katika vita dhidi ya ufisadi kupitia hotuba zao. Kijinsia, inabainika kuwa wanawake wana imani zaidi katika hotuba hizi ikilinganishwa na wanaume.

### 4.2.7 Mielekeo kuhusu Madai Yanayoangaziwa kwenye Hotuba

Watafitiwa walitakiwa kueleza iwapo wanayaamini madai yanayotolewa na wanasiasa kuhusu ufisadi katika hotuba zao. Data iliyotokana na swali hili ilitumiwa kupima mielekeo ya wananchi kuhusu suala hili. Mielekeo hii imewasilishwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali 4.20 Mielekeo kuhusu Madai Yanayoangaziwa kwenye Hotuba**

| **Jinsia** | 1 F | % | 2 F | % | 3 F | % | 4 F | % | 5 F | % | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 9 | 23.7 | 8 | 21.1 | 6 | 15.8 | 14 | 36.8 | 1 | 2.6 | 2.74 | Wastani |
| Wanaume | 15 | 39.5 | 6 | 15.8 | 1 | 2.6 | 12 | 31.6 | 4 | 10.5 | 2.58 | Wastani |
| **Jumla** | 24 | | 14 | | 7 | | 26 | | 5 | | 2.66 | **Wastani** |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.20, wanawake wana alama wastani 2.74 na wanaume 2.58 ambazo zinaonyesha kuwa jinsia zote mbili zina mwelekeo wa wastani kuhusu suala hili. Kwa ujumla,wana alama wastani 2.66 ambazo pia zinawakilisha mwelekeo wa wastani. Hii basi inaonyesha kuwa wananchi huyaamini baadhi ya madai yanayotolewa na wanasiasa katika hotuba zao kuhusu ufisadi lakini mengine hawayaamini.Aidha, kutokana na mwelekeo huu, inaelekea kuaminika kuwa, baadhi ya madai wanasiasa hutoa katika

hotuba hizi ni ya uongo.Kwa ujumla, sehemu ifuatayo imewasilisha muhtasari wa mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi.

### 4.2.8 Muhtasari wa Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa

Baada ya kujadili na kulinganisha kijinsia mielekeo ya wananchi kuhusu masuala mbalimbali, jedwali lifuatalo linawasilisha mielekeo ya wananchi kuhusu suala hili kwa ujumla.

**Jedwali 4.21 Mielekeo ya Wananchi kuhusu Hotuba za Kisiasa**

| **Kauli** | 1 | | 2 | | 3 | | 4 | | 5 | | **Alama wastani** | **Mielekeo** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | F | % | F | % | F | % | F | % | F | % | | |
| Mimi husikiliza sana hotuba za kisiasa kuhusu suala la ufisadi | 2 | 2.6 | 6 | 7.9 | - | - | 45 | 59.2 | 23 | 30.3 | 4.07 | Chanya |
| Hotuba za kisiasa zimesaidia pakubwa katika vita dhidi ya ufisadi | 28 | 36.8 | 14 | 18.4 | 5 | 6.6 | 22 | 28.9 | 7 | 9.2 | 2.55 | Wastani |
| Mafisadi huogopa wanapotajwa katika hotuba za kisiasa | 24 | 31.6 | 14 | 18.4 | 5 | 6.6 | 26 | 34.2 | 7 | 9.2 | 2.71 | Wastani |
| Ni vyema wanasiasa kuangazia ufisadi katika hotuba zao kila mara | 9 | 11.8 | 14 | 18.4 | 3 | 3.9 | 19 | 25 | 31 | 40.8 | 3.64 | Chanya |
| Wanasiasa wakiacha kuangazia suala la ufisadi visa vitaongezeka | 3 | 3.9 | 14 | 18.4 | 16 | 21.1 | 19 | 25 | 24 | 31.6 | 3.62 | Chanya |
| Wananchi hufurahia jinsi wanasiasa huangazia suala la ufisadi katika ,hotuba zao | 12 | 15.8 | 14 | 18.5 | 9 | 11.8 | 22 | 28.9 | 19 | 25 | 3.29 | Wastani |
| Madai ya wanasiasa kuhusu ufisadi | 24 | 31.6 | 14 | 18.4 | 7 | 9.2 | 26 | 34.2 | 5 | 6.6 | 2.66 | Wastani |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| katika hotuba zao ni ya kuaminika. | | | | | | | | | | | | |
| **Jumla** | | | | | | | | | | | **3.11** | **Wasta ni** |

Jedwali 4.21, linawasilisha matokeo ya uchanganuzi wa data kutokana na hojaji ya Likati. Matokeo haya yanaonyeshakuwa kati ya maswali 6 waliyoulizwa wahojiwa, matatu yaliibua mielekeo chanya miongoni mwao na mengine matatu yakaibua mielekeo ya wastani. Dhana zilizoibua mielekeo chanya ni: hali ya wasikilizaji kusikiliza sana hotuba za wanasiasa zinazoangazia suala la ufisadi; hali ya wanasiasa kuangazia suala la ufisadi kila mara katika hotuba zao na ya mwisho ni hali ya wananchi kuamini kuwa wanasiasa wakiacha kuangazia ufisadi katika hotuba zao visa vya ufisadi vitaongezeka.Kutokana na matokeo haya, imebanika kuwa wananchi wana imani na matumizi ya hotuba za kisiasa katika juhudi za kupambana na ufisadi. Aidha, matokeo haya yanaafikiana na mhimili wa pili wa nadharia ya UUH ambapo Van Dijk (1998) anaeleza kuwa watu wenye mamlaka katika jamii huwa na uwezo wa kuamulia jamii na kuishawishi dhidi ya kile wanachokiona kuwa kinyume na maadili ya jamii.

Kwa upanda mwingine, kuna dhana tatu ambazo wananchi walishikilia mielekeo ya wastani. Dhana hizi ni: imani kuwa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi huwaogopesha wafisadi; hali ya wananchi kufurahia jinsi wanasiasa wanavyoangazia ufisadi katika hotuba zao na ya tatu ni hali ya kuaminika kwa madai yanayotolewa katika hotuba za wanasiasa. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa wananchi wanakubaliana na hali hizi kwa kiwango fulani tu.

Aidha, uchanganuzi wa data kwenye Jedwali 4.21 unaonyesha kuwa kwa ujumla wananchi wana alama wastani 3.11 ambazo zinamaanisha kuwa mwelekeo wao ni wa wastani. Matokeo haya yanaweza kufafanuliwa kuwa wananchi wa Kenya wanakubaliana kwa kiwango cha wastani na hali ya wanasiasa kutumia hotuba zao kuangazia suala la ufisadi nchini. Hii ina maana kuwa, kwa viwango fulani wanakubaliana kuwa ni njia bora ya kupambana na ufisadi ingawa pia wanahisi ina mapungufu yake.Kwa ujumla, uchanganuzi wa data kuhusu mielekeo uliongozwa na mhimili wa kwanza ambao unaeleza kuwa, kuna uhusiano kati ya matukio ya kiusemi, siasa, jamii na utamaduni; hasa vile usemi unavyoathiriwa na itikadi na vile usemi wenyewe unaweza kuathiri matukio katika jamii (Fairclough, 1995). Hapa, athari za semi za wanasiasa kwa wananchi wa Kenya zilitumiwa kubainisha mielekeo yao kuhusu hotuba za kisiasa.

## 4.3 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amechanganua na kulinganisha athari za hotuba za kisiasa kuhusu suala la ufisadi kwa wananchi wa Kenya ambalo ni lengo la pili la utafiti na kisha baadaye akachunguza mielekeo yao kuzihusu ambalo ni lengo la tatu la utafiti. Nadharia ya UUH ndio iliyotumiwa katika kuhakiki maoni ya watafitiwa ili kubaini athari za hotuba hizi kwa wananchi na pia mielekeo yao kuzihusu. Matokeo ya uchanganuzi huu yaliwasilishwa kwa maelezo na takwimu kwenye majedwali. Kuhusu athari za hotuba hizi, imebainika kuwa wananchi wa Kenya huathirika kwa njia mbalimbali.Athari hasi na chanya zilibainika. Athari chanya zilizodhihirika ni: kuhamasika, kushawishika, kuzinduka, kufarijika, kufurahisha na kuwapa wananchi matumaini. Kwa upande mwingine, athari hasi zilizobainika ni: kuchochea ufisadi kuendelea, kujenga hali ya mapuuza, kutishika kwa

wafisadi na wenye nia ya kushiriki, kuogopesha wanaoshiriki ufisadi, kusababishia wafisadi kiherehere na kuwaudhi baadhi ya wananchi.

Kuhusu mielekeo, utafiti huu umebainisha kuwa wananchi wa Kenya wana mwelekeo wa wastani kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi nchini; yaani wanaonekana kuridhishwa na hotuba hizi kwa kiwango cha wastani tu. Katika sura ifuatayo, mtafiti atashughulikia matokeo ya utafiti huu kwa ujumla na kutoa mapendekezo yake.

# SURA YA TANO

# MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti anatoa muhtasari wa masuala yote yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu kuanzia sura ya kwanza hadi ya nne. Utafiti huu uliangazia uchanganuzi wa matini za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kuanzia mwaka 2015 hadi 2020. Katika jamii yoyote ile, viongozi mbalimbali hutazamiwa kuangazia masuala mbalimbali yanayoathiri jamii zao kwa lengo la kufahamisha, kuhimiza matendo mazuri na vilevile kukashifu mabaya ili wanaohusika wabadilike. Viongozi wa kisiasa nchini Kenya wameweza kutekeleza jukumu hili katika hotuba zao za kisiasa kwa malengo yaya haya kwa muda mrefu. Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.1, suala la ufisadi limekuwa mojawapo ya matatizo makuu ambayo nchi ya Kenya imeshuhudia kwa miaka kadhaa na hata kuorodheshwa na shirika la Transparency International (2019) miongoni mwa nchi ambazo zinashuhudia visa vingi vya ufisadi. Ni kwa sababu hii wanasiasa wengi nchini huliangazia suala hili katika hotuba zao kila mara. Hali hii ndio iliyompa mtafiti ilhamu ya kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba hizi ili kubaini zinavyoangazia suala la ufisadi na pia kutambua athari za hotuba hizi kwa wananchi pamoja na mielekeo waliyo nayo kuzihusu.

## 5.1 Muhtasari

Data iliyotumiwa katika utafiti huu ilikusanywa maktabani kupitia mtandao wa Youtube na vilevile kupitia utafiti wa nyanjani. Kwenye mtandao wa Youtube, mtafiti alipakua baadhi ya hotuba za wanasiasa teule zilizoangazia suala la ufisadi katika sakata mbili kuu; sakata ya Shirika la kitaifa la huduma kwa vijana (NYS) na sakata ya mabwawa ya Arror

na Kimwarer. Hotuba sita ziliteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Nyanjani, Mji wa Mumias ndio ulioteuliwa kwa sababu una wafuasi wa vyama mbalimbali vya kisiasa hivyo maoni yao yaliweza kuangazia mirengo yote ya kisiasa. Jumla ya watafitiwa 76 walitumiwa-wanawake 38 na wanaume 38 ambao walichaguliwa kimakusudi kwa kuzingatia viwango vyao vya elimu. Watafitiwa walijaza hojaji wazi na hojaji funge ya likati ambazo zilitumiwa kupata data kuhusu athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi na pia mielekeo ya wananchi kuhusu matumizi ya hotuba hizi katika kuangazia suala la ufisadi nchini.

Kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu, mtafiti alizingatia miundo miwili ya utafiti: muundo wa maelezo na muundo wa kisoroveya ili kuyashughuikia malengo yote barabara. Muundo wa kimaelezo ulitumiwa kufafanua na kulinganisha sifa za matini mbalimbali ya hotuba za kisiasa yaliyoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Aidha, muundo wa kisoroveya uliweza kutumiwa kusanya data kuhusu maoni ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa zilizoangazia suala la ufisadi. Maoni haya yalitumiwa kubainisha athari za hotuba hizi kwa wananchi na pia mielekeo yao kuzihusu.

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Usemi Hakiki (UUH) iliyoasisiwa na Fairclough (1989). Kwa kutumia mihimili ya nadharia hii, mtafiti alichanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa za viongozi teule wa kisiasa kuhusu suala la ufisadi kwa kubainisha sifa zake, uhusiano baina ya matini ya hotuba na uwasilishaji wake na kisha akabainisha uhusiano baina ya utendaji (uwasilishaji) na muktadha wa kijamii ambapo alichanganua na kulinganisha athari za hotuba hizi kwa

wananchi na pia mielekeo yao kuzihusu. Baada ya uchanganuzi, data iliwasilishwa kupitia maelezo, takwimu, pai chati na majedwali.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Baada ya uchanganuzi na ulinganisho wa data ya matini za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa kielelezo cha nadharia ya UUH, utafiti huu uliweza kubainisha mambo kadhaa. Kwanza, ilibainika kuwa kiisimu, matini ni matumizi ya lugha na ndio huunda na kujenga maana. Aidha, utafiti ulibainisha kuwa dhima kuu ya hotuba za kisiasa ni kushawishi hadhira kuhusu suala fulani. Isitoshe, ndiposa hotuba iweze kutekeleza jukumu hili ni lazima iwe na ukwasi wa tamathali za usemi. Ilibainika kuwa, viongozi wote wawili ambao hotuba zao zilichanganuliwa walitumiambinu 12 za kimtindo katika hotuba zao teule.

Mbinu ya kwanza iliyobainika ni matumizi ya istilahi maalum zinazohusiana na ufisadi na vita dhidi yake. Mojawapo wa istilahi ambayo ilitumiwa na viongozi wote wawili ni *wezi*. Viongozi hawa waliitumia istilahi hii kusawiri wafisadi kama wezi wa mali ya umma na hivyo basi kusawiriwa kama adui wa maendeleo ya nchi. Aidha, wote walitumia istilahi mbalimbali kudhihirisha vita dhidi ya ufisadi kama vile *washikwe*na *tutapambana*.

Pili, ni matumizi ya viwakilishi nafsi mbalimbali wanapoangazia suala la ufisadi. Viongozi hawa wawili walitumia kiwakilishi nafsi huru ‘mimi’ kudhihirisha mamlaka yao na kuwarai wananchi kuwaunga mkono katika vita dhidi ya ufisadi. Aidha walitumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza tegemezi ‘ni’ kwa dhima hiyo hiyo. Kwa kulinganua,

ilibainika kuwa ni matini za hotuba za Uhuru pekee ambazo zilisheheni matumizi ya kiwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi 'tu'. Hii basi ina maana kuwa yeye alithamini ushirikiano wake na watu wengine katika kutekeleza jukumu la kupiga vita ufisadi. Kiwakilishi cha nafsi ya pili katika umoja 'wewe' kilibainika pia katika matini za hotuba za viongozi hawa wawili. Walitumia kiwakilishi hiki kujitenga na wote waliohusika na matendo ya ufisadi na kuwataka wawe tayari kukabiliana na sheria ipasavyo. Hali kadhalika, viongozi hawa walitumia kiwakilishi cha nafsi ya tatu katika wingi 'wa' kuwasuta wafisadi kuwajibikia matendo yao ya ufisadi wenyewe.

Mbinu ya tatu ni kuwasawiri wananchi kama wenye mamlaka makuu. Wanasiasa teule walitumia kauli; *Wakenya wanasema wale wote ambao walihusika na wizi hii washikwe na washtakiwe* na *Wakenya wamechoka kungojea wakiona watu wanaenda, mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.* Kauli hizi ingawa zilitolewa na viongozi, zinarejelea hali ya wao kuwa wasemaji tu wa maamuzi ambayo yamekwisha afikiwa na wananchi. Kwa njia hii wanawachochea wananchi kuunga mkono mtazamo wao kuhusu suala hili.

Nne, ni matumizi ya toni ya kukejeli ambapo ilibainika kuwa viongozi hawa walikejeli hatua za taasisi za kupambana na ufisadi - EACC na mahakama -kwa kile ambacho walisawiri kama utepetevu wa kushughulikia washukiwa wa ufisadi. Mbinu hii pia inakaribiana na ile ya kinaya ambapo ilibainika kuwa wanasiasa hawa wanasawiri hali ya kinaya kuwa taasisi ambazo zinastahili kuwa mbele katika vita dhidi ya ufisadi ndizo zinazowatetea baadhi ya wafisadi hasa wale wakubwa na kulenga tu wale wadogo.

Mbinu nyingine ni matumizi ya lugha yenye takwimu. Mfano; *Milioni 800 imeibwa.* Ilibainika kuwa wanasiasa hawa wawili walitumia takwimu kudhihirisha usahihi, umuhimu na msisitizo wa ujumbe waliokuwa wakiwasilishia hadhira yao kama ilivyodhihirika katika mfano hapo juu. Aidha, katika muktadha mwingine, mbinu hii iliweza kusawiri hali ya kejeli. Mfano; *Mtu anapatwa ameiba* ***bilioni moja*** *akienda anapatiwa 'bail' ya* ***shilingi elfu hamsini.*** Kwa kuzingatia mfano huu, takwimu zimetumiwa kukejeli hali ya mahakama kuwaachilia wezi wa mabilioni huku wakihukumu wezi wa kiasi kidogo cha pesa kama elfu hamsini pekee.

Mbinu ya sita iliyobainika ni matumizi ya lugha yenye matumaini ambapo wananchi wanahakikishiwa kuwa viongozi wao wana mkakati wa kupambana na ufisadi ambao utawahakikishia kuwa mali zao hazitapotea tena kupitia ufisadi. Kwa mfano, wanatumia kauli kama; *Tumesema hiyo mali yote ambayo watu wamenyakua, tutahakikisha imerudishwa.*

Saba, ilibainika kuwa viongozi wote wawili walitumia toni ya kukashifu ambapo walikashifu taasisi zinazohusiana na vita dhidi ya ufisadi. Raila alikashifu tume ya kupambana na ufisadi ya EACC kwa kile alikiita *kusafisha wezi,* yaani kuwaondolea wafisadi mashtaka. Katika hotuba za Uhuru, naye pia anakashifu mahakama kwa kudai kuwa inawaachilia mafisadi wakubwa anapoeleza kuwa …*mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini*.

Mbinu ya kuchangaya msimbo pia ilitumiwa na viongozi hawa wote katika hali ya kusisitiza ujumbe wao. Mbinu hii ilitumiwa sana kusisitiza kiasi cha pesa zilizoibwa au kutumiwa visivyo. Kwa mfano, katika matini ya hotuba ya Raila anasisitiza kuwa pesa nyingi za umma zinaibiwa kupitia ufisadi anaposema; *Eight hundred bilion shillings ambayo Wakenya wanapoteza kila mwaka kwa ufisadi.*

Aidha, hotuba hizi zilisheheni matumizi ya kinaya. Imebainika kuwa wanasiasa hawa wawili walitumia mtindo wa kinaya kusuta utepetevu katika taasisi zinazohusika na vita dhidi ya ufisadi. Kwa kutumia mbinu hii, wamesawiri tabia za wanaohudumu katika taasisi husika kama wasiowajibikia vita dhidi ya ufisadi. Aidha, wameweza kuwazindua wananchi katika kubaini hali halisi ya mambo. Kwa mfano, Uhuru anatumia mbinu hii kukejeli utendakazi wa mahakama anapoeleza, *Mtu anapatwa ameiba bilioni moja akienda anapatiwa bail ya shilingi elfu hamsini.*

Matumizi ya takriri pia ilibainika katika matini ya hotuba za viongozi hawa. Kwa kutumia mbinu hii, wanasiasa hawa walilenga kusisitiza jumbe zao kuhusu matendo ya ufisadi nchini. Kwa mfano, walitumia kauli zifuatazo; *Si nilisema? Si nilisema?* na *Wewe ni mwizi! Ni mwizi!* Kando na kusisitiza hoja zao, kauli hizi zililenga kuibua hisia za majuto na chuki mtawalia.

Mbinu nyingine ni matumizi ya maswali balagha ambayo viongozi hawa walitumia kwa lengo la kuwazindua wananchi kutafakari kuhusu hali iliyoshuhudiwa. Kwa mfano; *Mbona wezi wa mabilioni hawahukumiwi?* Aidha, maswali haya yameweza kutumiwa kama njia

ya kuwashawishi wananchi kuunga mkono madai wanayowasilisha katika hotuba zao. Kwa mfano; *Si mpaka tu uchunguzi ifanywe?*

Mbinu ya mwisho iliyobainika katika matini ya hotuba teule ni 'matumizi ya virai shawishi.' Wanasiasa teule walitumia virai hivi shawishi kwa lengo la kuwashawishi wasikilizaji wao kukubaliana na mitazamo yao. Mfano 1; *Mara ile nyingine niliongea juu ya mambo ya wizi katika idara ya NYS.* ***Si nilisema? Si nilisema?*** Mfano 2; *Chukua msalaba yako wako peke yako!* ***Au namna gani wenzangu?***

Utafiti huu pia ulibainisha sifa 5 za hotuba za kisiasa kama ifuatavyo; kuwepo kwa taarifa, malengo, utata, msimamo na ushawishi. Taarifa na malengo muhimu yaliyobainika katika matini ya hotuba za viongozi wa kisiasa teule ni: kusawiri ufisadi kama uozo katika jamii, kukemea mafisadi; kukemea utepetevu katika taasisi zinazohusiana na vita dhidi ya ufisadi na pia kuwashawishi wananchi kuunga mkono hatua wanazopendekeza kuchukuliwa katika vita dhidi ya ufisadi. Kwa kuwa wana mamlaka katika jamii kutokana na nafasi zao za kisiasa, walilenga kushawishi wananchi kutojihusisha katika ufisadi kwani wanaamini kuwa ni kinyume na maadili ya jamii. Aidha, ilibainika kuwa viongozi hawa wawili walizua utata kwa kuwaingiza wapinzani wao katika suala hili au viongozi wa taasisi za kupambana na ufisadi ili kuamsha hisia fulani miongoni mwa wafuasi wao za kuona haja ya kujiunga nao ili kuikabili hatari iliyopo. Katika hotuba ya Raila, anamlaumu Rais Uhuru kwa kumwondoa mshukiwa mmoja katika orodha ya wafisadi aliyopeleka bungeni ili kuwasimamisha kazi kwa muda. Aidha, viongozi hawa wote wanakashifu idara ya mahakama kwa utepetevu katika kushughulikia kesi za ufisadi.

Hotuba za kisiasa zimeweza kubainishwa katika vipengele vitatu; mhutubu, mhutubiwa na hotuba yenyewe. Aidha, wataalamu wanasisitiza kuwa katika uchanganuzi wa matini ya hotuba za kisiasa, ni lazima wanasiasa husika, wapokezi wa hotuba na matini ya hotuba yenyewe waweza kuhakikiwa. Kwa misingi hii, utafiti huu kando na kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba teule za wanasiasa, maoni ya wananchi ambao ni wapokezi wa hotuba hizi yaliweza kuhakikiwa ili kubaini athari za hotuba hizi kwao na pia kubaini mielekeo yao kuzihusu.

Kuhusu athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi, utafiti huu ulitambua kuwa wananchi wa Kenya huathirika kwa njia hasi na chanya kutokana na hotuba hizi. Athari hizi zilibainishwa na kujadiliwa katika makundi matatu yafuatayo: athari kwa wafisadi; athari kwa wenye nia ya kushiriki ufisadi na athari kwa wananchi wanaopiga vita ufisadi. Aidha, ilibainika kuwa athari hizi huweza kuwekwa katika makundi mawili makuu; athari chanya na hasi. Athari hasi zifuatazo zilibainika.

Kwanza kabisa ni kuhamasika ambapo wananchi walikiri kuwa hotuba za wanasiasa zinapoangazia visa mbalimbali vya ufisadi ambavyo vinatendeka nchini wao hupata ufahamu wa yanayotendeka. Isitoshe, wanasiasa hukemea vitendo hivi vya ufisadi na kufafanua madhara yake kwa wanaojihusisha nayo na pia kwa taifa zima. Kwa kufanya hivyo, wananchi wanaosikiza hotuba hizi huweza kujenga shehena yao ya maarifa zaidi.

Athari ya pili ni kushawishika. Wananchi walikiri kushawishika kuwa vita dhidi ya ufisadi vinaendelezwa vyema viongozi wao wanapoangazia suala hili katika hotuba zao kila mara. Aidha, lugha kali wanayotumia kuwatishia wafisadi kuwa hatua kali dhidi yao itachukuliwa huwapa imani kuwa viongozi wao wamewajibika ifaavyo kukemea maovu katika jamii kama inavyotarajiwa.

Kando na kushawishika, ilibainika kuwa wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi huwazindua kwa njia mbalimbali. Ya kwanza ni kuwa wanapoangazia jinsi wizi wa mali ya umma unatakelezwa, wao hupata kuzinduka na kuwa makini. Pili ni kuwa, katika hotuba hizi, wanasiasa huangazia madhara ya ufisadi mbalimbali kwa wahusika na nchi nzima. Kwa kufanya hivyo, wao huzinduliwa kwa kuelimishwa kujua kuwa ufisadi ni adui wa taifa zima. Kwa njia hii, wao huona haja ya kufanya maamuzi ya kutoshiriki ufisadi na hata kushirikiana na viongozi katika vita dhidi ya ufisadi.

Wananchi wengine pia hufarijika na kupata matumaini kutokana na hotuba hizi. Baadhi yao walikiri kuwa wakati hotuba hizi zinakashifu wafisadi bila uoga na kuahidi kukabiliana nao kisheria, wao hupata matumaini kuwa viongozi wao watakabili tatizo hilo. Aidha, wao hufarijika wanaposikiza hotuba za viongozi ambao wanaahidi kuhakikisha kuwa mali iliyoibwa itarejeshwa na wezi hao hawataiba mali ya umma tena.

Aidha, ilibanika kuwa baadhi ya wananchi hufurahishwa na hotuba hizi. Hotuba hizi huwapa furaha kutokana na jinsi wanavyokemea wafisadi na kuwatia uoga. Wao hutumia

istilahi maalum za kukashifu wafisadi na kuahidi hatua kali za kisheria. Kwa njia hii, wananchi hufarahishwa na ukakamavu wa viongozi katika kukabili hali hii.

Wananchi hushawishika kwa njia mbalimbali kutokana na hotuba hizi. Wao huridhika na hali ya wanasiasa kukemea walioiba kwa kutumia lugha kali ambayo hudhihirisha kuwa kuna adhabu kali kwa wafisadi. Aidha, kwa kuangazia suala hili, wananchi huwa na imani kuwa wanasiasa wanatekeleza wajibu wao ifaavyo na hivyo basi wao hushawishika kuwa vita dhidi ya ufisadi viko imara.

Kwa upande mwingine, athari hasi pia zilibainika kutokana na hotuba hizi. Ya kwanza ni kuudhika. Ilibainika kuwa baadhi ya wananchi huudhika sana na hotuba hizi kwa kuwa baadhi ya wanasiasa wanadai kukemea ufisadi ilhali wao pia wanajihusisha nao. Isitoshe, walidai kuwa baadhi yao hukashifu tu wapinzani wao kisiasa ambao ni fisadi ila wandani wao kisiasa ambao ni fisadi hawakashifiwi bali wanawatetea.

Athari hasi ya pili ni kuwafanya wananchi kuwa na kiherehere. Wananchi walikiri kujawa na kiherehere wanaposikia viongozi wao walikililia wizi wa mali ya umma na kueleza madhara yake kwa taifa. Hii huwafanya kukosa utulivu kabisa kwani wanajua maisha yao yapo hatarini kutokana na ufisadi ambao unaangaziwa kila mara katika hotuba hizi.

Wafisadi nao hutishika na kuogopa kutokana na hotuba hizi. Ilibainika kuwa baadhi ya wafisadi hutishwa sana na kauli za wanasiasa katika hotuba hizi zinazodai kuwachukulia

hatua kali za kisheria wale wote wanaojihusisha na ufisadi. Wananchi walikiri kuwa lugha kali na ya vitisho kwenye hotuba hizi huwakosesha baadhi ya wafisadi amani.

Kando na kutishika, ilibainika kuwa baadhi ya wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi huchochea ufisadi kuendelea kwa sababu ya ahadi za wanasiasa zisizotimia. Walidai kuwa, wanasiasa hutishia kuhakikisha kuwa wafisadi wameadhibiwa ila hakuna lolote linalofanywa baadaye. Isitoshe, walidai kuwa baadhi ya viongozi hawa pia wanajihusisha na ufisadi pamoja na wandani wao. Aidha, wananchi wanaamini kuwa, kwa kuangazia masuala ya ufisadi katika hotuba za wanasiasa, wafisadi hujua mbinu zao zimegunduliwa na hivyo wanatafuta mbinu nyingine za kuendeleza mipango yao. Kutokana na hali hizi, wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi huchochea tu ufisadi kuendelea.

Athari hasi ya mwisho ni mapuuza. Ilibainika kuwa baadhi ya wananchi huzipuuza hotuba hizi kutoka na imani kuwa hazina manufaa yoyote katika vita dhidi ya ufisadi. Walidai kuwa vitisho wanavyotoa wansiasa katika hotuba hizi ni gumzo tupu lisilowekwa katika vitendo. Aidha, walisisitiza kuwa hawaziamini hotuba hizi kabisa kwani wanasiasa wanaohotubu wakikashifu ufisadi wanashiriki pia pamoja na wandani wao. Kwa misingi hii, baadhi ya wananchi hawaoni haja ya kuzisikiza hotuba hizi.

Kuhusu mielekeo, utafiti huu ulibainisha kuwa kwa ujumla wananchi wa Kenya wana mwelekeo wa wastani kuhusu hotuba za kisiasa zinazoangazia suala la ufisadi nchini; yaani wanaoonekana kuridhika na jinsi hotuba hizi zinavyoangazia suala la ufisadi na vita dhidi yake kwa kiwango cha wastani tu. Kwa mujibu wa maswali ya mtafiti kwenye hojaji,

masuala mbalimbali yilitafitiwa kuhusu hotuba hizi. Masuala haya ni; usikilizaji wa hotuba hizi, kuaminika kwa madai yanayoangaziwa, uwezo wa hotuba hizi kukemea na kuogofya mafisadi, kufurahishwa na jinsi zinavyoangazia suala la ufisadi, uwezo wake wa kupunguza ufisadi na hatima yake. Wananchi walidhihirisha mwelekeo chanya kuhusu masuala machache huku mengine wakiwa na mwelekeo wa wastani.

Wananchi walidhihirisha mielekeo chanya katika masuala yafuatayo. Kwanza ni suala la usikilizaji wa hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi. Ilibainika kuwa wananchi wengi husikiliza hotuba hizi kila mara kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Hii ina maana kuwa wanazithamini hotuba hizi na hivyo basi ilibainika kuwa wana mwelekeo chanya kuzihusu. Suala la pili ni kufurahishwa na jinsi zinavyoangazia suala la ufisadi. Hapa utafiti ulibaini kuwa wengi hufurahishwa na jinsi hotuba hizi huangazia suala la ufisadi na kutaka wazidi kuangazia kila mara.  Suala la tatu ambalo wananchi wana mwelekeo chanya kulihusu ni uwezo wa hotuba hizi kuchangia pakubwa katika kupunguza visa vya ufisadi nchini. Wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi zimechangia sana katika kupunguza visa vya ufisadi na kushikilia kuwa endapo wataacha kuangazia, basi visa vya ufisadi vitaongezeka.

Kwa upande mwingine, mielekeo wastani ilibainika katika masuala yafuatayo. Suala la kwanza ni hali ya kuaminika kwa madai yanayotolewa kwenye hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi. Ilibainika kuwa idadi ya Wakenya wanaoamini madai haya kama ya kweli na wasioyaamini inaelekea kuwa sawa.  Mwelekeo wastani pia ulibainika kuhusu jinsi wanasiasa wanavyoangazia suala la ufisadi ambapo baadhi walikubaliana na jinsi

wanasiasa wanavyoangazia suala la ufisadi katika hotuba zao na wengine kutokubaliana kabisa na namna wanavyolishughulikia.

Kadhalika, ilibainika kuwa wananchi wana mwelekeo huu wa wastani kuhusu suala la hotuba hizi kuwa na uwezo mkubwa katika mapambano dhidi ya ufisadi. Ifahamike hapa kuwa wananchi wanaamini kuwa hotuba hizi zimechangia katika kuukabili ufisadi kama ilivyoelezwa hapo awali ila hawakubaliani kuwa zina mchango mkubwa katika vita hivi. Mwisho, ilibainika kuwa wananchi wana mwelekeo wa wastani kuhusu uwezo wa hotuba hizi kuwaogofya wafisadi. Baadhi wanaamini kuwa wafisadi huogopa sana wanapotajwa katika hotuba hizi huku idadi inayokaribiana na hiyo wakishikilia kuwa hotuba hizi hazina uwezo wa kuwaogofya wafisadi.

## 5.3 Mahitimisho ya Utafiti

Binadamu amejaliwa uwezo wa kutumia lugha kuwasiliana na mwenzake katika jamii. Yanayoangaziwa katika mawasiliano haya huwa ni masuala yanayomzingira na kumwathiri binadamu kwa njia fulani. Aghalabu, viongozi mbalimbali hutazamiwa na jamii kuangazia masuala yanayoathiri jamii hasa matatizo ambayo jamii inakabiliana nayo na kutoa suluhisho. Katika nchi ya Kenya, ufisadi ni mojawapo ya matatizo yanayowakabili wananchi kwa kuwa husababisha kudorora kwa hali ya uchumi wa nchi. Ni kutokana na hali hii ambapo wanasiasa pamoja na viongozi wengine huangazia suala la ufisadi katika hotuba zao za kila mara kwa wananchi. Utafiti huu ulilenga kuchanganua na kulinganisha matini ya hotuba za kisiasa kuhusu suala la ufisadi kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.

Kama wanavyosisitiza wataalamu kuwa katika uchanganuzi wa matini ya hotuba za kisiasa ni lazima mtafiti ahakiki wanasiasa husika, wapokezi wa hotuba na pia matini ya hotuba yenyewe, utafiti huu ulishughulikia malengo matatu ambayo yalizingatia matakwa haya. Lengo la kwanza lilikuwa ni kulinganisha namna matini ya hotuba za kisiasa yanavyoshughulikia ufisadi, la pili likawa ni kubainisha athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya nalo la mwisho lilikuwa kudhihirisha mielekeo ya wananchi kuhusu hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi.

Utafiti huu ulibainisha kuwa matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi yanasheheni mbinu kadhaa za kimtindo ambazo wanasiasa hutumia kwa dhima ya kupiga vita ufisadi. Baadhi ya mbinu zilizobainishwa ni: matumizi ya misamiati au istilahi maalum zinazofafanua ufisadi au vita dhidi yake; matumizi ya viwakilishi nafsi kwa mfano nafsi ya kwanza umoja na wingi ilitumiwa kuonyesha juhudi za mwanasiasamwenyewe katika utendaji au ushirikiano wake na wengine; kuwasawiri wananchi kama wenye mamlaka makuu katika kukabili matatizo yanayowakumba kwa kufanya maamuzi mwafaka; toni ya kukejeli baadhi ya matendo yasiyofaa; toni ya matumaini hasa kwa kulenga kuwashawishi wananchi kuwa viongozi wao wanafanya juhudi mwafaka kutatua tatizo la ufisadi; toni ya kukashifu hasa matendo ya ufisadi na utepetevu wa baadhi ya viongozi wa taasisi mbalimbali; lugha yenye takwimu ambayo ilitumiwa kusawiri hali halisi ya madhara ya ufisadi; kuchanganya msimbo katika juhudi za wanasiasa kutaka kujieleza vyema zaidi; kinaya wanaporejelea utepetevu wa taasisi zinazohusika na vita dhidi ya ufisadi au viongozi wengine; matumizi ya takriri katika kusisitiza hali mbalimbali; matumizi ya

maswali balagha kuwatafakarisha wananchi na mwisho ni matumizi ya virai shawishi katika juhudi za kuwashawishi wananchi kuunga mkono maoni yao.

Kuhusu athari za hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya, utafiti huu ulibainisha athari kadhaa ambazo ziliweza kugawika katika makundi mawili makuu- athari hasi na chanya. Athari chanya zilizodhihirika ni: kuhamasika, kushawishika, kuzinduka, kufarijika, kufurahisha na kuwapa wananchi matumaini. Kwa upande mwingine, athari hasi zilizobainika ni: kuchochea ufisadi, kujenga hali ya mapuuza, kutishika, kuogopesha, kusababisha kiherehere na kuwaudhi wananchi.

Aidha, utafiti huu kupitia uchanganuzi wa maoni ya wahojiwa katika hojaji ya Likati, ulibainisha kuwa wananchi wana mwelekeo wa wastani kuhusu hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi. Matokeo haya yanaweza kufafanuliwa kuwa wananchi wa Kenya wanakubaliana kwa kiwango cha wastani na hali ya hotuba za kisiasa kuangazia suala la ufisadi nchini.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Baada ya uhakiki wa matini ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi, utafiti huu uliweza kubanisha kuwa wanasiasa hutumia lugha kwa njia ya kipekee kupitia mbinu mbalimbali za kimtindo kuusawiri ufisadi kama adui wa wananchi kwani unaathiri vibaya uchumi wa nchi. Mbinu kadhaa za kimtindo ziliweza kubainishwa na kuchangaliwa japo si kwa kina sana kwa kuwa zilikuwa nyingi. Utafiti huu unapendekeza wanaisimujamii kufanya utafiti zaidi katika eneo hili kwa kuangazia mbinu moja moja ili utafiti wa kina uweze kuangaziwa.

Aidha, ilibainika kuwa wananchi wanaamini kuwa hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi zina mchango muhimu katika vita dhidi ya ufisadi na hivyo wangependa viongozi hawa waendelee kuangazia suala hili katika hotuba zao kila mara. Katika utafiti huu, tulilenga matini ya hotuba za wanasiasa pekee katika kutekeleza jukumu hili ila kuna viongozi wengi ambao pia wanaangazia suala la ufisadi kila mara katika hotuba zao kwa dhima hii ya kupiga vita ufisadi. Ni vyema kwa utafiti mwingine kufanywa ili kuhakiki matini ya hotuba za viongozi wengine kama vile wa kidini, wanaharakati, viongozi wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wasomi mbalimbali kuhusu suala hili la ufisadi ili kubaini wanavyoangazia suala hili na mchango wa hotuba zao katika juhudi za kupambana na ufisadi.

Utafiti huu ulilenga maudhui teule ya ufisadi katika hotuba za wanasiasa teule kwa kuwa ufisadi ni mojawapo ya matatizo ambayo nchi ya Kenya inakabiliwa nayo. Ni wazi kuwa, kando na ufisadi, wanasiasa huangazia masuala mengine mengi ambayo yanaathiri nchi kama ukabila, umaskini, ukosefu wa ajira, gharama ya juu ya maisha miongoni mwa masuala mengine. Kwa sababu hii, utafiti huu unapendekeza utafiti mwingine kushughulikia masuala haya mengine yanayoathiri jamii ili kubaini sifa za lugha inayotumiwa na mchango wake katika kusuluhisha matatizo hayo.

Mtafiti ameshawishika kuwa, kando na utafiti huu, iwapo tafiti nyingine zilizopendekezwa zitashughulikwa katika tafiti za baadaye, basi kutakuwa na mchango mkubwa katika uhakiki wa matini ya hotuba za kisiasa kuhusu maudhui maalum. Isitoshe, sajili hii ya

lugha ya kisiasa itakuzwa zaidi iwapo sifa zaidi za lugha zitabainishwa na kujadiliwa kwa kina kama inavyopendekezwa katika utafiti huu. Aidha, taaluma ya uchanganuzi wa matini ya hotuba kwa ujumla itakuzwa zaidi iwapo uhakiki wa matini ya hotuba za viongozi wengine kuhusu suala la ufisadi utashughulikiwa. Hali kadhalika, uhakiki wa matini ya hotuba za viongozi mbalimbali kuhusu ufisadi zitasaidia taasisi zinazohusiana na ufisadi kubainisha mchango wa hotuba hizi ili waweze ama kuhimiza kuendelea kutumiwa iwapo zinachangia katika vita dhidi ya ufisadi au kuzipinga iwapo hazichangii katika vita dhidi ya ufisadi. Kwa ujumla tafiti hizi zitachangia katika maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa uhakiki matini.

## MAREJELEO

Adero, M.C. (2005). *Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya Kuanzia Mwaka 2002 hadi 2005*. M.A.Thesis; Kenyatta University.

Agheyisi, R. na Fishman, S. (1970). *Language Attitude Studies: A brief Survey of Methodological approaches*. Katika Anthropological Linguistics, VOL 12 No 5 1970, pp 137 -157.

Areba, I. M. (2017). *Uchanganuzi wa Lugha ya Wanawake Katika Mabaraza ya Chifu*: Mifano Kutoka Kata ya Kegati, Kaunti ya Kisii. (Unpublished M.A. Thesis) Chuo Kikuu cha Kisii, Kisii.

Atieno, E. O. (2016). *Uchambuzi wa Matini*: Matumizi ya Lugha ya Kiswahili Katika Vivutio vya Watalii. M. A. Thesis; Kenyatta University.

Beard, A. (2000). *Language of Politics.* London: Routledge.

Beaugrande, R. & Dressler, A. (1981). *Introduction to Text Linguistics.* New York: Longman.

Chilton, P. (2004). *Analyzing Political Discourse: Theory and Practice*. London: Routledge (Taylor and Francis).

Citizen Digital. (2018, December 28). *National Youth Service (NYS) Scandal II*. Retrieved January 03, 2022, from Multi-Bilion Corruption Scandals That Rocked Kenya In 2018: https://citizen.digital/news

Cook, G. (1989). *Discourse.*New York: Oxford University Press.

Crystal, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman.

Crystal, D. (1997). *The Cambridge Encyclopaedia of Language.* 2ndEdition. Cambridge: Cambridge University Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power.* New York: Longman Group Ltd.

Fairclough, N. (1995). *Discourse and Social Change*. UK: Blackwell.

Gray, D. E. (2009). *Doing Research in the Real World*. London: SAGE Publication Ltd.

Gray, M. (1984). *A Dictionary of Literary Terms*. Essex: Longman York Press.

Habwe, H.J (1999). *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches.* PHD Thesis, University of Nairobi.

Habwe, H. J. (2010). Dialogue drama in Kenyan Political Speeches and its Pragmatic Implications, *Nordic Journal of African Studies 19(3): 165–180*.

Hakansson, J. (2012). *The use of personal Pronouns in Political Speeches. A Comparative Study of the Pronominal Choices of two American Presidents*. Linnaeus University.

Halliday, M.A.K. (1985). *Spoken and Written Language*. Geelong: Victoria Deakin University Press.

Haugerud, A. & Njogu, S. K. (1991). *State Voices in the Countryside: Politics and the Kenyan Baraza.*African Studies Center, Boston: Boston University.

https://thefourthestategh.com/2021/05/07/the word 'corruption' missing in Akufo-Addo's State of Nation Address (thefourthestategh.com)

https://www.kenyans.co.ke/news/38525-SOTN 2019: President Uhuru Gives One Condition to Fire CSs - Kenyans.co.ke

https://www.bbc.com/swahili/habari-47811550-SOTN: Wakenya watarajie nini katika hotuba ya rais Uhuru Kenyatta? - BBC News Swahili

Johnstone, B., (2008). *Discourse Analysis*. London: Blackwell Publishing.

Joseph, J.E. (2006). *Language and Politics*. Edinburgh: Edinburgh University Press

Kenya National Bureau of Statistics. (2019). *City Population- Cities, Towns and Urban Centres*. Retrieved March 9, 2020, from City Population- Statistics, Maps & Charts: https://www.citypopulation.de/en/kenya/cities

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.

Kothari, C.R. (2007). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Mumbai. New Age International Publishers.

Lasswell, H. (1948). Bryson, L. (ed.). *The Structure and Function of Communication in Society.The communication of Ideas.* New York: Institute for Religious and Social Studies. p. 117.

Lune, H., Pumar, E. S & Koppel, R. (Eds.) (2010). *Perspectives in Social Research Methods and Analysis*. Thousand Oaks, CA: Sage Publications, Inc.

Lwaitama, A.F. (1988). *Variations in the Use of Personal Pronouns in the Political Oratory of J.K. Nyerere and A.H. Mwinyi.* Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Lwaitama, A.F. (1995). *A Critical Language Study of Tanzania Kiswahili Presidential Political Oratory*. PhD Thesis, Birmingham Department of Modern Languages, Aston University inBirmingham, U.K.

Lyons, J. (1981). *Language and Linguistics: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mahshid, S. N. J. (2014). A Critical Discourse Analysis of Political Speeches of Four Candidates of Rasht City Council Elections in 2013, with a view to Fairclough Approach, *European Journal of Social Sciences, Vol.1, Issue 2.*

Martin, J.R. & Rose, D. (2003). *Working with Discourse- Meaning Beyond the Clause.* Open Linguistic Series. Continuum International Publishing Group Ltd. 296 paginas.

Mercer, N. (1997). *The Guided Construction of Knowledge.* Frankfurt Lodge: Multilingual Matters Ltd.

Mesthrie, R. (2000). *Introducing Sociolinguistics*. Edinburg: Edinburg University Press.

McCarthy, M. (2000). *Discourse Analysis for Language Teachers*.Cambridge: Cambridge University Press.

McLeod, S. A. (2019). *Likert Scale Definition, Examples and Analysis*. Simply Psychology. https://www.simplypsychology.org/likert-scale.html

Mogeni, D. (2009, February 5). Why Corruption Persists in Kenya. Daily Nation. Retrieved May 12, 2020, from http://www.nation.co.ke/oped/Opinion/-/440808/525272/-/42v0lp/-/index.html.

Mugenda, O. andMugenda, E. (1999). *Research Methods; Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts press.

Muinde, S. N. (2009).*Uamilifu wa Tonisho katika Sentensi za Kikamba*. Tasnifu ya M. A ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Musa, Y.S. (2015). *Uchanganuzi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere kwa Mkabala wa Nadharia ya Balagha.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Egerton.

Nesler, M. S., Aguinis, H., Quigley, B. M. & Tedeschi, J. T. (1993). The effect of credibility on perceived power. *Journal of Applied Social Psychology*. 23(17), 1407-1425.

Ngechu, M. (2004). *Understanding the Research Process and Methods. An Introduction to Research Methods.* Nairobi: Acts Press.

Ngure, A. (2020, March 4). *Ukumbi wa Lugha na Fasihi: Tamathali za Usemi katika Lugha ya Siasa*. Retrieved April 21, 2023, from Taifa Leo: https://taifaleo.nation.co.ke

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na Fasihi ya Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam:Tanzania Publishing House.

Obiero, O. B. (2017). *A critical Discourse Analysis of Donald Trump's Announcement Speech*. M.A. Thesis: University of Nairobi.

Odeo, 1. I. & Maina, G. (2008). *Fani ya Isimu Jamii Kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford Universtity Press.

Oduor R. (2009). *Lugha na siasa nchini Kenya 2005*. Unpublished PhD Thesis, Moi University.

Randy, A. (2021, April 2). *Hotuba ya Kisiasa: Sifa,Aina, Mada na Mifano*. Retrieved April 21, 2023, from Warbletoncouncil: https://sw.warbletoncouncil.org

Rajab, W. T. (2017). *Tathmini ya Mabadiliko ya Maana ya Msamiati wa Kiswahili katika Muktadha wa Kisiasa: Mifano kutoka katika Hotuba za Kampeni Uchaguzi 2015*. M.A Kiswahili-Isimu; Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Roberts, E. V. (19995). *Writing about Literature*. New Jersy: Prentice Hall, Englewood Cliffs.

Sarfo, E. and Krampa, E.A. (2013). Language at War: A Critical Discourse Analysis of Speeches of Bush and Obama on Terrorism. *In International J. Soc. Sci. and Education, Vol.3 Issue 2.*

Schilling, N. (2013). *Sociolinguistic Fieldwork*. Cambridge: Cambridge University Press.

Scotton, C.M. (1993). *Social Motivation for Code Switching- Evidence from Africa.* Oxford: Clarendon Press.

Sekyi-Baidoo, Y. (2002). *Learning and Communication*. Accra: Infinity Graphics Ltd.

Sovu, A. Y. (2018). *Mtindo Katika Hotuba za Rais J.P. Magufuli na Mchango wake katika Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili*. Mulika Na.37. Retrieved December 15, 2022, from https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/2482

Stubbs, M. (1983). *Discourse Analysis*. Oxford: Basil Blackwell.

Szanto. G. (1978). *Theatre and Propaganda*. Texas: University of Texas Press.

The Standard. (2019, July 23). *Arror and Kimwarer Dams Scandal in Details*. Retrieved January 03, 2022, from Standard Digital: https://www.standardmedia.co.ke

The Star. (2019, November 26). *Handshake Report*. Retrieved May 14, 2020, from Nine Key Issues BBI Addresses: https://www.the-star.co.ke.

The Youth Cafe. (2020, 09 18). *The Kenya's Corruption Journey- A 10 year Audit on Provisions in the Costitution on Leadership and Integrity in Curbing Graft*. Retrieved January 03, 2022, from Public Corruption, Leadership and Integrity: https://www.theyouthcafe.com

Thomas, K. (ed) (1971). *Attitudes and Behaviour*. Harmondsworth, Penguin Books.

Transparency International. (2019, July 11).*Corruption Perceptions Index 2019 - Kenya*. Retrieved February 16, 2020, from Transparency International-Kenya:https://www.transparency.org.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

University of Pittsburgh. (2019, November 11). *Types of Speeches*. Retrieved January 22, 2020, from Public Speaking-Oakland Campus: https://pitt.libguides.com.

Uvehammer, F. (2005). *The impact of English strategies in political debate: A linguistic Discourse Analysis of the first Bush and Kerry Presidential Debate, 2002*. PhD Thesis. Metropolitan State University.

Van Dijk, T. A. (1985). *Handbook of Discourse Analysis Volume 2*. New York: Academic Press.

Van Dijk, T. A. (1993). Principles of Critical Discourse Analysis. *In Discourse and Society. 4(2), 249-283.*

Van Dijk, T. A. (1997). What is political discourse analysis? *Belgian Journal of Linguistics.* 11(1): 11-52.

Van Dijk, T.A. (1998). *Principles in Critical Discourse Analysis in the Sociolinguistics. Gender and Discourse Volume2.* New York: Oxford University Press.

Van Dijk, T. A. (2006). Discourse and manipulation. *In Discourse & Society.17 (3).359-383.*

Van Leeuwen, T. (2008). *Discourse and practice: New tools for critical discourse analysis*. Oxford: Oxford University Press.

Verba, S., Schlozman, K. L., Brady, H., & Nie, N. H. (1993). Citizen Activity: Who Participates: What do they say*? In American political Science Review 87(2):303-318.*

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd. Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi Ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003b). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wanjugu, V. (2010) *Sababu na Athari za Ubadilishaji Msimbo Shuleni*: Utafiti katika Shule ya Upili ya Akiba. M, A Thesis. Chuo cha Nairobi.

Wanyama, K. J. L (2022). "Uyahe na Raghba ya Jinsia kama Mikakati ya Propaganda: Uchunguzi Kifani wa Mdahalo wa Urais wa Kenya, 2013." *In Journal of Social Sciences, Education and Humanities (JSSEH, 2022) Vol. 1:No. 1 ISSN 2791-190X* .

Warambo, J. P., Odero, E.O & Suleh, E. (2015). A critical Discourse Analysis of Funeral Speeches in Kenya: A case of Junior Odinga's Speech. *In Research in Humanities and Social Sciences. Vol.5, No.4, 2015.*

Webste's New World College Dictionary, Fifth Edition. (2018). *Definition of Speech*. Retrieved January 22, 2020, from Houghton Mifflin Harcourt Publishing Company web site: https://www.yourdictionary.com.

Wendell, V. H. (1992). *Dictionary of Concepts in Literary Critism and Theory*. New York: Greenwood Press.

Wilson, J. (2015). *Political Discourse.* In Deborah Tannen, Heidi E. Hamilton & Deborah Schiffrin (Eds.). The Handbook of Discourse Analysis (2nd ed., pp.775-794). Malden, Massachusetts: Blackwell Publishers Inc.

World Bank. (1997, September). *Helping Countries Combat Corruption*. Retrieved May 15, 2020, from The Role of the World Bank: https://www1.worldbank.org

Wrong, M. (2014, May 6). *Everyone is Corrupt in Kenya, even Grandmothers*. Foreign Policy. Retrieved June 15, 2021, from http://www.foreignpolicy.com/ articles/ 2014 /05/06/everyone_is_corrupt_in_kenya_even_grandmothers.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho I: Hojaji

**HOJAJI KUHUSU ATHARI ZA HOTUBA ZA KISIASA KUHUSU UFISADI KWA WANANCHI WA KENYA NA MIELEKEO YAO KUZIHUSU**

**UTANGULIZI**

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Ninafanya utafiti katika mji wa Mumias kuhusu athari ya hotuba za kisiasa kuhusu ufisadi kwa wananchi wa Kenya na mielekeo yao kuzihusu. Nina maswali machache kwenye hojaji hii yanayohusiana na mada hii. Tafadhali yajibu maswali yote kwa uwazi na kwa uaminifu. Habari zozote utakazozitoa zitawekwa siri na zitatumiwa katika utafiti huu pekee kwa dhamira ya kiusomi. Tafadhali usiliandike jina lako mahali popote katika hojaji hii.

**SEHEMU YA A: MAELEZO YA MHOJIWA**

1.0Tumia alama hii (√) katika kila jawabu mwafaka utakalolitoa katika maswali yafuatayo.

1.1 Una umri wa miaka mingapi?

Chagua kati ya A, B, C na D

A. Kati ya miaka 20 na 30 ☐
B. Kati ya miaka 31 na 40 ☐
C. Kati ya miaka 41-50 ☐
D. Zaidi ya miaka 50 ☐

1.2 Jinsia yako ni gani? kike ☐ kiume ☐

1.3 Kiwango cha elimu. Tia alama (√) kwenye kiwango chako cha juu kielemu.

A. Shule ya Msingi ☐
B. Shule ya Secondari ☐
C. Stashahada/ Diploma ☐
D. Digrii ☐
E. Uzamili(masters) ☐
F. Uzamifu (PhD) ☐

1.4 Unaishi sehemu gani ya mji wa Mumias?

______________________________________________

1.5 Je unafanya kazi gani?

---

**SEHEMU YA B: HOJAJI WAZI**

2.1 Je, wewe husikiliza hotuba za wanasiasa kuhusu suala ufisadi?

Ndio ☐ La ☐

Toa maelezo mafupi kuhusu sababu ya kusikiliza au kutosikiliza

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

2.2 Huwa unasikiliza hotuba hizi wapi?

Redio ☐ TV ☐ TV na Redio ☐ Mtandaoni ☐

2.3 Je umewahi kuhudhuria mkutano wao hata mmoja ambao walihutubia suala la ufisadi nchini Kenya?

Ndio ☐ La ☐

2.4 Je, kulingana na wewe, hotuba hizi huathiri vipi wafisadi?

Fafanua jawabu lako kwa kifupi

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

2.5 Je, iwapo ungekuwa na nia ya kujihusisha na matendo ya ufisadi, hotuba hizi za wanasiasa kuhusu suala la ufisadi zingeweza kukufanya ubadili nia yako?

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

2.6 Je, unaamini kuwa ni muhimu kwa wanasiasa kuendelea kuangazia suala hili katika hotuba zao? Eleza kwa nini?

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

2.7 Je, wanasiasa wakiacha kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao wewe kama mwananchi utahisi vipi? Fafanua jawabu lako kwa kifupi

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

2.8 Je, ni nini kinachokufurahisha au kukuudhi katika hotuba za wanasiasa kuhusu suala la ufisadi ?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

**SEHEMU YA C: HOJAJI YA LIKATI**

***Tafadhali yajibu maswali yafuatayo kwa kutia alama (√) panapofaa.***

| | Kauli | Nakataa kabisa | Nakataa | Sikubali wala kukataa | Nakubali | Nakubali kabisa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mimi husikiliza sana hotuba za kisiasa kuhusu suala la ufisadi. | | | | | |
| 2. | Je, ni muhimu kwa wanasiasa kuangazia ufisadi katika hotuba zao kila mara? | | | | | |
| 3. | Je, wewe hufurahia jinsi viongozi wa kisiasa huangazia suala la ufisadi katika hotuba zao? | | | | | |
| 4. | Je, unakubali kuwa madai yanayotolewa na wanasiasa katika hotuba zao kuhusu ufisadi ni ya kuaminika? | | | | | |

5. Unaamini kuwa hotuba za wanasiasa kuhusu ufisadi zimesaidia pakubwa katika vita dhidi ya ufisadi nchini?

6. Je, unaamini kuwa mafisadi huogopa wakati vitendo vyao vya ufisadi vinakashifiwa katika hotuba za wanasiasa?

7. Iwapo wanasiasa wataacha kuangazia suala la ufisadi katika hotuba zao visa vya ufisadi vitaongezeka?

**Kiambatisho II: Vibali vya Kufanya Utafiti**

**a) Kibali Kutoka Chuoni**

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 810901 Ext. 4150**

**Internal Memo**

---

**FROM:** Dean, Graduate School

**DATE:** 27th September, 2022

**TO:** **Felix Shimenga Mworeh**
**C/o Kiswahili Dept.**

**REF:** C50/CE/34020/2016

**SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

---

We acknowledge receipt of your revised Research Proposal as per our recommendations raised by the Graduate School Board of 20th June, 2022 entitled **"Pendekezo la Utafiti Uchanganuzi Linganishi wa Matini ya Hotuba za Kisiasa Kuhusu Ufisadi Kuanzia Mwaka 2015 Hadi 2020".**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking and Progress Report Forms per semester. The Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.

**ELIJAH MUTUA**
**FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL**

C.c. Chairman, Department of Kiswahili.

Supervisors:

1. Dkt. Bonface Ngugi
   C/o Idara ya Kiswahili
   **Kenyatta University**

*EM/lnn*

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

**P.O. Box 43844, 00100**
**NAIROBI, KENYA**
**Tel. 8710901 Ext. 57530**

**Our Ref:** C50/CE/34020/2016

**DATE:** 27th September, 2022

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR FELIX SHIMENGA MWOREH – REG. NO. C50/CE/34020/2016.**

I write to introduce **Felix Shimenga Mworeh** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili.**

**Felix** intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, **"Pendekezo la Utafiti Uchanganuzi Linganishi wa Matini ya Hotuba za Kisiasa Kuhusu Ufisadi Kuanzia Mwaka 2015 Hadi 2020."**

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHIBA KIMANI
AG. DEAN, GRADUATE SCHOOL

*EM/lnn*


**b) Kibali kutoka NACOSTE**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 315082 Date of Issue: 28/January/2023

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Felix Mworeh Shimenga of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kakamega on the topic: UCHANGANUZI LINGANISHI WA MATINI YA HOTUBA ZA KISIASA KUHUSU UFISADI KUANZIA MWAKA 2015 HADI 2020 for the period ending : 28/January/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/22491**

**315082**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**

Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
    i. Endanger national security
    ii. Adversely affect the lives of Kenyans
    iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
    iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
    v. Adversely affect the environment
    vi. Adversely affect the rights of communities
    vii. Endanger public safety and national cohesion
    viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke